

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Nane – Tarehe 20 Juni, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 76

Mpango wa Kurasimisha Ardhi Vijijini

MHE. PETER J. SERUKAMBA (K.n.y. MHE JENISTA J. MHAGAMA)
aliuliza:-

Mpango wa kurasimisha ardhi vijijini unakwama kwa kuwa Halmashauri nyingi zinashindwa kutenga fedha kutokana na ufinyu na ukomo wa Bajeti.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kutenga fungu la kuwezesha mkakati huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kurasimisha ardhi ni azma ya Serikali kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuondokana na umaskini. Mpango huu unalenga kupima ardhi za Vijiji na kuwapatia wananchi Hati za kumiliki za kimila (*Certificate of Occupancy*) ili kuzitumia kama dhamana kupata mikopo katika mabenki. Mkakati huu unatekelezwa chini ya Mpango wa Kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge nchini (MKURABITA).

Malengo mengine ya mpango huo ni kuondoa migogoro ya ardhi kwa kuweka mipaka kati ya vijiji na vijiji na kupanga matumizi bora ya ardhi kwa kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi bora na matumizi mbalimbali kama vile wafugaji, kilimo na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yenye dhamana ya masuala ya ardhi hutenga fedha kwa ajili ya kujenga uwezo katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali inao mfuko (*Revolving Fund*) unatumika kuziwezesha Halmashauri kupima ardhi na kufanya marejesho ili fedha hizo zitumike kwa ajili ya kupima ardhi katika Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo ni Halmashauri zilizonufaika na utaratibu huu kutorejesha fedha hizo kwa wakati. Uzoefu wa utekelezaji wa mpango huu umeonyesha kuwa kupima ardhi kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe baada ya kuwajengea uwezo kunapunguza gharama za upimaji. Halmashauri zimeshauriwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa azma ya kupima ardhi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Songea ni moja ya Halmashauri zitakazoingizwa kwenye mradi wa MKURABITA kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo. Mafunzo yamefanyika kwa watalaam kuanzia Wilaya hadi vijiji mwezi Mei, 2011. Aidha, Halmashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imefanikiwa kupima ardhi katika Vijiji viwili vya Mtyangimbole na Gumbiro kama vijiji vya mfano.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuendelea kupima ardhi ili kuiongezea thamani na kuwaondolea wananchi umaskini. (*Makofi*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpango wa kupima ardhi kwa ajili ya kurasimisha ardhi nchini ambao ni tatizo kubwa Peramiho ni tatizo kubwa kwenye Wilaya zote Tanzania. Siku likiulizwa swali uko mpango wa MKURABITA.

Ningeomba sasa Mheshimiwa Waziri ni lini Serikali itupe muda kwamba suala hili la kupima ardhi Tanzania ili kila mwenye ardhi nchi hii, kila mwenye nyumba aweze kuwa na *title deed* yake ili iweze kumsaidia katika kuondoa umaskini, tunataka sasa muda wa jambo hili kukamilika katika nchi yetu? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo, Mheshimiwa Stephen Wasira ndio anakaimu nafasi hiyo ya uongozi hapa ndani ya Bunge na MKURABITA iko chini yake.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Serukamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi najua kwamba ninapozungumza wewe ndio Mwenyekiti wa MKURABITA niko *conscious* kuhusu hii habari kinachozungumzwa hapa ni kuhusu hela. Kwa upande wa Halmashauri nimeeleza nikasema tatizo ambalo tumelipata sisi acha hiyo MKURABITA kwanza anayosema ni kwamba tumechukua hela katika Wizara ya Ardhi na hela hizi zilikuwa ni katika *Revolving Fund* hatukurejesha zile hela hela nyingi zinaonekana kwamba bado zimebaki katika Halmashauri.

Ninachosema hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaziagiza Halmashauri zote ambazo zimechukua hela kwa ajili ya kazi hiyo baada ya kuza viwanja wahakikishe kwamba hizo hela zinarudi ili ziweze kusaidia Halmashauri nyingi zaidi ziweze kufanya hivyo.

Pili, *source* ambayo inatumika kwa ajili ya kusaidia jambo hili na hii hapa baada ya Brazil alipokuja hapa akasema kwamba tuifanye ardhi badala ya kuwa na *use value* ipate kitu kinachoitwa *exchange value* ndipo tukasema mambo ya kuzika zika na kuweka nini sijui, nini tuangalie utaratibu maalum ambao unajulikana unazika watu mahali wanajulikana hapa kuifanya ardhi. (*Makofi*)

Mimi nilipokuja hapa nimezungumza na Mheshimiwa Stephen Wasira sina hakika sana na kiasi ambacho kimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Lakini mpango huu ni mpango wa Serikali ambao upo na kwa kiasi gani hela zimetengwa kwa ajili ya kuweza kutekeleza mpango wote kwa nchi nzima ni kitu ambacho siwezi kukisema kwa sasa hivi hapa kwa sababu sina jawabu hilo. Lakini namwomba Mheshimiwa Peter Serukamba, tuwasiliane tutafute *figure* na tujue kwamba ni lini kazi hii itakuwa imeanza.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo ya Halmashauri, ni kwamba hawana vifaa vya upimaji na vifaa hivyo ni vya gharama kubwa. Je, Serikali itakuwa tayari lini kuwanunulia Halmashauri zote vifaa ili watalaan walioko Halmashauri waweze wakapima ardhi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, pamoja na kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, naomba kutoa majibu kwa swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kama ifuatavyo:-

Mpango wa kurasimisha ardhi na mali ya Watanzania ambayo inaitwa ya wanyonge ni mpango mahususi unaosimamiwa na MKURABITA. MKURABITA wanao utalaam lakini hawana fedha ya kutosha kufanya kazi hii peke yao.

Kwa hiyo, ushauri ninaoweza kutoa hapa Bungeni ni kwamba kila Halmashauri ikiweza kutenga fedha kwa ajili ya kazi hii ya upimaji halafu MKURABITA wakawa watalaan ambao wanafundisha vijana kule kwenye Wilaya na vijana wale wawe wanafanyakazi hiyo na wanaweza wakawapa vifaa kama GPS kwa ajili ya kupima. Hii inaweza ikaharakisha mpango wa kupima ardhi na kuhakikisha ya kwamba inatumika kama *collateral* kwa ajili ya uchumi wa wananchi. (*Makofi*)

Vile vile ni jambo la msingi kwamba MKURABITA iwe inaweka Wilaya kadhaa kila mwaka kama ilivyo katika mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ili ikifika mwaka 2014/2015 tunaweza tukafanya tathimini tuone ni kiasi gani kwa ushiriki katika MKURABITA na Halmashauri tutakuwa tumeshafikia katika kupima ardhi. (*Makofii*)

Na. 77

Upandishwaji Hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo Mbina

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO aliuliza:-

Mheshimiwa Rais, katika ziara za kampeni za Uchaguzi Mkuu 2010 Mbina Mjini, aliahidi kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo Mbina kuwa Halmashauri ya Mji Kamili.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbina Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilitoa ahadi ya kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo Mbina, kuwa Halmashauri ya Mji. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, mamlaka ya Serikali za Mitaa huanzishwa kwa kuzingatia vigezo na taratibu ambazo zimebekwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo kuwa Halmashauri ya Mji ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuwa na idadi ya watu wasiopungua 30,000;
- (ii) Uwezo wa kujitegemea kwa asilimia hamsini kwa mapato yake ya ndani;
- (iii) Kuwa na huduma za jamii zifuatazo: Hospitali, shule ya Sekondari, Kituo cha Polisi na maduka ya rejareja yenyewe leseni yasiyopungua 50; na
- (iv) Eneo liwe Makao Makuu ya Tarafa.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kufuata kama ilivyo kwa maeneo mengine ya utawala ni mapendekezo kuanzisha/kupandisha hadhi kujadiliwa katika vikao vya kisheria ambavyo ni Baraza la Madiwani la Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) ili kupata ridhaa ya vikao hivyo ambavyo vinawakilisha wananchi.

Hivyo naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ianze mchakato wa kuwasilisha maombi kwa kuzingatia Sheria na taratibu zilizopo. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itakapopokea maombi hayo itafanya kazi kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na kwa kuzingatia ahadi ahadi ya Mheshimiwa Rais.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana majibu ya Serikali. Lakini wananchi wa Mbinga Mjini na Mbinga nzima kwa ujumla wamenitura pia kuishukuru Serikali kwa niaba yao hasa kwa utendaji mzuri wa Wizara hii ya TAMISEMI kupitia Waziri Mheshimiwa Mkuchika, Kassim Majaliwa na Mheshimiwa Aggrey Mwanri na hasa ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa alipofika kwa mara ya mwisho.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda kuzipokea salama hizi kule Mbinga?

(b) Kwa vile Serikali ilikwisha kutoa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbinga na kwa sababu kuna Wenyeviti wa vitongoji waliochaguliwa na hawajapata mafunzo kabisa na jambo hili mara kadhaa nimewahi kuongea na Mheshimiwa Mwanri?

Je, Mheshimiwa Waziri sasa yuko tayari kuwashakikishia viongozi hawa wa Mamlaka ya Mji Mdogo kwamba watapata mafunzo kwa haraka?

WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ningependa kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Gaudance Kayombo, kama ifuatavyo:-

Kwanza kwa niaba ya Wizara tunashukuru kwa pongeza alizotupatia katika utendaji katika Wizara yetu. Pili, mimi na Manaibu Waziri tuligawana Mikoa ya kwenda kukagua shughuli zetu na Naibu Waziri Majaliwa tulimpangia Mkoa wa Ruvuma. Baadaye tutababilishana. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge swalii hili alipouliza kwamba je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufika Mbinga kupokea pongezi hizo? Hakuna shughuli nitakayoifanya haraka kama hiyo. Kwa hiyo, nitakuja. (*Makofiki/Kicheko*)

Suala la mafunzo kwa viongozi katika Serikali za Mitaa kwamba ni kweli baada ya uchaguzi Waheshimiwa Madiwani, mwaka jana baada ya uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Vijiji mwaka mmoja kabla wengi wanahitaji mafunzo sisi tumejipanga hivyo

kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa na hii ni moja katika mambo ambayo itayafikia katika hotuba ya Wizara yetu.

MHE. NYAMBARI CHACHA MARIBA NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Waziri, kwa kuwa Wilaya ya Tarime ina Mamlaka ya Mji Mdogo wa Tarime na kwa kuwa vigezo ambavyo vimewekwa na Waziri kama alivyosema inaonekana Mamlaka ya Mji Mdogo wa Tarime inavikidhi vigezo hivyo vyote. Je, ni lini Serikali itapandisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Tarime kuwa Halmashauri ya Mji wa Tarime?

SPIKA: Swali zito namna hiyo unauliza kwenye nyongeza. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyangwine Mbunge wa Tarime kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema hapa ukiwa na Mamlaka ya Mji Mdogo maana yake ni kipindi cha mpito kuelekea Halmashauri ya Mji kinachofanyika pale ni kuhakikisha tu kwamba watu hawajengi ovyo ovyo bila kupimwa na vitu vingine.

Kama nilivyojibu hapa nilipokuja najibu swali la Mheshimiwa Gaudance Kayombo Halmashauri ikifika mahali ikaona kwamba sasa wamefika katika hatua hiyo inayozungumzwa na yeye anasema hapa na bahati nzuri mimi nimetokea Tarime, ni kweli inafanana, ukichukua Hotuba ya Mheshimiwa Ngwilizi, ukiangalie mle ndani anazungumzia hiki ninachokisema hapa kwamba Halmashauri ikifika mahali ikaona kwamba inakidhi hivyo vigezo vyote tunavyovizungumza ituletee.

Lazima wapitishe katika Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa ili sasa sisi wote kwa pamoja tuweze kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba hiyo, inakuwa Halmashauri ya Mji Kamili. (*Makofit*)

Baada ya hapo sasa inakuwa ni Bajeti kamili kwa maana ya Halmashauri ya Mji.

Na. 78

Mitambo ya Kusukuma Maji Ukerewe

MHE. PROF. MAHIGI (K.n.y. MHE. SALVATORY NALUYAGA MACHEMULI) aliuliza:-

Wilaya ya Ukerewe imezungukwa na maji kwa asilimia 90 na Serikali kwa kulitambua hii ilifanikiwa kuweka mitambo ya kusukuma maji katika Vijiji vya Nansio,

Chabilungo, Gallu, Ihebo, Bukonyo, Bukindo, Bwisya na Irugwa lakini mitambo hiyo yote haifanyi kazi ukiacha ule ulioko Nansio.

Je, ni lini Serikali itashughulikia mitambo hiyo ili ifanye kazi na kuwaondolea wananchi adha na kero kubwa ya maji walijonayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salvatory Machemuli, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ukerewe ina jumla ya miradi tisa (9) ya Bomba ukiwemo mradi wa Maji Nansio. Hata hivyo ni kweli kwamba miundombinu ya maji katika miradi hiyo ni chakavu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe iliingia Mkataba na Mtaalam Mshauri *COWI Tanzania Ltd.* Kwa ajili ya kufanya shughuli za usanifu na uhamasishaji wa miradi ya maji. Ushauri uliotolewa ni matumizi ya teknolojia rahisi ya kuchimba visima vya maji katika vijiji vyote kumi na tatu vyenye matatizo ya maji kutokana na gharama kubwa za kurudishia mabomba mapya. Kazi hii imekamilika kwa hisani ya Benki ya Dunia ambapo katika mwaka 2010/2011 zilitengwa shilingi milioni 495.5 kwa kazi hiyo, Sababu kubwa zilizosababisha kuchagua teknolojia hiyo ni gharama nafuu za ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi bilioni 1.4 fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa Kazilankanda utakaohudumia vijiji kumi na tatu vilivyopewa kipaumbele kwa awamu ya kwanza.

Kazi zitakazofanyika ni kupata mkandarasi kuweka pampu za maji, matanki ya maji, kuchimbia mabomba ya maji na vituo vya kusambazia maji. Sambamba na ujenzi wa mradi wa maji Kazilankanda, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan - *JICA* inajenga miradi miwili katika vijiji vya Bukonyo visima virefu 2 na Namilembe visima virefu 3.

Mheshimiwa Spika, shughuli za ujenzi wa miundimbinu ya maji zinategemewa kuanza mwezi Agosti, 2011 mara baada ya kupata mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji.

MHE. PROF. MAHIGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

- (i) Je, miradi aliyoitaja Naibu Waziri itaanza kutekelezwa lini na itakamilika lini?

- (ii) Kwa kuwa matatizo ya Ukerewe kuhusu kero kubwa ya maji walionayo wananchi wa Ukerewe yanafanana na yale yanayowakabili watu wa Bukombe ni lini Serikali itaanza kushughulikia miradi ya maji kwa ajili ya wananchi wa Bukombe?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Professor Mahigi, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa kuhusu miradi hii inayozungumziwa kule Nansio Ukerewe, miradi hii ndiyo ile tunazungumzia habari ya *quick wins* na huko anakozungumzia, mimi nimekwenda mpaka kule nimeona kabisa hicho. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge ana-*impose* kuna tatizo la mji kule Nansio, ni kweli tumekwenda kwenye kile kisiwa, ni kitu cha ajabu kwamba unaona wamezungukwa na maji pale.

Hawana maji pale kwa sababu yale mabomba yanayozungumzwa hapa ni chakavu, sasa katika jibu hili ambalo nimelitoa hapa, tunesema kwamba shughuli zote hizi kwa sababu na *World Bank* wanakuja kule wanaaadid, shughuli zote zimeshakamilika sasa tunategemea kwamba kwenye mwezi August ndiyo tunategemea kwamba kazi hiyo itakuwa imeanza kwa shughuli hizo za ujenzi. *Otherwise mambo ya fysibility study* na vile vitu vya *design* kila kitu kimekalimika.

Mimi nimekwenda Bukombe mpaka kule Usiombo. Nafahamu kabisa kwamba kuna matatizo ya maji pale, sasa kwa vile nilikuwa sijajiandaa kwa ajili ya hilo eneo, mimi naomba Professor uje tu tukae wote kwa pamoja twende tukaangalie ile miradi, nisije nikajikoki hapa halafu ukarininginia tena ukaanza kusema wewe ulituambia hivyo. Naomba niende nikaangalie vizuri halafu baadaye tutasaadia na nina hakika kwamba Professor Mwandsya pamoja na ndugu yangu Naibu Waziri wanafahamu hilo, tutakwenda kuangalia hilo. (*Makofii*)

MHE. REGIA E. MTEMA: Mhehsimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Kilombero ni mionganoni mwa Wilaya zinazofaidika na mradi wa maji wa Benki ya Dunia, lakini mpaka hivi sasa miradi hiyo inasuasua, tunaambiwa fedha ziko benki, lakini haijaanza na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri ameshafika Wilayani Kilombero.

Je, unawaeleza nini wananchi wa Kilombero au Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kwa kadri fedha zinavyozidi kukaa benki ndiyo *purchasing power* ya fedha hizo inapungua, matokeo yake mwisho wa siku fedha hizo hazitaweza kukamilisha mradi?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hili swali nalo ni jipya, litakuwa kama lile la Profesa Mahigi, labda wewe unajua kila majibu, jibu. Ni jipya ni *very specific* sio rahisi kujibiwa vizuri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Regia Mtema, kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema Mheshimiwa Spika, mimi eneo hili nimelifika, tumeliona na kuna matatizo haya yanayozungumzwa hapa. Sasa labda nieleze kwa sababu hili swali linaulizwa na watu wengi na Wizara ya Maji tumekuwa tunawasiliana nao kwamba miradi yote ile ya *quick wins* ambayo imepelekwa kule, hela nyingi ukiangalia, hata ukiangalia ile taarifa ya CAG inaonyesha kwamba kuna hela nyingi sana ambazo hazijatumika sasa hivi kwa sababu ya utaratibu ule ambao umekubalika kwa maana ya urasimu ambao umejengeka pale, mpaka wapate no *objection* na vitu vingine kama hivyo. Ni *genuine* kabisa tunaliona na *that is why* imetokea kwamba Wizara ya Maji imeamua kuunda kitengo maalum ambacho kitaratibu hii mipango yote ya maji kwa maana ya hii miradi tunayoizungumzia hapa.

Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hili tunaendelea kushirikiana na wenzetu ili tupunguze. Hiki anachosema kwamba kuna hela nyingi sana zinaonekana kwamba zimekaa kwenye benki, ni kweli, lakini sasa hivi Wizara ya Maji kwa kushirikiana na sisi tutafanya kazi hiyo ili kuhakikisha kwamba tunaondokana na hilo tatizo. Wanaoratibu kuna kitengo kimeanzishwa pale kwa ajili ya kazi hiyo. (*Makofi*)

Na. 79

Huduma zitolewazo na Makampuni ya Simu

MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA aliuliza:-

Makampuni ya simu za mkononi yamewekeza katika maeneo mengi na hususan Vijijini na mara nyingi katika majukumu wanayotekeleza ni kusaidia huduma za jamii:-

(a) Je, ni kwa nini huduma hizo zinatolewa mijini badala ya vijiji ambako kuna hitaji zaidi?

(b) Je, kuna mkakati gani wa kuwa na mikataba inayowiana ili kuwezesha hata Serikali za vijiji kupata pato sawa na mikataba iliyosainiwa katika maeneo ya mijini ambako kuna watalaan wengi wa kisheria?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutambua na kupongeza juhudhi mbalimbali za makampuni ya simu nchini katika kusaidia shughuli mbalimbali za jamii na hata kutoa misaada mbalimbali pale panapokuwepo na wahanga wa majanga mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, makampuni ya simu hutoa huduma za jamii katika maeneo yote ya mijini na vijijini lakini zaidi kuzingatia maombi ambapo vigezo mbalimbali hutumika katika kuchuja maombi ikiwa ni pamoja na kuangalia namna ambayo msaada utafaidisha jamii husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumsihi Mheshimiwa Mbunge kuwa pale anapoona kuna haja ya kuhusisha makampuni ya simu kushiriki katika kutoa huduma za jamii katika maeneo mengine hasa ya vijijini basi maombi hao yanayohusikayapelekwe moja kwa moja kwa kampuni husika ili iweze kuona namna inavyoweza kusaidia.

(b) Mheshimiwa Spika, makampuni ya simu huingia katika mikataba ya upangishaji kwa kutegemea makubaliano yanayofanyika na mpangishaji ambapo maafikiano ya kiwango cha tozo huzingatia pato linatarajiwa kupatikana kutoka katika mnara wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kuititia Wizara yangu tayari imeratibu marekebisho ya sheria ya mawasiliano na kuwezesha kuwepo kwa sheria mpya ya mawasiliano ya kielektroniki na posta ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Januari, 2010. Kanuni za Sheria hiyo mpya zinazotarajiwa kukamilika sasa hivi zinaweka uwiano katika mikataba yote inayohusu masuala yote ya mawasiliano katika maeneo yote nchini.

MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa katika jibu la msingi, Mheshimiwa Waziri amesema kuna vigezo mbalimbali ambavyo vinatumika katika kuchuja na kuchambia haya maombi. Je, yuko tayari kulieleza Bunge hili ni vigezo gani vinavyotumika?

(ii) Kwa sababu amesema Wizara imepitia Kanuni na sheria ambazo zitarekebisha hii mikataba iliyokuwepo, haoni kwamba sheria hizi zimechelewa kwa sababu katika Jimbo langu sasa hivi kuna Vijiji vya Katahoka na Nyalukongo kuna minara ambayo haijalipa ushuru kwa muda wa miaka miwili?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoleza katika jibu langu la msingi, vigezo vinavyotumika katika kuamua ni huduma gani ya jamii iweze kutolewa katika eneo husika, uzingatie zaidi mahitaji ya wananchi eneo hilo. Kwa hivyo, vigezo vinatofautiana kati ya eneo na eneo kwa sababu watu kama wamepata majanga ya aina tofauti huwezi ukapeleka huduma inayofanana na watu waliopata tatizo katika eneo fulani au ombi katika eneo jingine.

Katika swali lake la pili anazungumzia kwamba sheria imechelewa, hapa sheria haijachelewa sana, sheria ilipitishwa mwezi Januari 2010 na Rais akaridhia, lakini ili uweze kuitumia hiyo sheria, unatengeneza Kanuni zake na Kanuni zinapitia katika mchakato, sasa hivi Kanuni hizi ziko kwa wadau, wanazipitia ili kuhakikisha kwamba zinakubaliana na yale wadau wote wanayaona ni sahihi katika kutekeleza sheria hiyo.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa makampuni haya ya simu yanapojenga minara mbalimbali katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya mawasiliano inategemea kupata shilingi kama milioni 10 kwa mnara mmoja kwa mwaka.

Je, Serikali haioni kwamba zinaangalia zaidi biashara kuliko kutoa huduma kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, makampuni haya yanafanya biashara, lakini biashara hiyo yanayofanya yana ushindani, ndiyo sababu tumeshuhudia kushuka kwa gharama za mawasiliano sana katika kipindi hiki kifupi na zaidizaidi vilevile tunaona makampuni haya yanashiriki katika huduma za jamii, (*corporate social responsibility*, kama yangekuwa yanajali biashara tu, ni kweli yasingekuwa yanajihuisha katika hili suala la *corporate social responsibility*, lakini labda nizungumzie hili suala la malipo ya minara kwa sababu nimelipata katika sehemu mbalimbali.

Malipo yanayotolewa na makampuni haya ya simu katika kupangisha minara pale ambapo wanaweka na wananchi, yanazingatia zaidi mkataba unaoingiwa kati ya kampuni husika na wenyeji au wale wanaohusika na eneo hilo.

Kwa hivyo, mkataba ule unapashwa uonyeshe ni malipo ya kiasi gani na yatalipwa wakati gani, sasa kama kutakuwa na kutolewana katika kulipa, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge wawasiliane na Wizara yetu ili tuone namna ambavyo tunaweza kushirikiana na kuhakikisha kwamba mikataba hiyo inafuatwa kama ilivyoingiwa.

Mawasiliano ya simu Jimbo la Kondo la Kaskazini

MHE. ZABEIN M. MHITA aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Kondo la Kaskazini wanakosa fursa ya kupanuka kwa teknolojia ya habari kutokana na kutokuwa na mitandao ya simu katika sehemu nyingi.

Je, Serikali itawapatia lini mawasiliano ya simu wananchi wa Kata za Kingale, Suruke, Serya, Hondonario, Changea, Thawi, Soera, Kikilo, Busi na nyinginezo ili nao watumie teknolojia hiyo kwa maendeleo yao?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondo la Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo yote nchini. Hata hivyo, asili ya Kijiografia ya maeneo mbalimbali, idadi ndogo ya wananchi katika maeneo husika kutowiana na gharama kubwa za kuwekeza mitambo ya mawasiliano, uhaba wa miundombinu ya barabara na nishati ya kutosha yenye gharama nafuu kwa ajili ya kuendeshea mitambo ya mawasiliano imekuwa kikwazo kikubwa kwa kampuni ya simu kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo nilizolezea, Serikali inaendelea kuhimiza makampuni ya simu nchini kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote kuhakikisha kuwa ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013 zaidi ya asilimia tisini ya Watanzania wote wawe wamefikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo, Mfuko wa Mawasiliano tayari umeainisha jumla ya vijiji kumi na moja (11) vyenye eneo la ukubwa wa kilometra za Mraba 1,793 katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Airtel* imeyaweka maeneo haya kwenye mpango wake wa tathmini yakinifu katika mhula wa nne wa utafiti kwa mwaka 2011 ili hatimaye kuweza kuwapatia Mawasilaino ya simu wananchi wa Kata za Kingale, Suruke, Serya, Hondonario, Changea, Thawi, Soera, Kikilo, Busi na nyinginezo ili nazo watumie teknolojia hiyo kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya simu ya *Zantel* imeahidi kupanua mtandao wake kuititia miundombinu ya kampuni nyingine ili kufikisha na kuboresha huduma ya mawasiliano katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge. Aidha, Kampuni ya simu *Tanzania TTCL* tayari imeahidi kuyaweka maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge katika mpango wake wa mwaka 2011-2013 ambao utekelezaji wake unategemea

upatikanaji wa fedha pamoja na kutumia fursa za mfuko wa mawasiliano ili kuweka minara na kufikisha mawasiliano katika Kata alizozitaja Mheshimiwa Mhita.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kwa mpango thabiti ambao unaonyesha kwamba wananchi watapatiwa huduma hiyo.

Kwa kuwa katika jibu lake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna mpango ambao kutafanyika tathmini yakinifu na hatimaye wananchi waweze kupatiwa mawasiliano hayo.

Je, baada ya hii tathmini ni lini basi wananchi hawa wa Kata nilizozitaja wataweza kupata mawasiliano ya simu za mkononi? (*Makofi*)

Katika jibu la Mheshimiwa Waziri amesema kwamba ametaja zile Kata nilizozitaja na nyinginezo kwamba zitapatiwa mawasiliano hayo. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri katika Kata nyingine naomba Kata zifuatazo nazo waweze kuzifikiria. (*Makofi*)

SPIKA: Hapana zinatosha hizo Kata, muda hautoshi, unataka Jimbo lote lipewe huduma ya simu ndiyo hivyo anavyosema. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhita, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mhita amekuwa akija ofisini kwangu na nilipofika hapa amekuwa akikumbushia maombi yake.

Ninapenda kumjibu tu kwamba kama nilivyojibu katika swal la msingi, tunajipanga, Serikali hii iko makini na imejipanga kuhakikisha kwamba kufikia mwisho wa mwaka 2013 zaidi ya maeneo mengi sana kufikia zaidi ya asilimia 90 yatakuwa yamepata mawasiliano hayo. Tunatambua umuhimu wa mawasiliano na tutahakikisha kwamba tunatekeleza hilo. (*Makofi*)

Pamoja na majibu hayo, amesema je, Kata zingine vipi? Nimhakikishie tu kwamba yawezekana hata ile minara itakayowekwa kwa sababu minara hii inapowekwa *under normal circumstances* inakwenda kilometra 35 yawezekana ziko karibu yakawa yamefikiwa. Lakini kama nilivyosema pamoja na zingine yawezekana zile ambazo sikuzitaja zikawa na zenyewe zimo katika mpango huu.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, kwa sababu sheria ya fedha ya Halmashauri za Wilaya nchini ya mwaka 1982 inayapa Mamlaka za Wilaya uwezo wa kutoza 0.3% ya mapato ya makampuni mbalimbali yanayoendesha biashara katika eneo la Wilaya ikiwepo Makampuni haya ya simu na kwa sababu makampuni

haya ya simu mengi ofisi zake ziko Dar es Salaam na kwa kuwa makampuni haya yamesambaza huduma katika Halmashauri mbalimbali na majiji mbalimbali katika Taifa.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuziwezesha Halmashauri za Wilaya kutoza kodi inayohusika kwa kuweka utaratibu ambapo mapato ya makampuni haya yatajulikana kupitia minara yake badala ya kupitia kwenye ofisi zao za Taifa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliiano, Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbewe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Serikali ilipoweka mpango wa kutoa ruzuka katika Halmashauri mbalimbali, ilizingatia kwamba mapato yanatofautiana kutoka Wilaya moja hadi nyingine.

Sasa tukisema kwamba Wilaya fulani ambapo kuna mnara au kuna chanzo cha mapato kiasi fulani, yawezekana Wilaya zingine ambazo hazina bahati ya kuwa na mnara zikakosa kabisa. Lakini kwa sababu Serikali inatambua hilo, ndiyo sababu inakusanya mapato yote na kisha kutoa ruzuku katika Halmashauri kama ambavyo inafanya sasa hivi. (*Makofi*)

Na. 81

Ujenzi kwa Kiwango cha Lami Barabara ya Isyonje- Makete

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuliza:-

Barabara ya Isyonje hadi Wilaya ya Makete ni kiunganishi muhimu kati ya Mbeya na Wilaya hiyo na pia barabara hiyo hupitia katika hifadhi ya Taifa Kitulo ambayo watalii wengi hutembelea.

Je, ni lini Serikali itaijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwajale, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa fedha, Serikali kwa sasa haiwezi kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali kupitia wakala wa barabara imekuwa ikifanya matengenezo ya aina mbalimbali katika barabara hii. Kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007 hadi 2010/2011 jumla ya shilingi milioni 773.01 zimetumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo. Serikali itaendelea kuiimarishe barabara hii kwa kutenga Bajeti kwa ajili ya kuikarabati na kuifanyia matengenezo kila mwaka ili iweze kupitia majira yote ya mwaka.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Barabara Isyonje mpaka Makete ni barabara muhimu sana kiuchumi katika kanda ile na kwamba Kitulo ndiko kwenye Hifadhi ya Taifa, na kwamba mimea ya aina yake duniani inapatikana pale. Lakini pia milima ya Livingstone ambayo watalii wengi sana hupenda kutazama na kuangalia kule na kutembelea inapatikana kule. Lakini asilimia karibu 95 ya maziwa yanayozalishwa katika shamba la Mifugo la Kitulo yanasa firishwa kupelekwa Mbeya kwa kuititia barabara ile na hapo hapo kiwanja cha ndege cha Songwe kinajengwa tayari kupokea watalii amba bila shaka watatamani kwenda kuangalia ile milima.

Je, Serikali haioni udharura wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kuongeza pato kwa taifa?

Swali la pili, jibu la msingi ambalo Mheshimiwa Waziri amesema ni kwamba barabara hii inatumia karibu milioni 700 kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara.

Je, haoni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kutengeneza barabara hiyo kwa lami ili kuepuka gharama ambazo kila wakati wamekuwa wakitumia mamilioni ya mapesa kutengeneza barabara hiyo? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumhakikishia tu kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa barabara hii kutoka Mbeya-Isyonje-Kikondo, siyo tu kwa sababu ya utalii katika hifadhi ya Taifa ya Kitulo na vile vile shughuli za maendeleo zilizoko pale.

Serikali inatambua vilevile eneo hilo lina utajiri mkubwa sana wa mazao ya biashara na chakula. Lakini vile vile barabara hii inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Njombe na Mkoa wa Mbeya amba ni hoja ya msingi kabisa. Vile vile ni barabara fupi sana kwa wananchi wa Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ukitoka Mbeya kuelekea Makete kuititia Makambako ni kilomita 352. Lakini ukitokea Mbeya kuelekea Makete kuititia Isyonje-Kikondo ni kilomita 125. Kwa hiyo, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii. Lakini kama nilivyosema ni kutokana tu na upungufu wa pesa. Kupanga ni kuchagua tutakapopata pesa za kutosha tutajenga barabara hii kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Samahani Mheshimiwa Spika, nilisahau kipande cha pili cha swali lake.

SPIKA: Niliona inafanana lakini. Haya jibu kama una majibu tofauti.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika nilisahau, sehemu ya pili ya swali lake ilikuwa ni kuhusu gharama za ukarabati wa barabara za changarawe ni mkubwa mno. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge. Ningependa tu kusema kwamba hata Serikali kwa kweli sasa hivi azma yake kubwa ni kugeuza barabara zote za udongo na za changarawe kuwa za lami na ndiyo maana sasa hivi tunajenga barbara nyingi na zenye urefu mkubwa wa kilomita 11,300 nafikiri ni kiwango ambacho

hakijawahi kufikiwa katika historia ya nchi yetu, kwa sababu mwaka 2005 Serikali ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani tulikuwa tumejenga barabara za lami za kilimita 6,500 na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuongeza Bajeti. Ongezeko dogo kila mwaka la Bajeti ya Wizara hii ingawaje haitoshelezi na kwa sura zenu ninavyoziona tu kabisa mko tayari kutuunga mkono pia mwaka huu 2011. Ahsante sana.

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupewa nafasi hii ili niulize swal la nyongeza. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii ambayo inapita kwenye hifadhi ya *Kitulo* (*Kitulo National Park*) na inapita kwenye shamba la ng'ombe la Kitulo na pia inapita kwenye Milima ya Lingstone na mradi mkubwa wa kufufua umeme wa Mto Rumakariya na kwa kuwa ni barabara hii iliyoulizwa kwenye kikao cha kwanza cha mkutano huu, ambayo inaunganisha Mkoa wa Njombe-Ruvuma na Mbeya kwa kupitia Wilaya za Ludewa na Makete.

Kikao cha Mkoa cha Barabara kiliazimia kilichofanyika tarehe 17Mei, 2011 kwamba barabara hii upo umuhimu wa kujengwa kwa kiwango cha lami na maombi yake yatapelekwa Wizara ya Ujenzi. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kwa kuzingatia umuhimu huu ambaa umeonekana kimkoa kuharakisha ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nimeshatamka kwamba Serikali inatambua kabisa umuhimu wa barabara hii na kama Serikali hatuoni umuhimu wa barabara hii kutoka tu kipande cha Isyonje kwenda Makete. Lakini tunaona umuhimu wa barabara nzima kutoka Njombe kuja Makete mpaka Isyonje na naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama yeze anavyojua tumeshaanza ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya Njombe kuja Makete kama ambavyo ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Tayari tumeshaanza kujenga sehemu korofi, tumejenga kilomita 12 za lami sehemu korofi. Tunaendelea kutenga pesa na kufikia mwaka 2015 ambapo tutaweza kupimwa kuhusu utekelezaji wa Ilani itakuwa tumeshaikarabati hiyo barabara pamoja sasa kuunganisha barabara ya kutoka Makete kuja Kikonde kwenda Isyonje. (*Makofi*)

Na. 82

Hitaji la barabara ya lami inayounganisha Mji wa Mbulu na Babati

MHE. MARTHA J. UMBULLA aliuliza:-

Wilaya ya Mbulu haina barabara yoyote ya lami inayoiunganisha na Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara, yaani Babati, wala njia zozote za kiuchumi kuelekea Arusha, Singida au Dodoma.

Je, Serikali inakubali kwamba ni wakati muafaka sasa wa kujenga angalau barabara moja ya lami itakayouniganisha Wilaya hii na soko la Babati, Arusha au kwingineko ili kuwapa wakulima ari ya kuzalisha zaidi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inalitambua tatizo hilo na kwa sasa inatekeleza ujenzi wa barabara kuu ya Singida-Babati-Minjingu yenyeye urefu wa km 224 kwa kiwango cha lami. Pia kazi zinaendelea za ujenzi wa barabara kuu ya Babati-Kondoa-Dodoma. Zote hizi zikiwa ni jitihada za kuwezesha mkoa wa Manyara ulioanzishwa mwaka 2002 ukiwa na changamoto kubwa za miundombinu ya barabara za kuunganisha Mkoa huu na Mikoa mingine kwa barabara za kiwango cha lami. Pia kuunganisha mji wa Babati na Makao Makuu ya Wilaya zote za Mkoa wa Manyara kwa barabara za kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, kwa azma ya kuunganisha mji wa Mbulu na Babati, barabara za kiwango cha ngangarawe za Mbulu-Dongobesh-Dareda-Babati na Mbulu-Mbuyu wa Mjerumani-Babati zimekuwa zikitengenezwa na kuitika wakati wote. Aidha, kwa ajili ya usafirishaji wa mazao ya kilimo kutoka Mbulu hadi Babati, barabara ya Mbulu-Dongobesh-Dareda-Babati imeboreshwa kwa kujengwa kwa kiwango cha lami kilometra 7 katika milima ya Dabil, iliokuwa awali ni kikwazo kikubwa kwa sababu ya vilima vikali na utelezi wakati wa msimu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kujenga barabara za lami kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote. Baada ya barabara hizo kukamilika, hatua itakayofuata ni ujenzi wa barabara za lami kuunganisha barabara za Mikoa na Makao Makuu ya Wilaya ikiwamo barabara ya Mbulu-Dongobesh-Dareda. Hata hivyo, utekelezaji wa azma hiyo ya Serikali utategemea kama kawaida upatikanaji wa fedha.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kupata nafasi hii. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa majibu yake ni ya muda mrefu kwa mfano barabara ya kutoka Babati-Kondoa-Dodoma haitachukua chini ya miaka mitano, sita na zaidi na vile vile barabara ya Babati-Hanang-Katesh na Singida pia itachukua muda mrefu na kwa kuwa Serikali katika mpango wake umedhamiria vizuri sana kukuza uchumi na ajira kwa Watanzania wote ndani ya muda wa miaka mitano na hata katika Bajeti yetu hii ya mwaka 2011/2012 imedhamiria vile vile kukuza uchumi na ajira kwa Watanzania.

Je, barabara zinazounganisha Wilaya ya Mbulu na njia kuu za uchumi, Serikali itakuwa na mpango upi wa dharura ili wananchi hao wasiachwe pemberi na mipango hii ya miaka mitano na Bajeti hii katika kukuza ajira na kukuza uchumi ili nao wasiachwe pemberi katika hii dhamira nzuri ya Serikali? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Mkoa wa Manyara ni Mkoa mpya ambao umekuwa na changamoto kubwa ya msingi ya kutokuunganishwa na Mikoa mingine kwa barabara za uhakika. Sasa hivi Serikali ndiyo imeanza kwa ujenzi wa barabara ya uhakika ambayo inatokea Minjingu kuja Babati kuitia miji muhimu kabisa Mkoa wa Manyara, Dareda, Katesh mpaka Singida. Hiyo yote ni mchango wa Serikali kwa ajili ya kufungua fursa za Mkoa wa Manyara. Lakini vile vile tuna barabara kutoka Babati kuja Dodoma moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba barabara itachukua muda mrefu miaka sita. Sijui kama hayo mawazo yake yanatokana na ushauri wa wataalam. Lakini mimi nimetoka kukagua barabara hiyo jana tena, barabara inaendelea vizuri. Tutakamilisha katika kipindi cha Ilani tulichosema cha miaka mitano. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

MHE. JITU V. SONI: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika barabara aliyoitaja ambayo inaunganisha Babati na Mbulu ya kuitia Magara. Mbulu-Magara-Babati kuitia Mbuyuni kuna daraja ambalo iliahidiwa na Mheshimiwa Rais na Wizara ilishatenga fedha kiasi fulani.

Htuoni kazi yoyote inayofanyika katika daraja hilo la Mto Magara ambao kipindi cha masika hapapitiki na pia kuitia Dongobesh-Mbulu barabara ya Mbulu-Dongobesh-Babati kuna maeneo korofi ambayo kipindi cha masika Mbulu inakuwa kama kisiwa.

Sasa Serikali inaona umuhimu gani wa kuhakikisha yale maeneo korofi yanashughulikiwa angalau vile vipande vibaya viwekwe kwa kiwango cha lami na hilo daraja ili wananchi wa Mbulu wasipate shida?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua kuhusu ujenzi wa daraja la Mto Magara kwenye barabara ya Mbulu hadi Mbuyu wa Mjerumani. Katika mwaka wa fedha unaoisha sasa, tulikuwa tumetenga pesa kidogo shilingi milioni 450 ambazo zisingetosha kabisa kujenga hilo daraja.

Lakini katika mwaka huu wa fedha unaokuja ambao tunaombea pesa tumeomba pesa nydingi za kutosha. Siwezi kutaja kiwango kwa sababu tutakuwa tunawapa faida makandarasi wanapokuja ku-*bid* kwenye hiyo tenda.

Psa ya kutosha kabisa kujenga hilo daraja, ningeomba Mheshimiwa Mbunge siku ambayo tutakuwa tunatoa Bajeti yetu awepo kuweza kutuunga mkono hilo daraja liweze kujengwa na vile vile kuhusu barabara za ndani katika mkoa wa Manyara tuna Bajeti ya kutosha ambayo tumeshaiwasilisha katika Ofisi yetu ya Wakala wa Barabara.

Mheshimiwa Mbunge kama angependa ningemshauri anione ili nimweleweshe ni kiasi gani cha pesa tulizonazo kwa ajili ya ukarabati wa barabara zote ndani ya Mkoa wa Manyara.

Kuteuliwa *Deputy Commissioner* wa Polisi Zanzibar

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR aliuliza:-

Kwa zaidi ya miaka sita sasa nafasi ya *Deputy Commissioner* wa Makao Makuu ya Polisi Zanzibar ipo wazi na kazi zake zinatekelezwa na askari wenye vyeo vya chini:-

- (a) Je, kwa nini hadi hivi sasa uteuzi wa *Deputy Commissioner* haujafanyika?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inawavunja moyo askari na inaweza kupunguza ufanisi wa kazi?
- (c) Je, ni lini *Deputy Commissioner* huyo atateuliwa?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uteuzi wa Naibu Kamishna Zanzibar hakuweza kufanyika mapema kwa sababu Wizara yangu ilikuwa katika mchakato wa kuyafanyia mapitio majukumu na muundo wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hivi sasa mchakato huo umekamilika na muundo mpya wa Wizara uliidhinishwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 9 Oktoba, mwaka uliopita.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haioni kwamba kutojazwa kwa nafasi hiyo ya Naibu Kamishna kunawavunja moyo askari kwa sababu Jeshi la Polisi lina taratibu maalum za kuwapandisha vyeo maafisa wake.

(c) Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Naibu Kamishna atateuliwa mara baada ya kupitia majina ya maafisa watakaopendekezwa kushika nafasi hiyo kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara na kwa vyovoyote vile suala hili halitarajiwi kuchukua muda mrefu kutoka sasa.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Spika, pamoja na jawabu zuri la Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, muundo huu wa Wizara umetiwa sahihi na Mheshimiwa Rais toka tarehe 9 Oktoba, 2010.

Je, mpango huu umeshaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, umelenga kuboresha vipi Jeshi la Polisi? Ahsante sana. (*Makofit*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba muundo huu na majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, iliidhinishwa na Mheshimiwa Rais, Oktoba mwaka uliopita. Lakini uteuzi wa nafasi hizi za juu katika Jeshi la polisi kwanza unafanywa kwa kuzingatia mambo muhimu matatu.

Kwanza unazingatia nafasi zinazohitajika kujazwa.

Pili, unazingatia masharti ya hiyo nafasi ambayo inahitajika kujazwa kwa kuangalia sifa, weledi, uhodari wa kazi na uzoefu.

Tatu, unahitajika kuangalia Bajeti iliyopo ili kukidhi matarajio na maslahi ya hao viongozi ambao wanateuliwa na kwa maana hiyo basi kama anavyoolewa wakati ulipoidhinishwa muundo huu Oktoba mwaka uliopita tulikuwa bado tunaendelea na Bajeti hii ya mwaka uliopita na Bajeti hii itamalizika Juni mwaka huu 2011 na kwa maana hiyo basi suala la Bajeti litazingatiwa katika Bajeti hii ambayo itapitishwa mwaka huu wa 2011/2012.

Kuhusiana na suala la muundo huu utasaidiaje katika kuimrisha utendaji wa Jeshi la Polisi kama anavyoolewa. Jeshi la polisi kama ilivyo tasisi nyingine ya umma, inapoteua viongozi waandamizi wenyewe sifa, wenyewe weledi, wenyewe utendaji na uhodari, bila shaka itasaidia sana katika kuimrisha utendaji wa taasisi hii,

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini baada ya kuzingatia yote hayo sifa, masharti, weledi basi nina hakika kwamba tukiyafanya hayo kama inavyotakiwa suala hili litasaidia sana katika kuimrisha utendaji wa Jeshi la Polisi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ujumla. (*Makofit*)

Na. 84

Matatizo ya Makazi kwa Askari Polisi – Zanzibar

MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE aliuliza:-

Askari wa Jeshi la Polisi Zanzibar (Ziwani) wanakabiliwa na matatizo makubwa ya makazi kama vile miundombinu ya maji, nyumba chakavu, uhaba wa vyoo na kuharibika kwa uzio uliokuwepo katika eneo hilo hali inayohatarisha usalama;

- (a) Je, kuna mpango gani wa kufanya matengenezo ya nyumba na vyoo kwa wakati huu?
- (b) Je, uziio wa boma la Ziwani utafanyiwa matengenezo lini?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inao mpango wa kukarabati majengo ya zamani pamoja na kujenga majengo mapya kwa ajili ya askari wa Jeshi la Polisi nchi nzima kulingana na upatikanaji wa fedha. Tunatarajia kwamba itakapofika mwaka 2015 tutakuwa tumekarabati majengo chakavu yakiwemo yale ya Jeshi la Polisi Ziwani, pamoja na kujenga uzio unaozunguka boma la Ziwani, kama alivyogusia Mheshimiwa Mbunge.

MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swal la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali inatarajia kukarabati majengo mapya ifikapo mwaka 2015. Na kwa kuwa, choo ni muhimu sana kwa binadamu.

Je, Serikali inanipa ahadi gani katika Bajeti ya mwaka huu, kutengeneza angalau vyoo hivyo vya Polisi Ziwani?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii adimu kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mzee, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema vyoo ni sehemu muhimu sana katika majengo. Kwa maana hiyo, basi tutafanya kila lililo katika uwezo wetu kwa kuangalia kiwango cha fedha zitakazopitishwa katika Bajeti ya mwaka huu. Na ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunafanya kila lililo katika uwezo wetu kuhakikisha kwamba suala hili la ukarabati na matengenezo ya vyoo kutokana na umuhimu wake, linapewa uwezo na linapewa uzito unaostahili.

Naomba tu nimhakikishie Mbunge, tunafanya kila lililo katika uwezo wetu basi, tutenge fedha hizo kwa ajili ya kutekeleza jambo hili muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwapigania Askari wa jeshi la Polisi walioko katika Jimbo lake. Tunamshukuru sana na tutaendelea kushirikiana naye katika kutekeleza majukumu haya tuliyokabidhiwa katika Jeshi la Polisi na katika Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa ujumla.

SPIKA: Siku nyingine maswali ya vyoo, yasije humu Bungeni. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, atauliza swal hilo.

Wananchi Kuporwa Maeneo ya Kilimo na Wawekezaji

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Jimbo la Mufindi Kusini, lina wawekezaji wengi katika viwanda vya mbaao na karatasi na hivyo kupelekea wananchi kukosa maeneo ya kilimo na ufugaji hasa vijiji vya Isaula, Kiyowela, Rugema, Mkalala, Kihanga na na Magunguli.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wananchi hao wanaoporwa maeneo yao na kulipwa fidia kidogo au kutolipwa kabisa?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanywa na Wizara yangu, umebainisha kuwa viko viwanda kadhaa vya mazao ya misitu katika Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa, ikitumiaji viwanda viwili vikubwa ambavyo ni *Mufindi Paper (MPM)* inayomiliki eneo lenye ukubwa wa hekta 9,398. Eneo hilo liko kwenye vijiji vya Isaula, Kiyowela, Idete, na Makungu. Kiwanda hiki kilibadilishwa jina kutoka *Southern Paper Mills (SPM) Mgololo*, baada ya kubinafsishwa. Kiwanda cha pili ni *Green Resources Limited (GRL)* inayomiliki kiasi cha hekta 2,000 kwenye vijiji vya Idete na Kiyowela.

Uchunguzi huo umebainisha pia kwamba kabla ya miradi hiyo kuanzishwa eneo vilipo viwanda hivyo lilikuwa likimilikiwa na Shirika la Maendeleo la Mufindi (*Mufindi Development Corporation (MUFIDECO)*) kuanzia tarehe 1 Julai, 1976 waliokuwa wamemilikishwa kwa madhumuni ya ufugaji wa ng'ombe (Ranchi) na baadaye kutwaliwa na Serikali kwa ajili ya uwekezaji kufuatia mradi huo kushindwa.

Vile vile kuna kundi la tatu la wamiliki wa ardhi kwenye Jimbo la Mufindi kusini ambaao ni wenye viwanda vidogovidogo vya watu binafsi na vya kuhamahama (*mobile*) vya kupasua mbaao na kutengeneza nguzo katika msitu wa Taifa wa *SAO Hill*. Pamoja na wawekezaji hao, wapo wawekezaji wadogo wa upandaji miti katika vijiji mbalimbali. Wawekezaji hao aghalabu hukodisha misitu toka kwa wananchi kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu na kupasua mbaao na kisha huhamia eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, ingawa uchunguzi wa kina juu ya madai ya ardhi ya wananchi kuchukuliwa bila fidia katika Jimbo la Mufindi Kusini bado unaendelea, tumebaini kuwa iko tabia inayoendelea ya wananchi wenye viwanda vidogo na wawekezaji wa upandaji wa miti kuuza ardhi na hivi sasa wengi wamepungukiwa na ardhi ya kulima, hivyo kulalamika kuwa wameporwa ardhi. Baadhi yao wamediriki kuvamia maeneo ya wawekezaji wakidai kuwa ni yao. Tumekubaliana na uongozi wa

Wilaya kuwa baada ya Mkutano huu wa Bunge, nitembelee wilaya hiyo ili tushirikiane kutatua mgogoro uliopo baina ya wananchi na wawekezaji. Tukibaini kuwa mwananchi yeoyote amechukuliwa ardhi yake bila fidia, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wahusika. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, tabia ya wananchi kuuza ardhi kwa kudanganyika na fedha kidogo wanayopewa na wawekezaji imeenea katika sehemu nyingi za nchi yetu. Wananchi wengi wanaouza ardhi, hubaki fukara baada ya kumaliza fedha za mauzo. Ili kulinda maslahi ya wananchi waishio vijiji wasipokonywe ardhi yao na wajanja wachache, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa viongozi wa Serikali za Mitaa na wananchi kwa ujumla ili kuhakikisha kuwa ardhi haitolewi kwa wawekezaji bila kuzingatia matakwa ya Sheria za Ardhi. Aidha, Serikali inaendelea kutambua na kupima vipande vya ardhi ya wananchi na kutoa Hatimiliki za kimila kwa kupitia vijiji vyao.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Viongozi na Watendaji wa Serikali, washirikiane na Wizara yangu kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuhifadhi ardhi na kuingia ubia na wawekezaji badala ya kuuza kwa manufaa yao na vizazi vijavyo.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilitoa ardhi kwa mwekezaji bila kuwashirikisha wananchi wa kijiji cha Isaula na sasa hivi kusababisha matatizo makubwa.

Je, Serikali itaweza kuwarudishia wananchi wa Isaula ili waweze kuendelea na kilimo na ufugaji?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la swali la msingi. Wawekezaji waliopo Mufindi pale, wale wakubwa wawili kwa maana ya *SPM* ambayo sasa hivi ni *MPM* pamoja na *GRL* yaani *Green Resource*, ardhi waliuziwa na Shirika la Maendeleo la Mufindi (*MUFIDECO*).

Sasa wako wananchi wachache ambao walizua *Green Resource* sehemu ya ardhi yao na ndio sasa hao ambao wanarudi kusema kwamba walinyang'anywa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama nilivyoeleza, kama tutabaini kwamba wananchi walichukuliwa ardhi na bila uongozi wa Serikali kujua. Suala hilo tatalishughulikia kwa

mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999.
(*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Leo tungenesema kutoa *marks*, Waheshimiwa Wabunge, mmejitahidi kuuliza maswali mafupi ya nyongeza na Waheshimiwa Mawaziri nao wamejibu kwa kifupi, ndiyo maana mmepata nafasi ya kuuliza angalao kila swali limepata waulizaji maswali ya nyongeza, anagalau wawili.

Sasa mngekuwa mnauliza mafupi zaidi, tungekuwa na watu wengi zaidi, lakini sasa mkituhutubia basi haiwezekani na Mawaziri nao wakishafika hapa, maswali ya nyongeza wanajibu utafikiri semina, nayo pia haifai. (*Makofii*)

Kwa hiyo, kila mtu ajifunze kipindi cha saa moja kiweze kufanya kazi kubwa zaidi. Kama swali ni zuri, ni kwa nini unauliza swali la nyongeza. Unasema swali zuri kabisa, halafu unauliza swali la nyongeza, la kazi gani? Kama hakuna jibu zuri, uliza tu swali linalohusika, tutumie muda wetu vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kuwatangaza wageni walioko hapa. Kwanza kabisa ninao Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *ALAT*, wakiongozwa na Mstahiki Meya wa Jiji la Dar-es-Salaam na Mwenyekiti wa *ALAT* ni yeze huyo huyo. Yuko wapi? Nafikiri ni Mheshimiwa Massaburi. (*Makofii*)

Halafu kuna wengine wengi, ninaogopa kutumia muda wangu kwa ajili ya kuwatangaza, lakini kwa leo tu ninaruhusu, kwa sababu inalekea hapa wanawahu nyie wengi hapa. Kwa hiyo, yupo Mheshimiwa Dkt. Didas Masaburi, Mwenyekiti, halafu yuko Mheshimiwa Diwani Daniel Okoka, Makamu Mwenyekiti wa *ALAT*; Okoka, siyo Mbunge huyu?

Yupo Dkt. Anthony Amani, Meya Halmashauri ya Bukoba. Yuko wapi, hawapo? Yuko Mheshimiwa huyu peke yake, Theresia Msuya, Mwenyekiti wa Mwanga, ahsante sana kwa kutukaribisha tulipofika Mwanga, tulifurahi sana. Na ni wewe peke yako tu, nafikiri, mwanamke Mwenyekiti wa Halmashauri, aah, nasikia wako wawili. (*Makofii*)

Halafu kuna Mheshimiwa Mwenda Hamisi Abdallah, yeze ni Mwenyekiti wa Kondoa. Yuko Mheshimiwa Kapunga, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbeya ahsanteni sana kwa kutupokea pia. Yupo Mheshimiwa Stephen Mhapa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Iringa, karibu sana. Tuna Mheshimiwa Elias Ngorisa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ngorongoro, ahsante sana. (*Makofii*)

Tuna Mheshimiwa Omari M. Guledi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tanga. Tuna Mheshimiwa Gulam Dewji, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. (*Makofii*)

Tuna Mheshimiwa Amiri Juma Nondo, yeze ni Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora. Yuko Mheshimiwa Abbas Abdallah Matutilo, Mwenyekiti wa

Halmashauri ya Liwale, ahsanteni sana. Yuko Mheshimiwa Benard David Polikapi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Misungwi, ahsanteni sana.

Yuko Mheshimiwa Amos Sagala Nyambikwi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime. Mheshimiwa Marwa Gisiri, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri nadhani hiyo hiyo ya Tarime. Kuna Mheshimiwa Stephen Kibaye, Diwani wa Kata ya Manga. Mheshimiwa Mhando Senyagwa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kyela. Yuko Mheshimiwa Amina Mbilinyi, yeze ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kibaha.

Waheshimiwa Wabunge, yupo Ndugu Noel Mahenga, Mkurugenzi wa Rungwe, poleni sana kwa msiba wa Mwenyekiti wa Halmashauri, nasikitika sana tulikuwa tumemwona. Ndugu Wilsoni Kabwe, yeze ni *City Director*, nafikiri wa Jiji la Mwanza.

Yupo ndugu Theresia Mahongo, yeze ni wa Halmashauri ya Iringa, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Iringa na yoko Mheshimiwa Amasi Mushandete, Mjumbe kutoka Shinyanga. (*Makofi*)

Nimewataja hao kwa sababu mbili muhimu. Kwanza wamekaa kwenye eneo la *Speaker's Gallery*, lakini wanawahu mulio wengi hapa. (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi 70 kutoka shule ya Sekondari ya Makutupora, wasimame na walimu wao hapo walipo, karibuni sana, msome kwa bidii. Waheshimiwa Wageni wengine wote mlioko hapa, pia mnakaribishwa. Mzee wangu pale, sijapata jina lake sijui ni nani? Aah, Mzee Mtopa, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Mtwara. Karibuni sana mzee wangu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi. Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo hii saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 227, katika Jengo la Utawala.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana watakuwa na Kikao katika ukumbi wa Msekwa (B).

Halafu Mheshimiwa John Mnyika, yeze ni Katibu wa Bunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA kuwa leo saa 8.00 mchana, wakutane katika ghorofa ya pili, jengo la Utawala Ukumbi Namba 231.

Halafu na huyu ni Katibu wa Michezo, anasema anaomba niwatangazie matokeo ya mechii ya kirafiki siku ya Jumamosi iliyopita kati ya Waheshimiwa Wabunge na Wasanii wa Filamu, *Bongo Movee* kama ifuatavyo. Mpira wa miguu, *Bunge Sports Club* wamefunga magoli 2 na *Bongo Movee* goli moja tu. Kwa hiyo, anasema na nyota wa michezo huo upande wa mpira wa miguu ni Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis; yoko wapi huyu Sadifa Juma Khamis? Ndio nyota huyo, ahsante sana, hongera. Halafu mpira wa

pete, *Bunge Sports Club* walifunga magoli 17 na *Bongo Movee* magoli saba. Kwa hiyo, nyota wa mchezo kwa upande wa mpira wa pete ni Mheshimiwa Grace Kiwelu, kila siku. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunaombwa tuwapongeze wenzetu na kwa sababu ni mechi za mwanzo mwanzo, basi muendelee hivyo hivyo na tutawapongeza vizuri tarehe 24 jioni, wakati Ubalozi wa Canada, watakapofanya sherehe yao hapa ya kusherehekeea siku yao ya Taifa, watafanya hapa hapa Dodoma. Kwa hiyo, siku hiyo tutawasherehekeea na hawa pia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kwa sababu mbili tofauti; moja nina kazi pale Ofisini. Kulikuweko na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro na sio Tabora, ahsante sana. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu mbili; moja nina shughuli Ofisini lakini ya pili ninapenda kuwapa uzoefu Wenyeviti wetu.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kuwe na nidhamu kabisa, wananchi wanani pigia simu kwa wingi na kuniandikia *message*. *Image* yetu mbele ya watu si nzuri. Huu mtindo wa Mwongozo, Taarifa, bila utaratibu tunatumia muda ambao wachangiaji wangekuwa wengi. Jamani tuendelee kukua, tusiendelee kuwa kero kwa watu. Walikuwa wanapenda sana kuangalia kipindi hiki cha Bunge, lakini sasa wengine wanakereka sana kwa tabia zetu. Kwa hiyo, mbadilike muwe watu Waheshimiwa kama tunavyoheshimiwa na watu waliotuchagua.

Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, anipokee. (*Makofi*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2011. Kwanza kabisa namshukuru Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo. Zaidi sana nawashukuru wapigakura wa Jimbo la Mtera kwa kunichagua kwa kishindo kuingia ndani ya Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Shukrani zangu pia ziende kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, na kwa namna ya pekee vilevile nimpongeze Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliyewasilisha bajeti - Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi tubadilike kidogo, tusifikiri kwamba kila kinachosemwa na Upinzani ni kibaya tu. Viko vizuri. Vilevile nachukua fursa hii kuwa Mbunge wa kwanza pengine wa CCM kumpongeza Dkt. Slaa kwa kuungana na Mheshimiwa Mbowe, na Mheshimiwa Mrema kushindwa kwenye uchaguzi uliopita nampongeza sana, maana na yeye ameingia katika kundi la waliowahi kushindwa wakiwepo akina Lipumba, Mheshimiwa Mbowe, pamoja na Mheshimiwa Agustino Lyatonga Mrema. Kwa hiyo, wale waliokuwa wakifikiri ni jambo la ajabu, ni jambo jema kuungana na wenzake ambao wamepata kushindwa mara nyingi. Anaweza kupata uzoefu wa namna ya kuishi katika kushindwa kupitia kwa wenzake. (*Makofi*)

Baada ya pongezi zangu hizo, nataka sasa nizungumzie mambo ya msingi yaliyoko kwenye bajeti hii. Nimesoma vizuri, nimeelewa tatizo kubwa la uendeshaji wa vipaumbele vyetu liko kwenye suala la utekelezaji. Tungependa kuona linatekelezwa kama ilivyopangwa, na kwa kweli nataka nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania wanaotusikiliza wawe na hakika kabisa kwamba uzoefu tumeshaanza kuupata, kwa hiyo, maneno ya Spika tunataka tuyasisitize, na safari hii nataka nichangie mpaka kumaliza dakika zangu kumi na tano bila kupigwa mwongozo, na wale waliojiandaa washindwe kwa jina la Yesu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tumekuwa tukizungumza kama vile tunafanya uigizaji. Anasimama Mbunge anasema kwa uchungu sana mabaya yote ya Serikali, lakini anaomba lami, maji, halafu mwishoni anasema huungi mkono bajeti hii. Ni uigizaji! Sasa kama huungi mkono bajeti, hivyo vitu vitaletwa na Mungu? Ni lazima uunge mkono bajeti ili ilete hivyo vitu. Kwa hiyo, Watanzania watatuangalia, watapata vichekesho sana watu tulioomba lami, tulioomba maji, tulioomba shule kesho tunasema hatuungi mkono bajeti. Sasa ukiwa huungi mkono bajeti, hivyo vitu vitakujaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme kuna vitu vingine tunavifanya hapa kama vile sinema, kama vile ni waigizaji wakati tunatakiwa tufanye vitu ambavyo hata Watanzania wakitutazama wajue kwamba wenzetu wanatutea na wanataka kweli maendeleo yapatikane na hayawezi kupatikana bila kuunga mkono bajeti hii, haiwezekani. Kwa hiyo, lazima tuiunge mkono bajeti, halafu tuisimamie Serikali kuhakikisha kwamba inatekeleza ili wananchi wetu waweze kupata maendeleo. (*Makofi*)

Naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja, lakini nataka nizungumze machache. Tumezungumza sana kuhusu maji. Ukija kila Bunge tunazungumza vizuri sana kuhusu maji mijini na kila Wabunge wa mijini wakisimama wanazungumzia maji kana kwamba watu wa vijijini tayari wanayo maji safi na salama. Tungeomba katika vipaumbele vyta ya mwaka huu maji vijijini itiliwe mkazo sana. Watu wetu vijijini wanapata taabu sana, siyo tu kuyapata maji mbali, bali wanakunywa maji machafu na kusababisha afya zao kuwa katika hali mbaya sana. Magonjwa ya *Typhoid* yameua watu wetu wengi sana kwa sababu kwanza vijijini siyo rahisi mtu kujua anasumbuliwa na nini, na siku hizi kuna balaa ya ugonjwa huo wa UKIMWI, mtu akiugua *Typhod* wanafikiria kwamba ooh, huyo mtu amepata UKIMWI. Kwa hiyo, tukiweka maji safi vijijini tunaweza tukaokoa watu wengi na tukaokoa nguvu kazi nyingi sana ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kuhusu barabara. Barabara zimezungumzwa sana na hata katika bajeti hii zimepewa kipaumbele, lakini tuangalie na barabara za muhimu vilevile, za Wilaya. Ukitazama Mkoa mzima wa Dodoma mtandao wake wa barabara mimi nadhani ndiyo unakuwa kikwazo hata kuwafanya baadhi ya viongozi hawataki kuhamia Dodoma. Maana mpango wa kuzungumza kuhamia Dodoma ulianza mimi sijazaliwa mpaka leo nimezaliwa, nimekuwa Mbunge, lakini bado hadithi tu, tunahamia Dodoma, tunahamia Dodoma. Hebu wa kwanza kuanza kuhamia Dodoma ingekuwa Spika basi, maana Bunge liko hapa, Dar es Salaam anafuata nini? Si akae hapa hapa Dodoma! (*Makofi*)

Angeanza Spika kukaa hapa Dodoma na Serikali najua ingekuja, kwa sababu hata pale Dar es Salaam tunapiga kelele ya foleni, wasababishaji wengine wa foleni ni viongozi, Mawaziri wote wako Dar es Salaam, vijana wao Dar es Salaam, familia zao Dar es Salaam, magari Dar es Salaam lazima kutakuwa na foleni. Mkija Dodoma, foleni itaondoka Dar es Salaam ndugu zangu, karibuni Dodoma. Hamieni hapa ili kupunguza mlundikano wa shughuli za Dar es Salaam maendeleo yaweze kupatikana kwa haraka. Kwanza kiongozi ukikaa Dar es Salaam pale hufanyi kazi, maana foleni itakuchukua masaa matatu, ukifika pale kunywa chai nusu saa, hujakaa kusoma magazeti nusu saa umechoka unarudi nyumbani, ndiyo maana kazi ya kutekeleza mipango ya Serikali haifanikiwi. Kwa hiyo, tungewasihi mje hapa tumekuwa tukihamisha walimu, madaktari kuwapeleka vijijini ambako hakuna umeme, wanakwenda, nyie Dodoma pana umeme, barabara, shida iko wapi ndugu zangu? Mpango upo, kwa hiyo, tungewasihi mkae hapa, mhamie hapa, ili tufanye kazi vizuri. (*Makofi*)

Nizungumzie habari ya maendeleo. Watu wengi wamesema sana kuhusu maendeleo kwa ujumla, na bahati nzuri juzi juzi hapa Mheshimiwa Wasira kasema sisi hatukuwepo. Nataka nikubaliane naye kwamba kweli hatukuwepo, lakini sisi tunajua nchi hii ina maendeleo sana, maana hali mbaya na sisi wenye tuliona. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, habari ya kwamba Tanzania haisongi mbele, siyo ya kweli. Hata vijana tuliozaliwa miaka ya 1970 kuja leo tunaona tofauti. Maendeleo yapo na yanaonekanakwa macho, isipokuwa kila mtu mdomo mali yake, anaweza kubisha. Kwa mfano, ukichukulia miaka ya 1982 hapa Dodoma mwaka 1982 pale kijiji cha Mvumi alikuja Askofu Marehemu Yohana Madinda na gari ndogo kwa mara ya kwanza, siku zote tulikuwa tunatumia lori kuja hapa mjini. Alikuja na *Peugeot*, bibi mmoja mzee akapiga vigelele sana anaizunguka ile gari ndogo anasema njoo ni mwone mtoto wa gari, gari imezaa! Watu wakatoka kujaa pale, bibi yule anaamini kwamba lile gari la kijiji ndiyo limezaa haka kagari kadogo! Akachungulia ndani ya lile gari kwenye uvungu akaona bomba la *exhaust* akasema halafu cha kiume, njoo ni mwone! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo hii kijiji kwangu pale hakuna mtu anaamini kwamba gari linazaa, wote wanajua magari yanatengenezwa na maendeleo makubwa. Nataka nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuleta maendeleo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie umeme. Hebu vipaumbele vyatuhinga na maeneo yaliyosahaulika katika Jimbo la

Mtera lenye vijiji 62, vijiji vyenye umeme viwili tu, tena umeme ule umeletwa na kanisa wamisionari. Kwa hiyo, unaweza kushangaa, tunalo bwawa, tunazo nyumba bora, lakini tunashuhudia nguzo za umeme zinapita kwenye mashamba yetu kwenda kwa waungwana. Ndiyo maana siku moja nikapandisha jazba, nikasema, basi tung'oe nguzo hata mbili ili umeme uzime sehemu nyingine, pengine mtatukumbuka. Ndugu zangu tupeni umeme, watu wanataka kupata maendeleo na umeme unapita kwetu na sehemu nyingine zinataka ushushe *transforma* tu kama Kata ya Muungano, Mvumi Makuru, *Mission*, ukienda Kata nyingine kuna maendeleo makubwa limekuwa kubwa eneo la Mpwayungu, ni *center* kubwa ya wafanyabiashara. Tarafa nzima yenyе kata tano hakuna mawasiliano, ina sekondari moja, hakuna umeme. Ndugu zangu tunapoteza nguvu kazi nyingi sana.

Hebu tuangalie basi katika kuimarisha hata ile Shule ya Sekondari tu ya Tarafa ya Mpwayungu, tuipe mabweni, tuipe walimu wa kutosha, maana sekondari moja inahudumia Kata tano, lakini hiyo sekondari haina mabweni, watoto wa kike wanapanga uswahilini. Mkitusaidia ndugu hata sisi hii *UDOM* mliyotujengea hapa itakuwa na manufaa kwetu. Lakini kinyume cha hapo, hatuwezi kuingia pale kwa kucheza ngoma. Watu wetu watakuwa wanasifiwa tu kwamba kuna *UDOM*, lakini wenyewe wakazi wa Mkoa huu watakuwa hawamo mle ndani. Maana nimeshuhudia hata juzi wakati chuo kinafungwa, nikaona Wabunge wengi walikuwa wako *busy* kupigiwa simu za kuombwa nauli. Mimi sikuombwa nauli maana hakuwepo mtu hata mmoja katika waliofukuzwa kutoka katika jimboni kwangu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naomba tutoe vipaumbele kwenye maeneo yaliyosahaulika, yaliyoachwa kwa muda mrefu ili tuyasaidie. Kwa mfano, njoo uangalie hospitali yetu ya Mkoa wa Dodoma. Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, nimepeleka mgonjwa pale Ijumaa saa 8.00 usiku. Tumemkuta Daktari mmoja Wodi Na.16, kitu ambacho hakiwezekani kabisa, kuna Vyuo; Waziri wa Afya, siku moja hebu nenda pale usiku utakutana na madudu ya ajabu. Tumempeleka yule mgonjwa, tumekuta foleni ya wagonjwa karibu nane. Yule dada alijitahidi kuokoa maisha yake mpaka kuja kulazwa ni saa 8.00 na bahati mbaya, juzi nikasikia yule dada amefariki, jana tumemzika. Kwa hiyo, unaweza kuona namna ambavyo matatizo yako makubwa kwenye Idara ya Afya. Sasa hivi Dodoma imekuwa mji, umekuwa una vyuo vingi, kuna maeneo mengi. Hebu tuboreshe haya maeneo ili watu wetu waweze kupata huduma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nizungumze kuhusu matangazo. Jamani kuna matangazo mengine yamekuwa yakilitesa Taifa hili. Unakaa kwenye TV, wako Masheikh, Maaskofu, linapita tangazo: "Safari Lager, urithi wetu." Hivi kama urithi wa nchi itakuwa ni pombe, hali ya nchi yenyeve itakuwaje? Ndiyo maana mnaona hata mijadala yetu wakati mwingine inakuwa kama vile tumelewa. Sasa kama tumerithi kutoka kwa Mungu, Mungu anaweza kuwarithisha watu pombe? Unatangaza: "Konyangi, *the spirit of Nation, spirit of Nation.*" Yaani kweli Taifa hili *spirit* yetu iwe ni konyagi? Kwa hiyo, kuna baadhi ya vitu vinatufanya tunamuudhi Mungu ndiyo maana hali inakuwa hivi. Maaskofu wako, Masheikh wako, wanaambiwa safari lager ndiyo urithi wa Mtanzania toka kwa Mungu wanakubali, hebu tukatae vitu vy'a namna hii. Baadhi ya vitu vinaliangamiza Taifa hili, sisi tunaona vitu vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kwa moyo kabisa niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutoa ukumbi kuipa Serikali ili ijenge Chuo. Ndugu zangu, ni chama cha kwanza katika dunia, maana hata matusi tunayotukanwa na hao watoto ni kwa sababu tumewafanya mambo mema. Serikali ya CCM imekubali tukaendeshe mikutano yetu kwenye godauni, lakini ukumbi wasome vijana wetu. Ndugu zangu hautapata chama cha namna hiyo katika dunia hii. Vyama vingi vimechukua kumbi, vimechukua kila kitu. Lakini CCM inatoa maeneo yake kuwapa vijana wasome na wenyewe wanarudi kwenye godauni pamoja na matusi hayo tunayopata. Tunashukuru sana viongozi wazuri wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Kuna vitu vingine vinaendeshwa na wenzetu vya kuchekesha sana. Mtu anasimama, anampongeza Mwalimu Nyerere halafu hapongezi CCM. Sasa Mwalimu Nyerere alikuwa anafanya kazi peke yake? Alikuwa anafanya kazi akiwa na Chama cha Mapinduzi na viongozi wa CCM. Kwa hiyo, ndugu zangu nachukua muda huu kuwapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine la mwisho ambalo nataka kulichangia. Nataka nizungumzie kuhusu pesa. Fedha zetu nazo vilevile zinatuangusha. Hivi kwenye pesa kuna haja gani ya kutangaza utalii kwenye noti unaweka nyoka, simba, ngedere, kwanini tusiache sura za waasisi wa Taifa hili? Kama tumeamua kuweka sura ya Mwalimu Nyerere, tuweke sura ya Mwalimu Nyerere na Karume, kwisha! Utalii tuutangaze kupitia vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama pesa zitakuwa zinatangaza utalii, basi hata nguvu yenye, haitakuwepo kwa imani tu za dini nyingine nyoka anahusishwa na shetani, wewe unamweka kwenye shilingi mia tano.

Kwa hiyo, mambo yanakuwa magumu! Kwa nini tusibadilishe hela yetu tukaipa heshima tukafika mahali tukachukua sura za waasisi wa nchi hii, Mwalimu Nyerere tukamweka kwenye pesa, tukamweka na Karume, biashara imekwisha? Utalii tuutangaze kwenye magazeti na vyombo vingine vya habari, lakini pesa za nchi zikitumika katika kutangaza utalii tunafika mahali tunakuwa na pesa nyepesi na ndiyo maana mnaona pesa haipandi kila siku. Pandisha hela, wewe utapandisha nyoka! Wewe utapandisha simba, tembo, hata hao wenzetu ambao dola tunaiona ina *value*. Unaona dola ina picha ya kiongozi wao wanamuensi mle; tunaona aibu gani kuwaenzi viongozi wa nchi hii? Ndugu zangu, mimi nataka niwasihii sana, tukibadilisha baadhi ya mambo ambayo yamekuwa yakinutesa itafika mahali tutaendelea. (*Makofi*)

Dodoma tunaomba viwanda, tumeona mmezungumza viwanda, habari ya kutupa hospitali ya vichaa, jela ya kunyonga watu, hatuwezi kupata maendeleo kwa watu kunyongwa hapa. Hatuwezi kupata maendeleo sisi, badilisheni, safari hii watu wakanyongwe Musoma au Tabora, yako maeneo mazuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa michango yako mizuri. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Lusinde kwa utangulizi wake, ameanza kwa kusema kwamba sisi sote lengo letu ni kujenga umoja wa nchi yetu. Michango yetu iunganishe Watanzania wote. Watawala watakuwa na hoja nzuri, Kambi ya Upinzani inawajibu wa kuunga mkono vilevile sisi kama watawala Chama cha Mapinduzi.

WABUNGE FULANI: Aah!

MWENYEKITI: Upande wa upinzani wanaweza kuwa na hoja nzuri, basi tuzifanyie kazi kwa manufaa ya nchi yetu. Baada ya kusema haya, namkaribisha msemaji anayefuatia, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, hayupo?

MBUNGE FULANI: Hayupo.

MWENYEKITI: Basi anayefuatia, kulikuwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, ameniomba kwamba ye ye hataweza kuchangia kwa kuongea anadharura kwa vile anayefuatia sasa atakuwa ni Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, tafadhali.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya kamili nikasimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa mzima wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, lakini nataka niwapongeze kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Ali Mohamed Shein, Makamu wa Kwanza wa Rais - Mheshimiwa Seif Sharif Hamad, Makamu wa Pili wa Rais - Mheshimiwa Balozi Dkt. Seif Ali Idd kwa kutekeleza kwa vitendo uundaji wa Serikali ya umoja wa kitaifa. Ukweli, hili nimefurahishwa mno na jinsi watu hawa wanavyofanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na leo Zanzibar kuna amani kubwa sana. Zanzibar ni njema na nina imani ndani ya muda mfupi ujao maendeleo ya Zanzibar yataanza kuonekana. Nashauri Serikali ya Muungano ifuate nyayo za Zanzibar. (*Makofi*)

Pili, nataka niwapongeze viongozi wetu wa Chama cha Wananchi *CUF*, kwa ngazi zote kwa kazi nzuri wanayofanya kuimarisha chama chetu, na nina imani kwamba mwaka 2015 ushindi mkubwa unatusubiri. (*Makofi*)

La mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napongeza wananchi wa Jimbo langu la Chambani, kwa kunirudisha tena katika Bunge hili, na mimi nitafanya kazi nao kwa karibu sana na kama walivyoona kazi yangu nzuri katika miezi sita ya mwanzo tulioifanya kule Jimboni, inapendeza.

Baada ya kusema mambo hayo machache, sasa nianze kuchangia bajeti. Nionavyo mimi, bajeti ya mwaka huu siyo nzuri kama baadhi watu wachache wanavyofikiria. Kwa mawazo yangu, bajeti nzuri ni ile ambayo inatoa unafuu wa maisha, unafuu ambao wale wenye mlo mmoja kwa siku, angalau wapate milo miwili au mitatu. Bajeti nzuri ni ile

ambayo inatoa hali bora za huduma za afya, elimu, maji safi na salama, lakini vile vile bajeti nzuri ni ile ambayo ina wigo mpana sana wa kukusanya kodi. Sasa sijui kama haya mambo yapo katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, bajeti hii ni ndogo sana ukiangalia bajeti nzima ya shilingi trilioni 13.525, kuna shilingi bilioni 1.9, hiyo ni kwa ajili ya mikopo tu. Sasa iliyobaki itakuwa kama bajeti kama shilingi bilioni 11.6. Sasa kama pesa hizo zilikuwa ni sawasawa, bajeti ya mwaka uliyopita shilingi bilioni 11.6 hazikuweza kukidhi haja ya kuondokana na tatizo la msingi. Je, itawezekanaje, bajeti hiyo ya shilingi bilioni 13 ambayo ina deni la shilingi bilioni 1.9 iweze kutoka na kazi za msingi. (*Makofi*)

Ndiyo maana katika bajeti za kisekta zimepunguzwa. Bajeti ya afya imepungua, bajeti ya uvuvi na mifugo imepungua na zile ambazo zimeongezwa, ongezeko lenyewe ni kidogo hasa ukilinganisha kwamba shilingi yetu imeteremka thamani kila wakati. Utakuta hata kama zile ambazo zimeongezwa, basi ongezeko lenyewe ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya maji, katika miaka mitano iliyopita, basi makusanyo ya ndani yalipungua kila mwaka, kwa mfano katika mwaka 2007/2008, ilikuwa shilingi bilioni 75; mwaka 2008/2009 shilingi bilioni 46; mwaka 2009/2010 kidogo imezidi kidogo shilingi bilioni 50; lakini mwaka 2010/2011 ilikuwa kama shilingi bilioni 30.7 tu.

Kwa kweli kama bajeti ya maji itapungua, utawezaje kutatua matatizo ya maji Dar es Salaam, Tabora, Nzega au Lindi? Lindi kule Limaliao na Pandeploti ambako kuna matumizi makubwa ya maji. Dar es Salaam ni kioo cha nchi hii, kama kutakuwa hakuna maji, maana yake ni kwamba, nchi nzima ina matatizo, na ni aibu. Lakini katika suala la mvua, kwa mfano kuna suala la malisho, malambo na mabwawa, kama hakuna fedha ya kutosha unawezaje kujenga mabwawa na malambo? Lakini vilevile katika suala la uvuvi, kwa mfano kuna uharibifu wa mazingira ya Samaki, elimu ya uvuvi, vifaa vya uvuvi ambavyo vinatakiwa vipatikane ili kuimarisha uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni mambo ambayo yanaonyesha kwamba kwa sababu bajeti ni duni au finyu, haiwezekani kuyarekebisha. Lakini kwa mfano, kwenye kilimo, bajeti ya kilimo imetolewa, lakini kwa kweli haikidhi matarajio ya wakulima wa Tanzania na wale wa nchi za SADC kwa sababu katika nchi za SADC tumekubaliana kwamba angalau bajeti ya kilimo iwe na 10% ya bajeti nzima. Lakini kilimo chetu ambacho kinasuasua, kina ukuaji chini ya 6.2% na kinachangia kiasi cha 4.2% katika kuajiri Watanzani wapatao milioni 75. Sasa kilimo chetu kina wasiwasi na kinasuasua na miradi mbalimbali ambayo imeletwa hapa haikuweza kusaidia kwa mfano katika miradi hii ya ASDP ambao ni mkubwa, umechukua karibu miaka sita na trilioni 2.7 haikuweza kufanya kazi iliyotarajiwa.

Fedha ya Kilimo, kwanza wengi wanasema ni mradi wa wafanyabiashara, wengine wanasema ni agenda za kisiasa. Lakini kwa kweli Kilimo Kwanza vilevile ni kauli tu, kwani hakina maendeleo makubwa. Tuna fursa nyingi za kufanya biashara na nchi jirani, kwa mfano, jiografia ya Tanzania ni nzuri, lakini badala ya kusaidia wakulima

ili waweze kuuza bidhaa zao nje, tunasema kuna matatizo ya usalama wa chakula, kwa hiyo wakulima wanaambiwa wasiuze chakula nje. Kwa hiyo, utakuta ni matatizo ambayo kila wakati mkulima anakandamizwa ili asiweze kunyanyuka, ingawa Serikali inasema kwamba inamuenzi mkulima, lakini kwa kweli hali ya mkulima wa Tanzania ni mbaya, kwani mikopo hakuna. Kila mara tunaambiwa kwamba mikopo itapatikana kwenye Benki ya Wakulima, lakini ni maneno tu, hakuna Benki ya Wakulima mpaka leo. Hii *TIB* ambayo imezungumzwa, ipo, wakulima wengi hawapati mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni ndogo kwa sababu mbili kubwa. Kwanza, vyanzo vya mapato ni kidogo. Vyanzo vyenyewe utasikia ni sigara zenye kichungi na zile ambazo hazina kichungi; ni vinywaji baridi na vinywaji vikali. Sasa Watanzania wakiamua kwamba hawanywi pombe wala hawavuti sigara, mnadhani mtapata wapi? Kwa hiyo, inabidi Serikali iwe na upeo mpana wa kutafuta vyanzo vya mapato na tumekuwa tukiwaambia mara kwa mara kwamba jamani kuna vyanzo vingi vya mapato. Kwa mfano, katika uchumi tumekuwa tukisema kwamba katika uvuvi kwa mfano tumesema kodi za leseni ziongezwe, tozo za Samaki wanaovuliwa zizidishwe, ijengwe *Fish Ports* ambapo meli zikija pale zinaweza zikavua.

Lakini vilevile kuna mambo mengi, kwa mfano utalii; misitu, mbao, magogo na kadhalika. Hivyo ni vitu ambavyo tunafikiri kama Serikali itazingatia vya kutosha, basi inawezekana kabisa Serikali ikaongeza mapato.

Vilevile kuna taarifa zenye uhakika kwamba Serikali haikusanyi mapato ya kutosha. Kuna watu wengi ambao wanatarajiwa kuchangia Serikalini, lakini hawachangii na Serikali inalijua hilo. Sasa nadhani Serikali ikikusanya mapato ya kutosha halafu ikawa na vyanzo vingine vya mapato, inawezekana kabisa bajeti ya mwakani ikakuwa nzuri zaidi badala ya kuwa bajeti finyu ambayo kwa kweli hairidhishi kwa Mtanzania yeoyote.

Jambo lingine ni kuhusu mfuko wa pamoja. Katika ukurasa wa 37 wa kitabu cha hotuba ya bajeti, imezungumziwa Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume hii imeundwa kwa mujibu wa Katiba ibara ya 134 na malengo yake makubwa ni kuzishauri Serikali zote mbili, yaani Zanzibar na Bara kuhusu kuleta uhusiano mzuri wa kiuchumi na kwa mantiki hiyo hiyo Serikali au Tume iliajiri *Consultant* kutoka nje kuzishauri Serikali zote mbili juu ya namna ya kugawana mapato na kuchangia huduma za muungano.

Cha kushangaza ni kwamba, Tume imefanya kazi yake vizuri kwa mujibu wa Katiba, lakini Serikali zetu zinapiga danadana, yaani mapendekezo ambayo yametolewa na *Consultant* wetu, yaani Serikali iijadili, yamekuwa yakipewa muda mrefu toka mwaka 2006 mpaka leo bado hatujapata ufumbuzi wa suala hilim na Serikali imeendelea kuvunja Katiba. Lakini Serikali ijue kwamba hilo ni tatizo. Mimi nasema haiwezekani kwa sababu Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano ni Serikali za CCM, zinatumia ilani ya CCM lakini inawezekanaje leo kwa muda wa miaka sita imepita jambo hili ambalo ni zuri la kuondoa mizozo halijapata ufumbuzi? Ni miaka sita imepita!

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana, lakini kuna mambo muhimu yanafichwa. Mimi nafikiri, kwa mawazo yangu, kwenye suala la faida ya Benki Kuu, kama mnavyojuu kwamba Zanzibar ilikuwa Mjumbe wa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki kabla ya kuvunjwa na ilipovunjwa ile fedha ya Zanzibar iliingia katika *capital* ya kuunda Benki Kuu. Hadi leo Zanzibar haijapata faida kutoka Benki Kuu kwa sababu Benki Kuu inafanya biashara inapata faida. Faida ya Benki Kuu Zanzibar haijapata na Zanzibar inaidai Benki Kuu fedha nyingi sana. Hilo ni moja ya jambo ambalo nafikiri linapigwa danadana.

Vilevile mgawo wa 4.5% ni mdogo na hoja zimetolewa, lakini bado Serikali inang'ang'ania palepale. Lakini kuna kero kubwa ya *double taxation*. TRA ni moja, lakini mzigo wa Zanzibar unaokuja Bara hutozwa kodi Zanzibar na ukifika Bara hali ni ile ile. Tumesema mara nyingi kama *double taxation*, ni ukandamizaji na uonevu, lakini bado Serikali inaendelea, ni kama kumpigia gitaa mbuzi, samahani! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka sana nizungumzie bei ya mafuta. Nataka niwatanabaishe watu ambao walifurahishwa na kauli ya Mheshimiwa Mkulo kwamba Serikali itafanya mapitio ya tozo mbalimbali au itakokotoa kwa ajili ya kuzipinguza na kupunguza bei ya mafuta. Kwa nini Serikali haikukokotoa hizo bei kabla ya kusoma bajeti? Kwa nini bajeti iliyosomwa haikungiza taarifa ambayo tayari imeshakokotolewa? Kwa sababu inawezekana kwamba mkokotoo huo usiwanufaishes wananchi, ni kwa kiasi gani bei ya mafuta ikipunguzwa kwa njia hiyo itasaidia kuinua maisha ya wananchi? Hilo ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifanye utafiti wa kina juu ya soko la mafuta kwa sababu katika soko la mafuta kuna uchakachuaji mkubwa wa mafuta. Sote tunajua hivyo kwamba mafuta yanayoshushwa Dar es Salaam yanapokwenda katika nchi jirani yanapita kati ya Kibaha na Chalinze. Kuna vituo vya mafuta zaidi ya 43 na vingine vinaendelea kujengwa, huku utakuta matenki yamekaa wala hakuna gari zinazojaza mafuta pale, Serikali inajua. Kuna uhakika mkubwa kwamba Serikali inafahamu suala hilo la kwamba mafuta yanachakachuliwa, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Je, hiyo inatokana na nini? Inatokana na tofauti ya kodi, yaani kuna tofauti ya kodi baina ya mafuta ya taa, *diesel*, na *petrol*. Wale ambao wana mtindo huo, wanachanganya mafuta hayo, kama takwimu zangu ni sawasawa ni kwamba mafuta ya taa kodi yake ni Sh. 52/= kwa lita.

(*Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha na anayefuatia sasa hivi ni Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mcemba Madelu, atafuatiwa na Mheshimiwa Rosse Kamilius Sukum na Mheshimiwa Leticia Nyerere ajiandae.

MHE. MWIGULU L. M. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Ukipewa fursa wakati mjadala unaelekea mwisho, maana yake unatakiwa utoe *concluding remarks* na *way forward*.

Mimi pia nitumie fursa hii kutoa mchango wenyewe mwelekeo huo ili Watanzania waweze kuelewa na hivi ndiyo naanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikalini na kwenye sekta binafsi huwa kuna wataalamu wa mambo haya tunayojadili, lakini kwenye vyama vyaya siasa huwa kuna Wanasiasa na bajeti hii tunayojadili leo imeandaliwa na wataalamu waliopo Serikalini wakitumia ushauri wa wataalamu wa Taasisi za kifedha duniani na kazi yao ya kila siku huwa ni kufanya utafiti ili kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayolikabili Taifa letu na kazi yao ya kila siku huwa ni kufanya kazi kiutaalamu kufuatana na utaalamu walioupata katika kutatua matatizo haya. Hivyo ndivyo walivyoweza kuipata bajeti hii ambayo ni bajeti iliyojaa matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye vipaumbele, tumeshaliongelea sana na sitaweza kurudia. Tumeona vipaumbele vilivyoweza kuongezewa fungu la bajeti ya mwaka huu. Lakini mbali na hiyo, hata kwenye uchambuzi wa kitaalamu inaonyesha kwanza bajeti hii kwenye upande wa mapato ya ndani ukijumlisha na ya Halmashauri, unapata shilingi trilioni 7.1. Lakini kwenye upande wa mishahara na matumizi mengineyo unapata ni shilingi trilioni 6.7. Kwa hiyo, kiutaalamu inaonyesha dhahiri kwamba bajeti hii inaweza kukidhi matumizi mengineyo pamoja na mishahara bila kutegemea fedha za nje. Hiyo ni sifa kubwa sana kwenye bajeti, kwa lugha nyingine ni kwamba fedha za nje zozote zile hazitapelekwa kwenda ku-*finance* mishahara pamoja na matumizi mengineyo. Kwa hiyo, fedha zile zote zitakwenda kwenye maendeleo, hiyo ni sifa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiangalia utegemezi, imepiga hatua kubwa mno kutoka 54% mpaka 17% na matarajio kufikia 10%. Hiyo ni hatua kubwa ambayo imeweza kujionyesha kuwa imeandaliwa kitaalamu.

Jambo lingine kwenye lile lile la utaalamu, ukiangalia mwenendo wa fedha za ndani zinazotengwa ku-*finance* maendeleo kwenye shughuli za maendeleo, mwaka 2005/2006 ilikuwa 23% lakini kwa sasa imekwenda mpaka 39%, ni hatua kubwa kwamba Serikali inatenga fedha za ndani ikiwa na mwelekeo wa kupandisha mwaka hadi mwaka zinazokwenda kwenye maendeleo. Hiyo ni sehemu ya kitaalamu mno na inaonyesha kwamba inaleta tija kwenye shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Watanzania kwamba tuna maana gani tunaposema hivi ni vipaumbele na vinasaidia viyi sekta nyingine? Tunaposema maji yamewekwa kwenye kipaumbele, inazisaidia Sekta nyingine. Unapokuwa umepata maji, ni moja kwa moja unasaidia mpaka Sekta ya Afya, kwani Sekta ya Afya haiwezi kwenda bila maji. Haiwezekani Muuguzi akafuata maji kilomita 12 huku anasubiri akahudumie wagonjwa. Lakini hata anapopangiwa kwenye eneo ambalo halina maji, inampa wakati mgumu kuamua pamoja na uzalendo kwamba akubaki na kuisaidia jamii iliyopo pale.

Vilevile kwenye elimu, unapompangia Mwalimu kwenye eneo ambalo halina maji anapata wakati mgumu sana, lakini pia hata namna ya kuandaa vipindi vyake kwa ajili ya watoto, ni kazi ngumu sana na hicho ni kipaumbele. Lakini hata kwa watoto, haya

yanatokea. Hata hivi tunavyoongea, katika Jimbo langu kuna vijiji vya Migilango, Kizonzo, Mseko, Kisharita na hata Ruono, ikishafika wakati wa kiangazi kuanzia muda huu mpaka Desemba, watoto wanasoma nusu siku ili wakatafute maji. Kwa hiyo, bajeti inapotengewa fedha za kipaumbele kwenye maji, maana yake ni kipaumbele kweli kweli, kinagusa maisha ya wanadamu ya kila siku, lakini inagusa na kwenye ile Sekta ya Elimu. (*Makofi*)

Hata kiustawi, nilishangazwa sana, nikaona mama mmoja anasema maji siyo kipaumbele. Hivi binti anayekaa na bibi yake, anapofuata maji kuanzia saa 12 jioni anarudi saa nane usiku hata kama ungempa Walimu wengi kiasi gani hawez i kufaulu masomo yake kama ataendelea na utaratibu huo. Hata kiustawi, binti anakwenda saa 12 anarudi saa nane usiku, ni wapi na wapi, kwamba unasema kuna bajeti inayolenga maji siyo kipaumbele.

Pia kwenye hilo hilo, tuangalie jamii za kifugaji, baba anakwenda kutafuta maji ya mifugo siku nzima, anaporudi mama anakwenda kutafuta maji usiku. Hiyo familia ikoje? Kwa hiyo, kwa kweli vipaumbele hivi vinalenga kuwaondoa wananchi wetu kwenye matatizo kiustawi pamoja na kupunguza umasikini.

Tuangalie kipaumbele cha barabara, kimeongezewa fungu kutoka lile la bajeti iliyopita. Unapotengeneza miundombinu, kwanza kwenye ustawi wa Sekta nyingine unakuwa umerahisisha. Kilimo kitaweza kufanikiwa vizuri, bei zitakuwa nzuri, lakini pia hata katika maisha ya kila siku ya binadamu unakuwa umesaidia sana, ndiyo maana nimekuwa nikipiga kelele sana kuhusu barabara ya Mto unaokwenda Mtekente hadi Urugu. Leo hii unapokuwa na mama mjamzito anabebwa kitandani, wanapita katikati ya maji, wanapimana kama ng'ombe wanaolima wapi, wana kimo kinacholingana, ni hatari mno. Lakini tunaposema Serikali imeweka bajeti, kipaumbele kwenye barabara, mtu anasema hiyo siyo kipaumbele, haitukani Serikali, lakini anawatukana wale wanaopata shida.

Kuna watu wengine labda siyo makosa yao, wamekulia maeneo ambako hizi shida hazipo. Mtu amezaliwa Ubungo, kasomea Ubungo, kawa Mbunge wa Ubungo, anaweza akabeza tu. Yeye kipaumbele chake ni mafuta ya gari yake tu, lakini kwa wale wanaoishi kijijini Serikali imewalenga na hivi ndivyo vipaumbele vya kweli na kweli wataweza kupiga hatua. (*Makofi*)

Nimeiona hata kwenye bajeti ya kivuli nikasema, kwa kweli labda siku nyingine hata hili neno kivuli labda mlitolee semina elekezi, maana yake inatoka kwenye kivuli inakwenda kwenye giza sasa. Haiwezekani mtu anayeijua Tanzania hii kwa ajili ya kukwepesha uchakachuaji eti aseme mafuta ya taa nayo yapandishwe iwe sawa na bei ya petroli. Kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakijiji wote wa Tanzania kuanzia watoto mpaka kwenye vituo vya afya wanatumia mafuta ya taa hayo hayo, unataka upeleke iwe sawa na bei ya petroli kwa sababu unakwepesha petroli isichakachuliwe! Kama watu wanavaa suruali za kubana, unasema basi na bei ya sketi nayo ipandishwe? Havihuiani! Hili

niwaambieni kwamba Watanzania mkiwa mnatambua sasa kwamba, “ukiona baba wa Kambo anakuchekesa, siyo kwa sababu anakupenda, ni kwa sababu anampenda mama yako.” Ukiwa kweli unampenda huyu Mtanzania huwezi ukatekenya panapoonekana patachekesha badala yake utalenga ule uhalisia na utatoa ushauri wa kitaalamu.

Nimeangalia bajeti ile ile uone ni kiasi gani inalenga kutekenya tu. Mtu anasema napunguza matumizi ya kawaida na wakati ule ule najua hii ni lugha nzuri, itawafurahisha Watanzania na wakati ule ule anasema naongeza mshahara wa kima cha chini. *This is elementary contradiction!* Ni vitu vinyopingana kwa uwazi kabisa, huwezi kupunguza matumizi ya kawaida ambayo *elementary essentially* ni mishahara na wakati ule ule ukasema mkono mwingle umeongeza mshahara. Huko ni kutaka *ku-confuse* umma kwamba yule anayeguswa na hili alipokee na huyu anayeguswa na hili aweze kulipokea.

Kwa kima cha chini, nimeangalia bajeti yao, wamesema matumizi ya kawaida wameyapunguza mpaka kile kiwango ambacho ni kama 7.9. Wakati ule ule ukizidisha kwa wafanyakazi waliopo ile Sh. 315,000/= ukizidisha unapata shilingi trilioni 6.5, ukitoa unapata shilingi trilioni 1.4, utaendesha kweli Taifa kwa shilingi trilioni 1.4 ununue madawa? Vifaa vya kufundishia, uendeshe majeshi, uendeshe vyombo vya usalama kwa shilingi trilioni 1.4 *that is the cross line*, haiwezekani. Kwa hiyo, kwa sababu unajua ni kivuli, hakuna sehemu yoyote utakayotumia bajeti hiyo, unataja tu ufurahishe watu. Lakini dhana ya kivuli huwa siyo hiyo, dhana ya kivuli unatakiwa utoe ushauri ambao una-make sense.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimeyasema hayo, kwenye hii bajeti, nitoe ushauri kwa Serikali. Kuna mambo ambayo ni ya muhimu sana ambayo mmeyaongelea. Mmeongelea fungu la vijana kuanzia kwenye mpango. Naomba nisisitize yale niliyokuwa nasema, kwanza lazima uwepo mfuko maalum kwa ajili ya vijana, na Serikali itoe tamko kwenye lile fungu, asilimia ile inayotengwa kwa ajili ya Halmashauri kupeleka kwenye maendeleo zilee vijana ili waweze kujajiri na ile iwe ni agizo mwaka hadi mwaka mnapokagua mwangalie Halmashauri gani imesaidia nini kuhusu vijana.

Nilisema wakati ule kwamba vijana wenyewe ujuzi wa useremala wakopeshwe vitendeakazi, watengeneze madawati na Halmashauri ziwalipe na ziwalipie ile mikopo watakayokuwa wamekopa kununua vifaa. Hili linawezekana na tutakuwa tumeshatibu ajira na tumetibu kwenye madawati. Kuna vijana wetu wa kike, nao watafutiwe vifaa vya kufumia, wafume *uniforms* zote za shule za Serikali na watakuwa wameshapata soko. Leo hii hata skafu yangu ambayo huwa napenda kuivaa ni *made in China* na watu hawana ajira na wana ujuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye upande wa uvuvi. Wametengeneza vizuri sana kwenye bajeti kwa kuondoa ile nanii, itashusha gharama za kupata nyuzi, lakini Serikali lazima iingilie mara kwa mara. Kuna watu wanaopewa majukumu ya kuratibu mambo ya maziwa na mabwawa, lakini wanageuza kuwa lile ni shamba lao. Mara kwa mara wanakamata watu na wakati mwingle watu wanakimbia hawafanyikazi.

Hilo ni tatizo na Serikali itoe agizo kote na liende mpaka Doromoni kule kwangu waache kukamata kamata watu. Serikali ina nia nzuri ya kuwafanya vijana wajiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi mabaya, nimeona mpango mzuri ulioletwa kwenye bajeti. Serikali iwe imara na kama tatizo ni sheria, leteni tuipitishe hapa. Haiwezekani kila wakati tukawa tunasema bila aibu kwamba mishahara hewa ilikuwa kiasi hiki. Tangu lini hewa ikapokea mshahara? Tuna watunza kumbukumbu, tuna anayelipa na kuna ofisi kule fedha zilikokwenda! Iwekwe sheria ambayo haitakuwa imepindisha, ikitokea kuna mtu amelipwa hewa, mtunza kumbukumbu na yule aliyelipa mwaka hadi mwaka awajibike moja kwa moja. Hiyo nadhani hata haihitaji kesi na haihitaji kuendeshwa muda mwingi pamoja na kwamba tunatakiwa tuwe na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naendelea kwenye lile la vijana, nimesema muda siyo mrefu tutakuwa na wanafunzi wengi sana wa Vyuo Vikuu ambaa wanamaliza Vyuo Vikuu, hivyo lazima tupanue wigo wa kujiajiri. Naendelea kusisitiza kwamba Serikali ilete hilo suala na isipoleta, mimi nitaleta kama hoja binafsi. Vijana wa Vyuo Vikuu watumie vyeti vyao vya kumaliza masomo kuweza kupewa mkopo. Tunamwanda daktari kwa gharama kubwa kuliko gharama ya kiwanja cha Sh. 200,000/=, inakuwaje tunapokea kiwanja cha Sh. 200,000/= badala ya kile cheti ambacho kimetafutwa kwa bei kubwa ya gharama za Serikali, na Watanzania ni watu waaminifu? Atakimbia aende wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala lingine la mbolea, kuna suala la pembejeo za kilimo hizo nazo zimekuwa hazifiki kwa walengwa. Nia ni nzuri sana, lakini kwenye hili nalo iwepo sheria ambayo ni kali na adhabu kali ili watu waogope kufanya hayo. Tunapokuwa tumetoa hivyo vitu, tuhakikishe kwamba vinafika na kama havijafika, iwe ni *straight* wale waliohusika waweze kuwajibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la chakula. Hii dhana ya hifadhi ya chakula kwenye maghala yaliyoko kwenye kanda inasaidia sana, wakati wa upungufu wa chakula inashusha bei, lakini wakati wa ziada ya chakula inainua bei ili mkulima asipate hasara. Lakini inapotokea tatizo kwamba yule mkulima maskini aliyekusudiwa anapokwa na baadhi ya wajanja, nadhani inapokuwa imegundulika Serikali ichukue hatua bila kusita. Hiyo itasaidia sana kuweza kujenga heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kundi la watendaji vijijini, naishauri Serikali watekelezaji wetu wa kwanza kabisa wanaokimbia na ilani ni watendaji wa vijiji, wangaliwe, waongezewe kipato ili waweze kutekeleza vizuri ilani yetu na kweli hao ndio ambaa huwa tunawategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia zote mia moja huku nikiwa kifua mbele. (*Makofi*)

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote, kwa kuwa ni mara ya kwanza nazungumza, naomba nimpongeze Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika Mwanamke wa kwanza Tanzania. Pia, nakipongeza

chama changu cha CHADEMA kwa kuweza kunitua mimi kuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara. Pia, nisiwasahau wananchi wa Hanang ambao walinipandisha chati na kuniwezesha kufahamika kwamba ninafaa kuwa Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema chochote, mwenzangu aliyejipa amesema kwamba Kambi ya Upinzani imepandisha bei ya mafuta ya taa. Naomba ninukuu kwa kusema kwamba ukurasa wa 31, Kambi ya Upinzani imesema kwamba inapendekeza pia kuwianisha viwango vyta ya mafuta ya taa na bei ya mafuta ya dizeli na petroli ili kudhibiti uchakachuaji wa mafuta ambao unaligharimu Taifa fedha nyingi sana na kuleta uharibifu mkubwa sana. Nimenukuu hivyo kwa sababu naona kwamba anawadanganya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nielekee moja kwa moja kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na ninaomba niende kwenye sehemu ya usimamizi wa fedha za umma ambayo iko ukurasa wa 33. Hii ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, iliyotolewa mwaka 2009/2010 imekiri kwamba kuna kutetereka kwa udhibiti na usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na hayo maneno nikisema kwamba, basi katika kurekebisha kwa kuunda nafasi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali au Msaidizi atakayeshughulika na Usimamizi wa Serikali, naomba niseme kwamba mfumo huu peke yake hautoshi kwa sababu huyu peke yake hataweza kufuutilia mpaka katika vijiji vyetu miradi inakoendelea na Wilaya na Mikoa. Nadhani ni vyema kabisa kwamba Mpango huu sasa ufuate viwango vyta kimataifa vyta utoaji wa taarifa za kiuhasibu. Pia Serikali ione ni muhimu sasa kufuutilia fedha zile wakati zinapotolewa tu na endapo ubadhirifu utaonekana, basi Serikali iwawajibishe wanaohusika mara ubadhirifu huo unapotokea. Endapo hatufanyi hivyo, ni wazi kabisa kwamba hakuna tunalolifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapendekeza kwamba ni vyema kabisa sasa ifikie mahali tuweze kuunda mpango mwengine wa ufuutiliaji wa fedha za umma kule Wilayani kwetu. Kwenye Wilaya mbalimbali, Halmashauri na Mikoa tuwe na Kamati ya ufuutiliaji wa fedha za umma inayotoa taarifa kwa Mkaguzi Mkuu pia. Hii itatusaidia sana kwa sababu ubadhirifu mwingu unafanyika kwenye kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie sehemu ya raslimali watu. Sehemu ya raslimali watu imeonesha wazi kwamba tuna mgawanyo ambao unaonekana siyo sahihi kwa upande wangu. Kwanza kabisa sehemu ya VETA kupangiwa asilimia mbili ni ndogo mmo. Tufahamu kabisa kwamba endapo tungewekeza kwenye VETA ni wazi kabisa kwamba wale vijana wetu wanaomaliza Kidato cha Nne, wangeelekea huko na wengine wanaomaliza Kidato cha Sita wangeelekeza kwenye VETA na wangeweza kujajiri wenywewe au kuajiriwa.

Sasa tunapoelekeza asilimia mbili tu, maana yake tunaangusha raslimali watu wengi huko vijijini na mfahamu kabisa kwamba, kama safari hii shule nyingi zimewafelisha vijana wetu na hawana mahali pa kwenda, wamebaki vijijini hawajui la

kufanya. Sasa kungekuwa na VETA za kutosha, ni wazi kabisa kwamba tungewawezesha hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la VETA linakua gumu kwa sababu ya kusema kwamba tutafanyaje na tutajengaje. Mimi naomba nitoe mfano, wakati ubinafsishaji ulipokuwa unafanyika kwenye Wilaya ya Hanang, wamebinafsisha mashamba ya NAFCO, lakini Serikali haijaona kwamba kulikuwa na majengo yanayoitwa CMC ambayo yalijengwa kwa ajili ya shule, badala ya mabwana shamba wale kupelekwa Canada wawe wanosomea Tanzania, kumbe Serikali ingechukua yale majengo yakawa ya VETA yakawawezesha wanafunzi wengi kuelekea pale na wakawa wamejitosheleza kwenye u-raslimali watu kwa kujitegemea wenyewe. Sasa naomba Serikali iangalie hilo upya, kwa maana kwamba yale majengo yapo, yamebinafsishwa, kama inawezekana, basi hiyo sekta binafsi ielekezwe kwa kuwekeza kwenye VETA zaidi badala ya yale majengo ambayo yako CMC Wilaya ya Hanang kukaa bila kuwa na kazi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la uwekezaji wa asilimia nne kwenye mikopo. Hii mikopo imeanza siku nyingi na ilitakiwa irejeshwe: Je, marejesho hayo yalipelekwa wapi? Kwanini ipelekwe asilimia nne kwenye bodi ya mikopo? Mimi nadhani marejesho yale yanayoendelea kurejeshwa, yarudi yaendelee kufanya kazi ya kukopesha wanafunzi, asilimia nne iende kwenye VETA na asilimia mbili ibaki kwenye mikopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Ninakwenda hapa ili niweze kielezea Serikali kwamba, hivi ni kwanini tuweze kuwekeza kidogo kwenye Sekta ya Kilimo na Mifugo wakati asilimia 75 ya raslimali watu wako hapo? Hivi ni kwanini tusiwekeze kwa asilimia kubwa pale au kuangalia sekta ya kilimo kama vile umwagiliaji, tukahakikisha kwamba programu hii ya umwagiliaji inafanya kazi vizuri na inaweza kuzalisha vizuri? Serikali haioni kwamba hatuna sababu ya kuagiza ngano nje ya nchi wakati ardhi yetu ni nzuri, ina rutuba ya kutosha, tuna mabonde ya kutosha, tuna maji ya kutosha na tuna mabwawa na mito na kadhalika? Hivi kwanini tusiwekeze sehemu kubwa kwenye umwagiliaji tuachane na suala la kununua ngano nje ya nchi? Tuna ngano ya kutosha hapa kwetu, mfano, Wilaya ya Hanang, Karatu na Njombe. Wote hawa ni wakulima wa ngano na ardhi ni nzuri, kwanini tusiwekeze huko ili tuachane na kuagiza ngano nje ya nchi na watu wetu waweze kujaajiri kwa kuuza ngano ndani ya nchi yetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ya ngano yaliyobinafsishwa ya Hanang yanalimwa ekari 9,000 tu badala ya kulima ekari 35,000. Hivi tuna sababu ya kuwabinafsishia hawa watu? Kumbe Serikali ingeweza kuendelea kulima kama kawaida badala hata ya kubinafsisha haya mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba sasa ielekeze kwenye kuondoa umaskini kwa wananchi kwa kuweka masuala ya umwagiliaji kwanza kwa nchi hii, fedha zote zielekezwe kwenye umwagiliaji. Hii shilingi bilioni 926 kuwaambia wananchi kwamba tumetoka kwenye ekari 330 tunakwenda kwenye ekari 1000, hivi nchi hii ekari 1000 ni kitu gani kwa umwagiliaji wakati tuna mabonde mengi ya kutosha?

Tunaweza kufanya hiyo kazi! Naomba hili liangaliwe sana na litatusaidia sisi wananchi tuondokane na umasikni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la ufugaji na kilimo, pia tumesahau kuwa na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo. Mazao ya kilimo tunasema tunasindika. Kwa kweli tunasindika kwa kiwango kidogo sana. Naishauri Serikali iwekeze kwenye sekta binafsi fedha za kutosha ili waweze kufungua viwanda vya kutosha hapa nchini ili watu wetu waweze kuajiriwa na pia waweze kupata mahali pa kuuza mazao yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunalalamika kuhusu migogoro ya mifugo, hatuna jinsi nyingine ya kupunguza mifugo zaidi ya kuchinja, namna ya kuwachinja ni kufungua viwanda vya kutosha ili waweze kuchinjwa na tuweze kuuza raslimali hizo ambazo zimesindikwa. Wananchi wetu wanadanganywa kwamba tunafungua viwanda, siyo kiwanda kinachofunguliwa, ni machinjio. Machinjio ya Ruvu, Shinyanga na ya hapa Dodoma. Je, maeneo yote ambayo tupo wafugaji wengi, kwanini wasifungue viwanda vya kusindika nyama tuuze badala ya kumuuzza ng'ombe kama alivyo mzima? Tuwekeze huko tayari inakuwa ni raslimali tosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze pia sehemu ya sheria ya usalama barabarani. Hii sehemu ya usalama barabarani wameweka faini ya Sh. 20,000/=, sasa wanataka ipandishwe kwenda Sh. 50,000=/. Kwa kweli naomba niseme kwamba tunapozalisha kitu kingine, tunazaa kingine. Ni wazi kabisa kupandisha hiyo faini moja kwa moja ina maana sasa tutoe rushwa ya kutosha kwa sababu hatuwezi kumudu hiyo faini ya Sh. 50,000=/. Sh. 20,000/= ilikuwa tatizo: Je, Sh. 50,000/= inawezekana? Mimi naomba Serikali ifute kiwango hiki ibaki ile Sh. 20,000/= ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye suala la utawala bora. Suala la utawala bora tumezungumzia suala la migomo ya wanafunzi wetu, lakini sehemu kubwa inaonesha wazi kabisa kwamba vijana wetu wanapogoma tunaamua kuwfukuza au kuwasimamisha kuwapa *suspension*. Kwanini Serikali isitatue tatizo la hawa wanafunzi? Kuna nini? Inafahamika wazi kwamba wanafunzi walianza kulalamika kabla, wakaleta taarifa, Serikali ilikaa na ikaona kabisa kwamba kwa kweli walistahili kulipwa fedha za *field*. Sasa badala ya kulipa fedha zile za *field*, matokeo yake wanasema kwamba wamegoma, wameandamana, wamefanya nini na kufukuzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Serikali haioni ni nani anayehusika pale kuchelewesha fedha hizo za wanafunzi? Je, Serikali haikumtambua huyo mtu au huyo *Dean* anayehusika na masuala hayo akachukuliwa hatua? Mwezi wa nne walifukuzwa, mwezi huu wamefukuzwa na mwezi unaofuata watafukuzwa, lakini ukiangalia na hata sisi tuna wanafunzi pale, tuna watumishi pale, tumesikia kwa masikio yetu kwamba wanamlalamikia mtu, lakini kama wanamlalamikia huyo mtu, kwanini asiondolewe hapo *UDOM* ili wafanyakazi wafanye kazi kwa amani, na hata wanafunzi wasome kwa amani? Mtu akishachokwa inabidi asogezwe ili watu wakae kwa amani nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sehemu ya Polisi. Polisi wanalinda amani ya raia, usalama wa raia na mali zao, lakini kwenye bajeti Polisi hawaonekani kama ni watu wanaostahili kuangaliwa sana. Bajeti ya shilingi bilioni 7.4 ni kitu gani kwa wenzetu Polisi? Wanataka majengo, wanahitaji vituo mfano mzuri ni Wilaya ya Hanang, vituo vya Polisi viwili wanapangisha kwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kupangisha ni kitu gani? Wengine wanasaidiwa ili wakae kwa muda. Mimi naona sasa Wizara iangalie suala hilo hasa Wilaya ya Hanang. Basutu walipata mafuriko mwaka wa 1998, majengo ya Polisi yote yalikuwa kwenye mafuriko. Mwaka 2000 tena mafuriko yakarudi, ndiyo moja kwa moja hapakustahili tena eneo hilo. Kwanini sasa Polisi wasijengewe maeneo mapya? (*Hapa kengele iligonda kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika bajeti ya mwaka 2011/2012. Kama tunavyofahamu, bajeti hii imetoa vipaumbele kama ifuatavyo: imetoa kipaumbele kwenye umeme, maji, miundombinu, kilimo na ajira. Ili vipaumbele hivi viweze kutekelezeka, wakati umefika sasa Watanzania tuweke msukumo katika kufanyakazi kwa bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika fungu la maendeleo ya jamii. Bajeti kubwa ya fungu hili inatokana na mikopo kutoka nje kwa wahisani. Taifa linapotegemea mikopo kwa ajili ya maendeleo ya jamii, ni hatari. Kwanini nasema hivyo? Endapo wahisani hawa watabadilisha mawazo wasitoe hizo fedha, hakika miradi mingi ya maendeleo itakuwa imekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusema kwamba tusikope, wala tusichukue kabisa misaada, hii ni kawaida katika Taifa lolote lile kukopa na kuchukua misaada. Lakini Taifa letu ni lazima tuwe waangalifu. Tunapokopa ni lazima tuangalie makubaliano ambayo yanatulinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taratibu za ulipaji wa madeni, kuna kitu kinachoitwa *statute of limitation*. Kwa ruhusa yako naomba nifafanue kwa Kiingereza. “*Expiration of time limit for enforcing the collection of debts is called statute of limitation.*” Maana yake pamoja na kwamba Serikali yetu imetenga asilimia 14 kwa ajili ya kulipa madeni nadhani ingekuwa ni vyema tusiitumie hela yote hii kulipa madeni. Kwani inawezekana kabisa kuna madeni mengine ambayo yamepitwa na wakati na hatutakiwi kuyalipa. Wakati wa uongozi wa Baba wa Taifa hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, nchi yetu ilipata misamaha mingi ya kodi. Misamaha hii tulipata ama kwa kushinikiza ama kwa kukataa kulipa kwa kutoa sababu za msingi kabisa. Wakati umefika sasa Taifa letu tuwe waangalifu, tusikimbilie kulipa madeni hata yale ambayo hayana umuhimu wa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie msamaha wa vifaa vya ulinzi na usalama zikiwemo *CCTV Cameras*, ma-*magnetometers* na vifaa vingine vya ulinzi. Sioni kama kuna sababu ya msingi ya kuondoa kodi kwenye vifaa hivi ukizingatia kwamba vifaa hivi havipunguzi uhalifu nchini. Nashauri vifaa hivi viendelee kutozwa kodi ili ile pesa ielekezwe kutoa mafunzo kama ifuatavyo: Kuna programu inayoitwa *Primary Prevention Programme*. Katika programu hii, vijana wetu watafundishwa yaliyo mema, watafundishwa jinsi gani ya kuepuka uhalifu. Vile vile kuna programu nyingine ambayo inaitwa *Secondary Prevention Programme*. Katika programu hii, wale ambao wamefanya uhalifu au wamevunja sheria watapewa mafunzo ya kuwasaidia ili waweze kuwa raia wema. Nadhani ingekuwa vyema Serikali ikaendelea kutoza vifaa hivi ushuru na hiyo pesa itumike kuwafundisha vijana wetu ili hatimaye tutatue tatizo letu la hali ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wote kwa pamoja tusaidiane kuamua kama bajeti hii inalenga walio wengi au la. Je, bajeti hii inazingatia mama mjazito anayetembea kilomita 30 kwenda kliniki wakati mfukoni hana hata Sh. 100/= ya kununua *aspirin*? Je, bajeti hii imezingatia watoto wa mitaani wanaozagaa mitaani kwa sababu wazazi wao wameshindwa kuwalea kwa ajili ya umaskini uliokithiri? Je, bajeti hii imezingatia wale wamachinga ambao hawana mitaji na hawana maeneo ya kufanya biashara zao? Je, bajeti hii imemzingatia yule Mwalimu anayeshinda na watoto shulenii kwa kuwafundisha katika mazingira magumu na baadaye anakopwa mshahara wake? Je, bajeti hii imemzingatia yule Daktari na Muuguzi anayefanya katika mazingira magumu na hatimaye kupunjwa mshahara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, bajeti hii imemzingatia yule Hakimu na mtumishi wa Mahakamani anayepunjwa malipo yake na kutuhumiwa kwa kupokea rushwa? Je, bajeti hii imezingatia wale wazee wastaafu ambao mpaka sasa hivi wanapigwa danadana kuhusu haki zao? Je, bajeti hii imezingatia wale akinamama wanaozalishwa watoto na kushindwa kusaidiwa kulea watoto hawa na kuhangaika mitaani? Je, bajeti hii imezingatia wale waathirika ambao uwezo wao wa kufanya kazi umepungua? Je, bajeti hii imezingatia wale vijana wanaofanya uhalifu na hatimaye hawapati msaada wowote wala ajira? Je, bajeti hii imezingatia yule mjane anayenyang'anywa kila kitu baada ya kufiwa na kuachiwa pea moja ya khanga? Je, bajeti hii imezingatia wale vijana wanaoendesha pikipiki na kutozwa ushuru mkubwa ambao hawana uwezo nao? Je, bajeti hii imezingatia wale wananchi wa Jimbo la Kwimba ambao wana mabomba ya maji yasiyotoa maji na badala yake yanatoa matope na vyura?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ningependa unisaidie kuamua kama bajeti hii inagusa Watanzania walio wengi au la? Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi. Naomba niwashukuru pia wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kuendelea kuchapa kazi na ujumbe wangu kwao kwamba "hakuna maisha bora yanayopatikana ila kwa kuchapa kazi." Ujumbe wangu kwa vijana walioko vyuoni, "kamwe maendeleo au maisha bora hayataletwa kwa maandamano, msidanganyike, kumbukeni fimbo iliyoko

mkononi ndio iuayo nyoka.” Yaani kamata kwanza shahada au stashahada halafu, utafute siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inatekelezeka, ni bajeti nzuri ,tuna kazi kubwa ya kuisimamia utekelezaji wake. Naishukuru Serikali kuweka vipaumbele na naomba nianze na kipaumbele cha kwanza, yaani umeme. Ni kweli kwamba kukosekana kwa umeme ni tatizo kwa wananchi, ni tatizo pia kwa uzalishaji wa viwanda vyetu, lakini viko vyanzo vingi ambavyo vimeainishwa na tunaamini kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilivyo Serikali sikivu itafutilia jambo hili na kwa uhakika tutapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi iko Mkao wa Lindi, Songsongo. Tunategemea mikataba ya gesi ya Songsongo isiwe na mafundo ili Serikali ikitaka kurudia kama ikiona yanayotekelizwa hayaendi vizuri Serikali iweze kubadilisha mikataba hiyo. Tunaambiwa Songsongo nao wamekodisha shughuli zao kwa *Pan African Energy*. Je, mikataba hiyo ikoje? Kama Serikali inalaumiwa kwa mikataba ya madini, basi kipindi hiki ni wakati wa kujisahihisha na tunategemea mikataba iwe wazi na gesi ipatikane isaidie wananchi nishati ya kupika ili tupunguze kukata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TANESCO* nalo tunawalaumu sana, lakini hatujaua kuna tatizo gani. Inawezekana sisi wadau na Serikali pengine hatulipi ankara zetu, kwa hiyo, *TANESCO* wanakosa mtaji wa kuijendesha. Liko wazo la kuleta wabia sekta binafsi. Ni wazo zuri, lakini ningombwa nishauri kwamba Serikali iwe makini katika hili ili mtu wa kawaida asije akapata matatizo kwa sababu ya gharama kubwa za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa bajeti ya umwagiliaji ni shilingi bilioni 926. Nia ni kutoka kwenye hekta laki 330,000 zinazomwagiliwa kufikia hekta milioni moja. Nafarijika sana na hii bajeti kwa sababu wako wakulima wa *Lower Moshi* Mkao wa Kilimanjaro ambao wanalima mpunga na kuna hekta 2,300. Ni *scheme* ya siku nyingi iliyoanza miaka 25 iliyopita na *scheme* hii iko pia kule Ndungu Wilaya ya Same. Wakati umefika kwa *scheme* hizi kukarabatiwa kwa sababu zina *impact* kubwa, na kama zimekaa kwa miaka 25 zinafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo chetu kinarudishwa nyuma na watendaji wabovu hasa Watendaji wa Vijiji, wakiungana na Wenyeviti wa Vijiji, wakiungana pamoja na Wakala wa Mbolea wanakwenda wanarubuni wananchi, wanawalipa hela kidogo, wanaweka sahihi katika vocha. Wakala anapeleka vocha Benki, analipwa hela, lakini ukweli ni kwamba anakuwa mbolea ile hajaitoa kwa wananchi na ndiyo maana wananchi wanaendelea kulalamika. Mfumo wa vocha za mbolea ni mzuri, lakini kuna haja ya usimamizi mzuri zaidi. Pengine ni vizuri Waheshimiwa Madiwani wahuishwe kwenye kusimamia maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imewajali pia wafugaji, imeondoa ushuru kwenye malighafi ya kutengeneza chakula cha mifugo, lakini pia imeondoa VAT katika malighafi ya kutengeneza chakula cha kuku. Nafarijika sana kwa sababu wako

akinamama wengi sana ambao wamechukua mikopo midogo midogo kwa ajili ya kufuga kuku wa kienyeji kama chanzo cha mapato yao.

Bajeti hii imejali pia wajasiriamali, lakini naomba nijikite kwa wale ambao wanasindika, wako takribani 250. Hawa ningeshauri Serikali kupertia *SIDO* wapate mafunzo zaidi na pia wapatiwe mashine ya kusindika vyakula hivyo. Tusinghau kwamba wasindikaji hawa kwa sababu ya ufunguzi wa soko la Afrika Mashariki, inabidi washindane na wenzao wa nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya elimu ya shilingi bilioni 2.2 ni asilimia 12 zaidi ya bajeti ya mwaka jana. Serikali ilijenga Shule za Kata na zilikwenda vizuri na ziliingiza wanafunzi wengi sana. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwa hilo na ninaishauri Serikali nguvu ile ile iliyojenga Shule za Kata iendelee ili ziweze kukamilika na kuimarika.

Naipongeza Serikali, wanafunzi wengi wamechukuliwa kwenye Vyuo vya Ualimu, kwa hiyo, tuna uhakika na inawezekana kipindi wana-graduate mwaka huu tutapata walimu wengi kutoka Vyuo vya Ualimu na walimu wamehakikishiwa ajira katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko Shule za Sekondari ambazo zilikuwa na Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne. Lakini Serikali ikaamua kutoa Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne ikaziweka kwamba ni Shule za Sayansi za Wasichana. Mfano wa hizi shule ni shule kongwe ya Ashira, Weruweru na ya Machame Mkoani Kilimanjaro. Hizi shule zina maabara, hosteli na kila kitu isipokuwa zinahitaji Walimu wa Sayansi.

Ninaishauri Serikali, kwa vile tunakwenda kwenye mfumo wa asilimia 50 kwa 50 Bungeni na Serikalini tutahitaji Madaktari wanawake na Wahandisi wanawake, ninaomba Serikali ipeleke Walimu wa Sayansi na Serikali inaweza kuweka wazi mfumo ule wa kuajiri wastaafuli ili waweze kusaidia katika shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna ukaguzi ambao unatakiwa ufanywe kwenye Shule za Msingi na za Sekondari. Wako Walimu ambao wanakwepa kufundisha hata asilimia 30 ya vipindi ambavyo wanatakiwa kuvifundisha. Lakini Idara ya Ukaguzi imekuwa kama Idara Yatima kule kwenye Halmashauri. Hazina vifaa, pikipiki wala magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, Shule za Msingi na za Sekondari ziko mbalimbali. Mimi ningeshauri ikiwezekana kwa vile hawa wanaripoti kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu ikiwezekana waripoti kwa Mkurugenzi, lakini pia na Wakurugenzi wapewe agizo kwamba wale Walimu ambao wanakwepa majukumu yao wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana takriban wanafunzi laki tisa wamemaliza Kidato cha Nne na katika hao, wanafunzi 38,000 tu waliingia Kidato cha Tano. Lakini sambamba na hilo, tuna vyuo vya wananchi ambavyo viko 53 nchini na katika hivyo

Vyuo tisa tu ndio vinafanya kozi ndefu. Vingine vyote vinafanya kozi za kushona na kupika miezi mitatu au sita.

Ningeishauri Serikali, hatuna haja ya kujenga vyuo vipywa ya *VETA*. Mitaala ya hivi vyuo vya wananchi viongezwe ili iweze kuchukua majukumu ya Vyuo vya *VETA* pale ambapo hakuna Chuo cha *VETA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya Watanzania imeongezeka kutoka milioni tisa wakati tumepata uhuru mpaka sasa hivi tuko milioni 43. Kwa uhakika lazima mazingira yataharibika na mazingira yameharibika katika kila kona ya Tanzania. Katika misitu 540 tulionayo, hekta 400,000 zinatoweka kila mwaka. Kwa sababu kuni na mkaa zinatumika kwa asilimia 90 kama ni nishati na asilimia 10 tu ndio nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipenda hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, tunapenda hifadhi ya Serengeti na Ngorongoro, tunapenda utalii, tunapata kipato kutoka huko. Ninaomba kwa hali na mali Serikali ibuni nishati mbadala ili tuweze kuokoa misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa kwamba katika Ziwa Victoria, magugu maji yale, Wizara ilipeleka wadudu wa kula yale magugu. Kwa hiyo, Ziwa Victoria likawa safi. Kule Kilimanjaro Wilaya ya Mwanga kuna Ziwa linaitwa Jipe. Ziwa hili limefunikwa na magugu sana, ni *shared waters*, tunashirikiana na Kenya. Lakini ukiangalia upande wa Kenya ni kweupe. Naomba Serikali iliangalie hili kwa ajili ya kuweza kumaliza magugu ya Ziwa Jipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye kipaumbele cha miundombinu. Tumesema tunapenda utalii, tunapenda hifadhi zetu na tunapata fedha. Lakini kule Kilimanjaro karibu na mji wa jirani unaitwa Taveta karibu na mji wa Tanzania unaitwa Himo mkoa wa Kilimanjaro, wenzetu wanajenga *airport* kubwa ya Kimataifa. Naiomba Serikali iliangalie namna ya uwekezaji katika kiwanja chetu cha *KIA*, la sivyo tunaweza tukamezwa na hiki kiwanja cha majirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni tani 200, zinazotegemewa kununuliwa na Serikali. Naipongeza Serikali, lakini pamoja na nia njema ya Serikali ya kununua hizi tani 200, pamoja na ufunguzi wa Soko la Afrika Mashariki, pamoja na uhuru wa Sudan ya Kusini unaokuja mwezi ujao na ripoti ya ukame Mikoa ya Kaskazini na ripoti ya ukame Mikoa ya Magharibi, naiomba Serikali iongeze kiasi hiki cha tani 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie na michezo. Michezo ni afya, furaha na ni ajira. Naomba niwapongeze timu ya Simba na Yanga, nimeona wamefanya vizuri, lakini niombe Serikali iendelee kui-support *TFF* kwa ajili ya michezo kama *football* na *netball* iendelee kuwa mizuri. Kuna michezo ya *basketball* ambayo inategemea sana vijana warefu ambao tunao nchini.

Kwa hiyo, ninaomba tuwe na Thabiti wengi wapeperushe bendera yetu nchini na nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia yale ambayo yapo. Kwanza, napenda kuunga mkono kabisa bajeti hii ya Serikali. Najua ni nzuri, imegusa maeneo mengi ambayo kwa kweli ilikuwa ndio kilio cha wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, naomba nieleze kidogo kuhusu Pensheni ya Wazee. Kila wakati tunapigwa simu kwamba labda mfumo wa kuwalipa hawa wazee ubadilike kidogo, badala ya kulipa kwa miezi sita, iwe kwa kila mwezi. Naomba sana kwa sababu nimepigwa simu mara nyingi wakiomba iwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naomba nichangie ni kuhusu maji. Mradi wa maji ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia, ni mradi ambao umeanza muda mrefu lakini utekelezaji wake unachukua muda mrefu sana kiasi cha kuwakatisha tamaa kabisa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu kuna vijiji vingi ambavyo vilitajwa kabla sijawa Mbunge kwamba vitapewa maji kwa kufadhiliwa na Benki ya Dunia, lakini mpaka leo hii imekuwa ni kero kubwa sana, sijui kuna nini. Nafikiri hela za wenzetu zimekuwa na masharti makubwa sana, inakwenda miaka mitatu mpaka mine, kuna nini huko? Naomba Serikali iliangularie suala hilo, kama kweli hii miradi imedhamiriwa kuwasaidia wananchi basi ingetekelezwa kwa haraka zaidi isiwe kama ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuliongelea ni barabara hii ambayo nimeuliza swali hapa asubuhi ya leo, barabara ya Isyonje kwenda Makete. Kama kweli Serikali imedhamiria kuongeza pato la Serikali, barabara hii ya Isyonje kwenda Makete isingekuwa ni barabara ambayo haikuwekwa kwenye mpango wa kujengwa kwa lami kwa sababu kikwazo kikubwa kabisa cha kuwapeleka Wawekezaji katika Milima ile na sehemu ile ni barabara. Watu wanatamani wajenge hoteli kule, lakini wakijenga nani atakwenda kule, barabara mbaya, hata kama wanaikarabati kwa kiwango cha changarawe kwa muda wote lakini kwa kweli ni barabara ambayo isingebezwaa na Serikali, ilitakiwa iwekwe kwenye mpango wa kuitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ihakikishe kwamba barabara hii inapata hela hata kama ni za dharura. Kitulo ni mahali ambapo kuna kila aina ya mambo ambayo ukienda kule utashangaa. Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu ambaye hajawahi kufika Kitulo akifika atakuwa anashangaa, ni maeneo ambayo kwa kweli unasema hapa Mungu aliumba Dunia na inawashangaza watu wengi. Mimi nimefanya kazi pale Kitulo, kila wakati nilikuwa naenda katika Milima ile nashangaa jinsi Mungu alivyouumba. Sasa kwa nini tuwanyime watu wasiende kushangaa Mungu jinsi alivyouumba Dunia eti kwa sababu ya kikwazo cha barabara? Naomba Serikali ifikirie kuitengeneza barabara hii ya Isyonje kwenda Makete ili wawekezaji waweze kwenda kule. Huhitaji kuhubiri injili kule, ile Milima inamhubiri Mungu yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Songwe kinajengwa na Serikali haina mpango wowote kuangalia ni namna gani wataendesha shughuli ya

biashara pale. Nafikiri biashara mojawapo ambayo ingesaidia kabisa uwanja ule uweze kufanya kazi vizuri ni kuweka fursa ya barabara kama hizi ambazo zitasaidia kuwaleta watalii wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Ujenzi kama hajawahi kufika Kitulo basi siku moja afike aangalie. Nafikiri akishaangalia, hatafanya ajizi tena kutotenga hela kwa ajili ya ujenzi wa barabara pale. Tunahitaji kuu-*promote* utalii na huwezi uka-*promote* utalii kwa kusema maneno, hapana! Lazima uweke miundombinu ambayo itasaidia kukuza utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1993, nilikuwa Singapore, tulipokuwa darasani Mwalimu anafundisha kwanza ku-*promote* utalii katika nchi yake, anasema kama umefika Singapore hujafika Sentosa, hujafika Chinese Dynasty, hujafika kwenye Jumba la Sayansi pale, bado hujafika Singapore lakini ukienda kule ni *very artificial* wala siyo *natural* kama Kitulo. Unaona tu watu wametengeneza ndege, kuna Kasuku yupo pale basi, ndiyo hayo tunaona lakini vitu vyote wametengeneza, maua mazuri na unajua Singapore ni Mji mzuri, basi ndiyo hilo lakini sisi kule Kitulo unaangalia vitu *very natural* na wewe unashangaa. Kwa msisitizo huu, naomba Waziri atusaidie kuhakikisha kwamba ile barabara inajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu Mgodi wa Madini wa Songwe ambao wanasema una madini ya thamani sana. Kuna wakati ambapo nilienda na Waziri wa Nishati pale aliangalia na wakati mwingine Rais pia alipita pale na akaamuru lile Gereza la Songwe lihame ili ule Mgodi uanze kufanya kazi, lakini bado sijajua ni kitu gani hapo katikati kimechelewesha ile kazi isiweze kuanza. Naomba labda Waziri kwa sababu anajua aweze kueleza katika majibu yake. Naomba ule mradi kama kweli umefikia mahali pa kufanya kazi uweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo naomba kulieleza zaidi ni kwamba katika hotuba ya Waziri wa Fedha, ukisoma ukurasa wa 59, ameongea sana kuhusu kuwapa uwezo Madiwani. Kwa kweli Madiwani ndiyo ambao tunafanya nao kazi kwa karibu sana, kwamba Serikali itahakikisha inawapa uwezo Madiwani ili wawze kutimiza majukumu yao vizuri. Kwa kweli hapo naipongeza hotuba ya Waziri, naipongeza Bajeti hii na nasema ahsante sana kwa sababu mkifanya hivyo, mtakuwa mmeshatuokoa sana kufanya kazi vizuri na Madiwani wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kulichangia ni kuhusu mbolea. Kule kwangu kuna maeneo mengi na yapo maeneo tofautitofauti, ukienda kule Umalila, Tarafa ya Isangati, ukija huku Mporoto wao wanaanza kulima mahindi mwezi wa saba wanaita *dry farming* na wangehitaji wapate mbolea mapema zaidi. Naomba kama Waziri hajalifahamu hilo atusaidie ili wale wananchi wapate mbolea mapema, hasa kule Ilembo na maeneo mengine ya Santiria maana mwezi wa saba ndiyo wanapanda mahindi. Hata hii mbolea ya kawaida, naiomba Serikali ijaribu kuwashisha zaidi, kumekuwa na kero kubwa, wakati mwingine mbolea zinachelewa na watu wameshalima mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, bado tunahitaji uboreshaji wa ugawaji wa hizi mbolea za ruzuku, imekuwa ni kero na matatizo makubwa sana. Nafikiri Serikali iko makini na kuna Watalaaam amba wanajua ni njia zipi ambazo wanaweza wakazibuni zitakazosaidia kuleta ufanisi katika ugawaji wa mbolea hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti nina swalii, bei ya simenti pale Songwe au Mbeya ni kubwa zaidi kuliko Dodoma. Nilikuwa najiuliza hivi kuna nini ama kuna mkataba gani uliowekwa hapo kuifanya bei ya simenti inayozalishwa Songwe, Mbeya bei yake kuwa kubwa kuliko inavyouzwa hapa Dodoma na wakati huo imesafirishwa kwa magari na pale haisafirishwi. Naomba Waziri wa Viwanda hapa anisaidie, kuna nini.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, lakini pia Kiwanda cha Nguo cha Songwe, ni Kiwanda ambacho walichukua Wawekezaji lakini naona mashine zinanyofolewa, hakuna kitu kinachoendelea pale. Nilijaribu kwenda kwa Waziri kumweleza suala hili, lakini sijapata jibu ambalo ni sahihi, naomba pia Serikali iangalie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni Kiwanda cha Nyama cha Mbalizi; katika Mpango wa Miaka Mitano, nimeona kwamba ni sehemu tatu tu ambapo viwanda vitafunguliwa au vitafufuliwa kama Shinyanga na maeneo mengine lakini Kiwanda cha Nyama cha Mbeya hakipo kabisa kwenye Mpango. Naomba Serikali itueleze kwamba ina mpango wa kweli wa kuendeleza kile kiwanda au inataka kukifuta kabisa? Kama ina mpango huo, mbona kwenye mpango wa Serikali hakipo kabisa? Naomba Waziri atakapo jibu, anisaidie kulielezea hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu fidia ya wananchi wa Songwe Kiwanja cha Ndege pamoja na Irungu. Tatizo la fidia za Songwe na Irungu ni tatizo la muda mrefu sana na sijui kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi kumaliza tatizo hili, hakuna siku ambayo inakaa na wananchi na kuwaeleza kwamba jamani tumefikia hapa. Mwaka jana alikuja Waziri wa Miundombinu na wakati huo akiwa Mheshimiwa Waziri Kawambwa, akasema atajaribu kutuma Tume ya kuangalia suala hili, lakini mpaka leo hakuna chochote kilichofanyika. Naomba malalamiko na kilio cha wananchi wa Irungu na Songwe, Serikali ikiangalie na ikitatue. Ni kiasi cha kukaa tu na wananchi na kumaliza tatizo hili ambalo ni kero kubwa sana. Hata leo hii kuna Mheshimiwa Diwani na Wananchi wengine ambao wametumwa na wananchi kutoka Irungu wanakuja kwa ajili ya suala hili la fidia zao na nakwenda kumwona Waziri baadaye. Naomba Serikali ilishughulikie suala hili, ndiyo maana nataka iwepo kwenye *Hansard* ili lisipotee lakini lishughulikiwe ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa kutunza wakati, anafuata sasa Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Mlaki ajiandae na Mheshimiwa Highness Kiwia atafutia.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuweza kunipatia muda ili nami niweze kuchangia kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, napenda kuwashukuru wananchi kwa imani yao kubwa kwa Chama chetu CHADEMA. Napenda pia kuwashukuru kwa ujumla wake wananchi wa Tarime.

Vilevile napenda kutoa taarifa ambayo siku ya Alhamisi umma ilipotoshwa, ambapo Waziri, Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Spika walisema hapa kwamba nimeshtakiwa na nina kesi Mahakamani. Napenda kusema kwamba sina kesi Mahakamani na sijashtakiwa popote pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, napenda pia kuipongeza Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa ushauri mzuri walioutoa na kuboresha Bajeti ya mwaka 2011/2012. Vilevile naipongeza bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani na nashauri Serikali iweze kuyafanya kazi yale yote mazuri yaliyoainishwa, kwa sababu yote yametolewa kwa mustakabali wa Taifa letu, ili mwisho wa siku Tanzania ya leo iweze kuwa Tanzania yenye neema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, kama muda utaruhusu, napenda kuchangia sehemu kama nne. Kwa kuanzia, naomba kuzungumzia kuhusu uwekezaji. Ni dhahiri kwamba, wote tunapenda uwekezaji, uwe wa ndani au wa nje, lakini pia tuangalie Taifa tunapata faida gani kutokana na uwekezaji, Mwekezaji husika naye ni lazima atataraja kupata faida na wananchi au wazawa amba wanakuwa katika sehemu zenye miradi hiyo na wenyewe wanapata faida gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kwenye sekta ya madini, kuna mikataba naweza nikasema mibovu ambayo inabidi iwe *revised*. Nashauri tunapokuwa tumeamua kuwekeza basi Serikali ichukue hatua ya kujumuisha Wadau watatu kwa maana ya Mwekezaji, Serikali na Wananchi ili waweze kushiriki katika kuandaa mikataba na kwa kufanya hivyo nina imani ita-*harmonise* ile sehemu na tutaepusha migogoro ambayo tunaiona hivi sasa katika sehemu mbalimbali za miradi. Katika hilo, napenda ku-*cite* mfano wa Nyamongo. Tumeshuhudia Mwekezaji wa *Barrick African Gold*, ameingia mkataba lakini kuna baadhi ya vitu hatekelezi. Kuna asilimia moja walikubaliana ya malipo ya pato la mgodi lakini hadi leo wananchi husika hawajawahi kuipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mikataba, pia napenda kuishauri Serikali wanapokuwa wanampeleka Mwekezaji, wajitahidi kuhakikisha wanatenga sehemu ndogondogo kwa ajili ya wachimbaji wadogowadogo kwa sababu kabla ya kuwekeza, kuna Watanzania amba walikuwa wanaendelea kujishughulisha na uzalishaji katika sehemu husika. Kwa hiyo, wanapokuwa wamemkaribisha Mwekezaji, wajitahidi kutenga sehemu ya wachimbaji wadogowadogo na hiyo itasaidia sana katika kuhakikisha kwamba tunaepuka migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wawekezaji wanapokuja, wahakikishe mahitaji muhimu ya kijamii kama vile miundombinu ya barabara, hospitali na shule zinaendelezwa katika sehemu husika. Ukiwa unatoka Tarime kwenda Nyamongo, utafika

unaumwa kwa jinsi barabara ilivyo mbovu, wala huwezi kujuu kama hiyo sehemu kuna madini yanachimbwa. Kwa hiyo, napenda sana Wawekezaji wanapokuja basi waboreshe sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuchangia suala zima la kodi, kuna ushauri mwangi umetolewa, hata Kambi ya Upinzani imependekeza kwamba *Pay As You Earn* kwa maana ya kwamba kodi inayokatwa kwa wafanyakazi ipo juu sana. Ni dhahiri kwenye *Pay As You Earn* tukipunguza kutoka ya sasa kwa *higher income earner* ambayo ni asimilia thelathini ikaweza kushushwa walau kwa kuanzia kwa sababu Kambi ya Upinzani ilikokotoa ikaona kwamba inawezekana kushushwa mpaka asilimia 27 ambayo ni *accommodatable* na kwa *low income earner* wakiweza kushusha mpaka asilimia tisa kwa kuanzia kwa mwaka huu wa fedha itasaidia sana. Kwa hiyo, nashauri Serikali ichukue ushauri huo kwa kuweza kuwasaidia wafanyakazi wenzetu waweze kuwa na tija ya kufanya kazi, badala ya kufanya kazi huku wakiwaza kwamba baadaye inabidi watoke wakafanye kazi nyingine ili kuweza *ku-supplement income* ya hela nyingi inayoenda *TRA*, ili mwisho wa siku *net income* yaani *take home* iwe kubwa kuliko kwenda kwenye mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuweza kufidia hilo punguzo la asilimia tatu kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 27 na asilimia tano kwa *low income earner* kutoka asilimia 14 mpaka tisa, Serikali inaweza ikajikita zaidi kuhakikisha kwamba inaziba zile *loophole* zote. Kuna wafanyabiashara wengi sana hawalipi kodi, iweze kuingiza utaratibu ambao utachangia zaidi kuleta mapato au kuwajibika zaidi kuhakikisha kwamba inakusanya kodi kutoka kwenye vyanzo vingine ili kuweza *ku-compensate* hilo punguzo kwa mwaka huu. Pia nashauri kwamba kwa mwaka ujao wa fedha waweze kupunguza zaidi hata kufikia asilimia 25 au 24 na asilimia nane au saba kwa wale wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipengele hiki cha kodi pia tumeshuhudia katika Kitabu cha Hotuba ya Waziri na vilevile katika *Financial Bills*, amesema kwamba *Traffic Notification Fees* itatoka shilingi 20,000 hadi shilingi 300,000, hiyo ni zaidi ya asilimia elfu moja mia mbili na kitu lakini katika kutamka alisema kwamba itatoka shilingi 20,000 mpaka shilingi 50,000 *yet*, hiyo pia ni asilimia mia moja hamsini. Hebu tuangalie tunapokuwa tunatoa mapendekezo, tujaribu kucaa uhalisia wa mwananchi wa kawaida na tusiweke kulingana na sisi kwamba tunapata mishahara mikubwa, tukafikiria kwamba tukiweka elfu hamsini ni sawa au tukiweka laki tatu ni sawa. Kwa sababu hata ilipokuwa elfu ishirini tu bado ilikuwa ni shida mtu kuitoa na tukawa tunazidi *ku-create* mwanya kwa *ma-traffic* kula hela. Elfu ishirini yenyewe ilikuwa shida, ukimkamata mtu, ukimwambia nakuandikia *notification*, atakuambia naomba nikupe elfu mbili au elfu tano ili aachiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lengo ni kutengeneza ajira, leo hii mtu *ame-committee offence* ya barabarani, umchaji elfu hamsini au laki tatu, hebu tufikirie kwamba huyo kijana labda ameajiriwa, ni Dereva Taksi, anatakiwa kupeleka mwisho wa wiki elfu sitini, leo umchaji laki tatu, *definitely* mwajiri wake atam-*fire*. Kwa kufanya hivyo, sidhani kama tutakuwa tunaongeza ajira au tunapunguza ajira katika harakati yetu nzima ya kutaka kukuza uchumi kwenye nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, napenda pia kuzungumzia hoja yangu ya tatu ambayo inahusiana na matumizi ya Serikali. Ni dhahiri kwamba limezungumzwa na baadhi ya Wabunge hapa lakini pia napenda kukazia kwa kusema kwamba imefika wakati sasa Serikali iamue kupunguza matumizi kwa ujumla wake, ili hiyo hela ambayo inakuwa *saved* hapo iweze kuwa *allocated* kwenye mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuainisha sehemu ambazo pamoja na yale yote ambayo yameongelewa, Serikali inaweza ikajikita kuhakikisha kwamba inapunguza matumizi yasiyo ya lazima. Napenda pia niwaombe Wabunge wenzangu, hebu tujaribu kufuta ile nauli tunayopewa ya kuja kwenye vikao hapa. Katika kuonesha mfano mzuri kuelekea kwenye kupunguza matumizi ya Serikali, tuiondoe. Tusiwe tunalipwa *Transport Allowance* ya ndani na naomba mniunge mkono kwa hili. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Serikali iainishe muda maalum wa magari ya Serikali kutumika. Tumeshuhudia kuna magari ya Serikali yanatumika hata baada ya muda wa kazi. Kuwepo na *system* ya magari ya Serikali, kufanya *retirement* ya mafuta, kumwekea mafuta Afisa husika basi aje aelezee kwamba nimewekewa mafuta kiasi fulani, nimekwenda sehemu fulani mpaka sehemu fulani matumizi yake ni haya. Vilevile tumeshuhudia kuna uharibifu mkubwa sana wa magari ya Serikali kwa sababu kama nilivyosema yanatumika asilimia kubwa kwa *trip* binafsi ambayo inapelekeea magari hayo kutengenezwa kwa gharama kubwa sana na hiyo inaleta mzigو mkubwa katika kuendesha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri kupunguzwe Semina Elekezi na malipo ya juu sana ambayo tumeyaona ambayo hayana tija katika Taifa. Nafikiri kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunapunguza pia matumizi na hivyo kuongeza *surplus* kwa *balance* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri tuangalie huu ukarabati wa Ofisi za Serikali ambao unafanywa kila mwaka. Hivi ni kweli haya majengo kila mwaka yanakuwa yanaharibika kihivyo maana hata majumbani kwetu hatukarabati nyumba kila mwaka. Kwa hiyo, inabidi kitu hicho kichunguzwe, *in this way*, *tuta-cut down* matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika harakati ya *ku-cut down* matumizi ya Serikali, nashauri pia Serikali iachane kabisa na manunuzi ya *furniture* kutoka nchi za nje. Tuna wajuzi wengi ndani ya nchi ambao wanatengeneza samani nzuri sana na ambazo zinadumu na zinauzwa kwa bei rahisi sana lakini *uki-import* kutoka nje, itakugharimu hela nyingi. Kwa hiyo, naomba pia na huo ushauri Serikali iuchukue na iufanyie kazi ili tuweze *ku-cut down* matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napenda pia kuzungumzia kuhusu vifaa vya ujenzi. Ni dhahiri kwamba vifaa vya ujenzi viko juu sana na kama kweli lengo letu ni kuhakikisha kila Mtanzania anaishi maisha bora kwa maana ya kuishi kwenye nyumba bora na kuondokana na kuishi kwenye matembe, tumeshuhudia miaka 50 ya uhuru bado

asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania wanaishi kwenye tembe au wanaishi kwenye nyumba ambazo siyo imara. Napendekeza basi Serikali kama kweli itachukua ushauri wa Wabunge tofauti na wangu pia kuweza kupunguza matumizi ya Serikali, itakuwa na *some savings*, izielekeze kwa kutoa ruzuku kwenye vifaa vya ujenzi ili viweze kushuka bei kama ilivyofanya kwenye ruzuku ya kilimo kama mbolea na vitu vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuwepo na *cross sectoral subsidies*, hii itasaidia maana unakuta kuna sekta nyingine itakuwa inazalisha zaidi ina-*compensate* na sekta nyingine, mwisho wa siku ukiangalia mapato kutoka kwenye hizo sekta *then* *yata-compensate* katika kuhakikisha kwamba tunatoa ruzuku katika vifaa vya ujenzi. Kwa kufanya hivyo, tutawasaidia wananchi wengi waweze kuwa na nyumba bora. Mtu akiwa na nyumba bora *definitely* hata *mind* yake itakuwa *set* kuweza kujikwamua zaidi kiuchumi, akishakuwa na nyumba bora atapenda awe na kitanda kizuri, godoro zuri, atapenda kujishughulisha na *kuji-engage* moja kwa moja kwenye shughuli zote za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia kuhusu maji. Maji tangia nazaliwa hadi sasa hivi nina wajukuu, ni tatizo katika nchi yetu. Wananchi huko vijijini wanahangaika sana wanatembea zaidi ya kilomita mbili kutafuta maji. Maji yenye we unakuta pengine ni maji ambayo siyo safi wala salama. Kwa hiyo, napenda kabisa Serikali ijikite kuhakikisha inasaidia kupata maji yaliyo safi na salama si mijini bali pia watoe *priority* vijijini ili akina mama wasiweze kupoteza muda mwingi kutafuta maji na badala yake waweze kutumia muda mwingi kuzalisha, kwani tunajua kwamba wazalishaji wakubwa ni akina mama hivyo tuwasaidie muda wao usipotee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napenda sasa nitoe ushauri maana nilidhani muda utaniishia. Tukumbuke kwamba Waheshimiwa Wabunge tumetumwa na wananchi kuja Bungeni kufanya kazi ya kuwawakilisha kama kutunga sheria, kuisimamia Serikali na kuitisha Bajeti kama hivi tunavyofanya. Kwa hiyo, ikitokea Mbunge ametoa wazo zuri tusilibaze. (*Makofi*)

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa Bungeni tena ili kuweza kuchangia bajeti hii ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa ujumla wake na hasa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, kwa bajeti nzuri sana ambayo inazingatia wananchi wa kima cha chini na maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja na hapa natoa ushauri tu kwa sababu bajeti ni nzuri. Natoa ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea maeneo matatu kwa haraka sana, nitaongelea kilimo, viwanda na madini. Kabla sijaongelea hayo mambo matatu, napenda nimnukuu Mheshimiwa Rais katika hotuba yake akiwasilisha Mpango wa Miaka Mitano alisema kama ifuatavyo nanukuu:-

“Utekelezaji wa Mpango huu ili kufikia malengo ya nchi yetu kuwa na kipato cha kati ifikapo mwaka 2025 itafikiwa tu kama juhudzi za Watanzania wote zitakuwepo, akawaomba Watanzania kila mmoja wetu kwa umoja wetu tusaidieni kufanikisha Mpango huu”. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kushirikiana na Serikali lazima sisi Watanzania pamoja na Serikali yetu *mindset* yetu ibadilike. Nchi za wenzetu kama *Vietnam* amba walitoka katika mfumo uliofanana na wa kwetu au tulioko sasa mfumo wa ujamaa (*socialism*) na *communism*, walipobadilisha mfumo au walipobadilisha uongozi wa nchi kufanya *public and private sector lead economy*, walibadilisha kwanza *mindset*, walitumia kila walicheweza kuhakikisha kwamba wananchi wanabadilika, wanafanya kazi kwa bidii, wananchi wanaacha mambo ya kuwa Mangimeza, wananchi wanajitahidi na Serikali kuondoa urasimu. Kwa hiyo, Watanzania wote pamoja na Serikali yetu inabidi tubadilishe *mindset* yetu ili tuanze kufanikisha mpango mzuri ulioletwa hapa mbele yetu pamoja na bajeti yetu hii ambayo tunaisubiri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niongelee moja kwa moja bajeti, imeelezea vizuri sana kuhusu kilimo, jinsi ambavyo kitaboreshwa hasa umwagiliaji, pembejeo, mikopo na kadhalika. Hii itamsaidia mwananchi wa kipato cha chini na kuongeza chakula nchini. Naomba kutoa ushauri, mkazo mkubwa vilevile uwekwe katika *commercial farming* kwa sababu tumekuwa kama tunaweka kwenye *substance farming* kwa ajili ya kilimo tu, Serikali lazima izingatie *commercial farming*. Nachojaribu kuonesha ni kwamba tujenge (*good economic base*), msingi imara wa uchumi, hapa ndipo maendeleo yote tunayoongelea katika bajeti hii yatawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi yetu ya kilimo tunaitumia kwa asilimia 24 tu, asilimia yote iliyobaki ambayo ni nzuri bado iko tupu na mapori. Serikali iamue tunasema mpango mkakati (*deliberate effort*) za kusaidia zichukuliwe ili tuweze kutumia kilimo chetu kuongeza pato letu la nchi. Pato la Mtanzania ambalo linatoka katika kilimo ni asilimia 23.8 tu ambapo tungetegemea kilimo kuwa kama uti wa mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipoongelea miaka 20 iliyopita kwamba haitafanya biashara, tukatoa mashamba tukabinafsisha, naweza nikatumia neno la Kizungu kwamba tuli- *abdicate*, tuliachilia *private sector* ifanye, lakini sidhani kwamba mpango ulikuwa unatakiwa hivyo, wala *World Bank* hawakusema namna hiyo. Tunapaswa tumsaidie huyu mkulima, kumshika mkono kwa kupima mashamba makubwa, hata kwa kuanzia zile *state funds* tuwe na 10 tu, halafu baada ya hapo tufanye utafiti wa kina wa kutazama udongo wetu utafaa kwa zao gani, hiyo ni Serikali inafanya. Tuna watu wengi kama pale *SUA*, kuna Profesa Semu, ni mtaalam wa udongo, tumieni hizi *brain ziweze* kutusaidia. Tukishaamua namna hiyo, kwa mfano, pale Kibaha walifanya utafiti ikaonekana mihogo inaweza ikaota sana na kuna soko kubwa sana la mihogo (*cassava starch*) huko *Europe* ambapo nchi yetu ingeweza kupeleka mihogo tu au hiyo *starch* nje na tukawa na kiwanda kizuri tukaweza kupata fedha nyingi kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, tuweke miundombinu, nikimaanisha Serikali, nitawaeleza fedha mtapata wapi. Uwekwe umeme, uwekwe umwagiliaji, zile *scheme* kama mlivyoziongelea katika haya mashamba makubwa. Kuna tatizo limesemwa sana hapa kwamba kuna ugumu wa kupata hati miliki, wanateseka, hii ni *constraint* ya nchi katika kilimo. Tuiseme namna hiyo kwa sababu katika Sheria ya Vijiji, Na.5 ambayo mmetupatia humu Bungeni, tunashukuru sana, inaonesha kwamba ile ardhi ya kijiji tunaweza tukaihuisha ikawa ardhi chini ya Kamishina ambayo ni chini ya Rais na hapo tukapima haya mashamba kwa wingi sana. Mashamba haya yakabitihewe wawekezaji wa ndani na wa nje yakisimamiwa na Serikali. Serikali itoe utaalam, *finance, loans* ambazo ni *government guarantee* mazao yatakayopatikana hapo yaongezewe thamani. Serikali ina uwezo wa kumwalika *Multinational Company* kama Hains, wanatengeneza *buckbeans, tomatoes*, matunda, tukimleta mmoja, tumweke pale katikati ya Chalinze na Morogoro, karibu na Ngerengere, mboga zote, maharagwe yote ambayo yanalinwa katika maeneo mbalimbali nchini tutaweza kuongeza thamani na tutaweza kuyasindika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwalike *De Lu Monte*, ikija hapa nchini tutashukuru. Yuko hapo Kenya tu, tukataka kumleta hapa tukaambiwa hakuna maeneo, maeneo ni ya watu, matunda yanaiza kule Muheza. Tunaomba sana tuweze kumleta *De Lu Monte* hapa, yuko tayari, tisinunue *juice* za *De Lu Monte* kutoka Kenya tuwe nazo na sisi hapa tuuze katika soko kubwa ambalo litakuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende harakaharaka kwenye viwanda, viwanda ni muhimu sana, nchi za wenzetu wakati walipokuwa wanaanza mambo ya viwanda walifanya *industrial revolution* na sisi tufanye mpango, twende tuwasaidie wananchi katika viwanda. Viwanda vinachangia asilimia 10 tu ya *GDP* ya nchi yetu, tuwasaidie watu, tumshike mkono huyu Mtanzania, tumuoneshe uchumi, tumuoneshe utaalam, tumpatie eneo, tumsaidie apate fedha na tumsaidie masoko ya kuuza. Masoko yako mengi sana, utafiti umefanyika na tunaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zingine *government* inachukua mtaalam ambaye anakuongoza, inatembeزوا *package* kuanzia pale unapoanza kiwanda kitakuwa aina hii, kina utalaam huu na tutatengeneza mazao kadhaa. Tutaiza wapi, masoko yapo, tuna fursa mbalimbali ambazo zinatusubiri na tunaweza tukazitumia kuweza kuuza vitu vyetu. Nasema bila kuwa na viwanda na kilimo kwa ajili ya kusindika mazao yetu, uchumi wa nchi yetu hautaweza kukua kama tunavyofanya. Wenzetu wa Malaysia waliweza kuanzisha *Malaysia Industrial Development Authority (MIDA)* kumshika mkono mwananchi mpaka mwisho aweze kufanikisha. Naomba sana, kuna Wizara ya Uwekezaji iwe *coordinator* katika Wizara ya Kilimo na Viwanda na isimamie suala hili na hii ndio inaweza kusimamia kutengeneza *package, bankable project* za kusaidia wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe tahadhari, kama hatutachukua hatua za dharura kukuza kilimo na viwanda, tutakuwa soko la wenzetu. *Regional integration* zetu za *East African Community, SADC* na sasa hivi tumemuona Mheshimiwa Rais amesaini *tripartite, three trade area* ambalo hili ni soko la watu 700 jamani tutauziwa vitu kutoka

Cape Town mpaka Cairo biashara iwe huru hapo tutauza nini, tulivyo sasa hivi kwa *SADC* tunauza asilimia tano tu. Afrika Kusini inatuuzia asilimia 58 kwa *Community East African*, tunauza asilimia 24, Kenya inatupa asilimia 44 bila sisi kuwa na cha kuuza tutashindwa. Naomba Serikali ilitazame hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la madini. Sisi ni *largest producer*, we are *number three* katika Afrika, tutumie hii dhahabu. Kwa kifupi tuombe sana Serikali isaidie *STAMICO* wanunue *shares* katika hii migodi ili tuweze na sisi kutumia na kufaidika katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijapigiwa kengele ya pili, naomba niongelee kuhusu *NGO*. Naomba Serikali ifikirie tena kuondoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kuna *NGO* nzuri ambazo zinafanya kazi ya Malaria, UKIMWI, kama *MEDA* tunaomba ifikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nimalizie kuzungumzia kuhusu msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Jamani Dar es Salaam ndio Jiji, biashara kubwa ziko pale, tuna viwanda vingi sana pale, kama hatutafikiria kwa umakini kabisa na kuhakikisha kwamba tunajitahidi kuondoa ule msongamano, tunapoteza masaa mengi sana barabarani, tunaomba Serikali isaidie. Kwenye Mipango tumeiona mpango wa *DART*, magari yatakayokwenda kwa haraka, tumeona wanataka kuanzisha reli, tunaomba Serikali itoe fedha ili tuweze kuhakikisha kwamba Dar es Salaam usafiri unakuwa wa kueleweka. Tumeamua tunajenga *fly over* pale Dar es Salaam, tukataja na maeneo, lakini hapa kwenye bajeti sioni mahali ambapo inaonesha kwamba tutajenga hizi *fly over* lini na fedha iko wapi, tunaomba uwe mkakati maalum. Nchi za wenzetu, Jiji kubwa kama Dar es Salaam linakuwa na Wizara yake peke yake kama Kenya ili kuondoa kabisa haya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niweke mambo sawasawa kuhusiana na ukusanyaji wa kodi pale Dar es Salaam. *TRA* inajitahidi sana. Sasa hivi *TRA* ikishirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni wameweke mkakati wa kupita nyumba hadi nyumba, *plot* hadi *plot* kuhakikisha kwamba tunakusanya *land rent* na mapato haya yatatumika kuboresha miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam. Naomba kabisa nichukue nafasi hii kuwapongeza sana *TRA* pamoja na Manispaa za Dar es Salaam ambazo tunafanya kazi hiyo kwa nguvu sana siyo kama ilivyoleweshwa hapa kwamba tumelala na vitega uchumi hawavijui. Tuna *Regional Manager* mzuri sana anaitwa Mr. Mita, anafanya kazi kwa nguvu sana. Jimbo la Kawe lina mali nyingi, lina majumba makubwa ya kifahari na sasa hivi orodha ipo na mkitaka tuilete kabla Bunge halijaisha tutaleta, ya nyumba ambazo zimekwishatambuliwa ili ziweze kulipa hiyo *rent*. Naomba niliweke sawa suala hilo. Pia Manispaa ya Kinondoni iko tayari kuonesha wametazama wapi kwa mkakati mpya wa kukusanya mapato ili kuweza kupata mapato kwa ajili ya mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Ilemela kwa kazi kubwa waliyoifanya pamoja na mabomu mengi yaliyopigwa lakini hatimaye nikatangazwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilemela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze wananchi wa Jiji la Mwanza kwa kazi kubwa waliyoifanya ambayo kimsingi kabisa siyo tu kutupa Meya lakini pamoja na Naibu Meya katika Jiji la Mwanza kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie fursa hii kuipongeza Bajeti Kivuli iliyowasilishwa na Kambi ya Upinzani, bajeti ambayo ina mwelekeo, yenye kuleta matumaini, yenye kuonesha uwezo wa kupiga hatua ya maendeleo katika Taifa letu. Bajeti ambayo kimsingi kabisa inapaswa kusomwa na *positive mind* ili iweze kuleta *positive results*, lakini inaposomwa na *negative mind* si tu kwamba anayesoma ataona giza *but the person who reads it will end up in the pit of darkness*. Kwa Kiswahili nitasema kwamba inaposomwa na mawazo au mtazamo mbaya, msomaji si tu kwamba ataona kiza bali ataangukia katika shimo la giza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimekuwepo hoja nyingi sana ambazo zimejadiliwa, mimi ni mchangiaji wa mwishomwiso, mambo mengi yamejadiliwa, Kambi ya Upinzani imewasilisha mengi na imeyazungumzia vizuri sana. Kwa hiyo, nitajikita kwenye mambo machache, ambayo naamini ndiyo wananchi wangu wa Jimbo la Ilemela wangependa niyajadili katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na hoja inayoonesha jinsi gani Watanzania wengi hawaridhiki na hali ya uchumi wa Taifa letu ilivyo kwa sasa na hoja hii imekuwa ikilinganishwa na umri wa Taifa letu kama nchi tangu uhuru na hali ya uchumi ilivyo sasa. Kimsingi hatuna maana kwamba hakuna kitu kilichofanyika, lakini kinachozungumziwa hapa ni kwamba mafanikio yaliyopo hayaendani na rasilimali ambazo Taifa letu limejaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujaribu kuangalia, miaka kumi baada ya uhuru hali ambayo Taifa letu ilikuwa nayo. Miaka kumi baada ya uhuru, elimu ilikuwa bure, afya ilikuwa bure lakini leo hii angalia haya maeneo na wengine hapa wamepitia mfumo huohuo wa kusomeshwa bure. Sasa unapoangalia uwiano huo, lazima utapata mkanganyiko katika fahamu zako, utashindwa kujua unatoka wapi, unakwenda wapi. Kwa hiyo, si kwamba hakuna kilichofanyika lakini kilichofanyika hakiendani na utajiri ambao Taifa letu unamiliki. Tatizo ambalo inalikabili Taifa letu leo ndiyo yaleyale yaliyopelekea Baba wa Taifa kuona umuhimu wa kuondoa Ukoloni maana alisema hatuondoi Ukoloni kwa sababu ya rangi zao au tunapenda kutawala, tunaondoa Ukoloni kwa sababu umeshindwa katuondolea ujinga, maradhi na umasikini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango mingi sana ambayo imeainishwa, ukiangalia kwenye ukurasa wa 14 kwenye Kitabu cha Bajeti ambapo kimsingi imekuwepo mipango ya namna hii ya muda mrefu, mfupi, nitanukuu ukurasa wa 14. Utaona hapa kuna suala la mfumo wa bajeti 2010/2011 ulizungumzia Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, MKUKUTA II, Malengo ya Maendeleo ya *Millennium*, ukijumlisha na Ilani ya mwa 2005 mnaifahamu, Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) na Mkakati wa Taifa wa Madeni. Mipango ya namna hii haijaanza leo na ni dhahiri kwamba mipango ya namna hii mara zote haifikiwi malengo na haizai matunda yanayotarajiwa, ndiyo tatizo kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa wakati wa Azimio la Arusha alisema ili Taifa hili liweze kuendelea, linahitaji ardhi, watu, siasa safi na viongozi bora. Tamko hili wengi wanalibeza kwa sababu hawaoni hapo ikitamkwa fedha. Inatamkwa ardhi, watu, siasa safi na viongozi bora sio suala la pesa. Pesa ni matokeo ya matumizi mazuri ya rasilimali za Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi kabisa, kama ilivyokuwa wakati wa Ukoloni, Ukoloni ndiyo ulionekana kikwazo cha maendeleo ya Taifa hili. Naomba niseme kwamba Ukoloni kwa sasa umekuja kwa sura mpya, sura ya ufisadi ambao ndiyo kikwazo cha maendeleo ya Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa, katika kikao cha bajeti cha 35, Mei 17, 1960, alisema nitanukuu:-

“Ufisadi na rushwa ni adui mkuu zaidi kwa maslahi ya wananchi wakati wa amani kuliko vita”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na jitihada zote kama Taifa tunazopiga ili kuleta maendeleo katika Taifa hili, hakuna namna tunaweza tukafanikiwa kulitoa Taifa hili mahali hapa tulipo kama kwanza hatutaunganisha nguvu zetu za pamoja kupiga vita ufisadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nitakwenda moja kwa moja kwenye vipaumbele. Bajeti Kivuli ya Kambi ya Upinzani imezungumza mengi na imeyazungumza vizuri sana na nitaanzia na umeme. Wananchi wangu wamenitura nimwambie ndugu yangu, rafiki yangu, kaka yangu Ngeleja kwamba haya masuala ya *megawatts* wamechoka kuyasikia, wanachotaka ni umeme, *megawatts* tubaki nazo hukuhuku Bungeni, sitini, sabini kwa mia moja hawahitaji kusikia, wanachotaka kuona ni umeme. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa suala la maji, tatizo la maji katika nchi yetu linatofautiana kijiografia. Unajua unapozungumza kisima cha maji uka-refer na Mkoa wa Mwanza hususani Jimbo la Ilemela, wananchi hawakuelewi maana tayari wana kisima walichopewa na Mungu, Ziwa Victoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu wana-Ilemela na wananchi wa Jimbo la Ilemela sio visima ni pampu zenyne uwezo wa kuweza kuchota maji kutoka Ziwan, kusukuma katika maeneo yao na tayari maji yapo. Haiingii akilini mwao kuona maji yanayozungumziwa leo hii yanakwenda Tabora, Kahama na maeneo mengine na kuna watu wengine hususani maeneo ya vijiji ambao ni mita hamsini kutoka wanapoishi mpaka Ziwan, lakini hawapati maji hayo mpaka wakachote na ndoo. Kwa hiyo, kwa wao unapozungumzia suala la maji la visima, wanaposikia maji yanakwenda huku na kule wanaona kama ni sinema ya Kinigeria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa labda ubadilishe *mic* yako.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Naomba uhame *microphone* hiyo, hamia nyingine uokoe muda wetu.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nifidiwe muda wangu. Kwa hiyo, kimsingi mimi naishauri Serikali inapojadili suala la maji hususani kwa Jimbo la Ilemela ielekeze katika kuleta pampu zenyne uwezo wa kusukuma maji kutoka Ziwan kuelekea kwenye makazi ili wananchi wote waweze kunufaikia na Ziwa lile, Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitahamia kwa harakaharaka kwenye upande wa afya. Kimsingi Jimboni kwangu Ilemela, tatizo la huduma za afya sio tatizo tu bali ni janga. Hatuna Hospitali ya Wilaya, Vituo vya Afya havina madawa, hakuna hata gari ya kubeba wagonjwa na vituo vingine sasa hivi vimebadilika kuwa nyumba za popo na madawa hakuna. Sasa kuna haja gani ya kupeleka Vituo vya Afya bila kuwa na dawa? Maana umuhimu wa Vituo hivyo ni pale huduma zitakapopatikana. Kwa hiyo, naishauri Serikali pamoja na mipango yake yote iangalie haja ya kuwepo na Hospitali ya Wilaya, lakini pia iondoe tatizo la dawa katika Vituo vyangu vya Afya. Pamoja na hivyo, tuna Hospitali pale ya Jeshi ya Mkoa ambayo kimsingi iko pale kwa lengo la kuhudumia Wanajeshi, lakini sasa kwa asilimia 90 inahudumia wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, naomba Hospitali ile iwezeshwe kwa wakati huu ambapo bado mchakato unaendelea wa kupatikana Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo ambalo linanitatiza na katika hili naomba niseme kwamba sitaunga mkono bajeti hii. Pamoja na kwamba inaonekana bajeti hii ya afya imeongezeka kwa asilimia 0.3, lakini kwa upande wa dawa imepunguziwa zaidi ya shilingi bilioni tisa, kwa eneo ambalo ni muhimu na kufanya hivyo ni sawasawa na kuongeza idadi ya vifo vya akina mama na watoto. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati tunajadili bajeti hii, naomba Serikali iliangalie hili kwa kina na kwa mapana sana. Kwa sababu gani? Tunajua ilivyokuwa hapo awali katika bajeti iliyopita, pamoja na hali ile ilivyokuwa wote tunajua hapa, hali ya Vituo vyetu vya Afya na Hospitali zetu kuhusu suala la madawa, iweje wapunguze

kwenye dawa? Hakuna sehemu zingine za kupunguza mpaka tupunguze kwenye dawa? Mimi kwa kweli kwa hili hapa siungi mkono hoja na naomba nipate ufanuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la deni la *MSD*, Bohari Kuu ya Dawa ya Taifa. Deni hili linaongezeka siku hadi siku, bajeti iliyopita ilikuwa ni shilingi bilioni 36, sasa hivi ni shilingi bilioni 46, ongezeko la zaidi ya asilimia 100, sasa tunakwenda wapi? Tunaambiwa kwamba bajeti imeongezeka, lakini deni hili ndiyo linasababisha ukosefu wa dawa katika nchi hii. Naomba nipate ufanuzi, Serikali ina mpango gani juu ya kuondoa hili deni la *MSD* na deni hili kuongezeka kwake hakutokanani na ununuza wa dawa bali linatokana na kugomboa dawa bandarini, zilizokuja kwa msaada. Sasa hii haiingii akilini mwangu, dawa zinakuja kwa msaada bado tunashindwa kuzilipia, kwa kweli katika hili nalo pia siungi mkono hoja, naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwenye suala la ardhi kwa harakaharaka. Katika tunu lillobakia katika Taifa letu ambalo kimsingi kabisa tunaweza tukasema kwamba ndiyo eneo pekee Watanzania walio wengi, maskini ndiyo wana uwezo wa kulimiliki, lakini urasimu ulioko pale ni kikwazo cha Watanzania wengi kuweza kumiliki. Tumeshindwa kuwapa maeneo ya madini Watanzania, wazee wengi hawawezi kumiliki viwanda, sasa hata ardhi? Naomba Serikali na bajeti hii iangalie katika kuwawezesha Watanzania wengi waliokuwa maskini waweze kumiliki na kupata hati miliki za ardhi, maana ndiyo mtaji pekee waliobakia nao. Maana leo kupata ardhi ni kama vile kutafuta tiketi ya kwenda mbinguni, ina maana tunafungua milango ya uwekezaji kutoka nje lakini Watanzania wengi hawamiliki ardhi, mwisho wa siku ardhi hii itachukuliwa na wageni tunarudi kulekule kwenye Ukoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia iko migogoro ambayo kimsingi naweza kusema inasababishwa na Serikali. Unakuja mradi wa barabara kama ilivyo kule kwenye Jimbo langu, 2007 wameambiwa wasiendeleze makazi yako, watalipwa fidia uendelee ujenzi wa barabara, lakini huu ni mwaka 2011 hawajalipwa fidia na wakija kulipwa fidia watalipwa fidia kwa tathmini ya mwaka 2007, sasa huku ni kuendeleza makazi au kumrudisha Mtanzania aliye maskini nyuma? Miradi ya namna hii, naomba niseme kwamba Jimboni kwangu, wananchi wangu wamesema hivi kama Serikali haina pesa basi ni vyema iwaruhusu waendelee kuendeleza makazi yao na itakapokuwa tayari kuwalipa fidia, ndiyo iletu miradi hiyo. Kwa sababu kuwazuia wasiendeleze makazi yao na wakati wanajua watawalipa kwa fidia ya mwaka ule unaokuja, huko sio kuwaendeleza, ni kuwarudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitazungumzia suala ambalo limezungumziwa na wengi, suala hili la faini ya makosa barabarani. Mimi hivi viwango sijui vimetoka wapi, sikusomea masuala ya *accounts*, lakini nashindwa kujua ni tathmini zili zifanyika, ni vigezo vipi vilivyofanyika, ni utaalamu gani huo wa kutoka kwenye asilimia 10 kwenda kwenye asilimia 100, mimi kwangu hii haiingii akilini mwangu. Taarifa hii kwa wananchi wangu wanasema kwamba huo ni mzaa, hawaelewi na hawajawahi kusikia ongezeko la kiasi hicho. Naomba Waziri husika aliangalie jambo hili vizuri sana kwa sababu kilichotakiwa hapa sio suala la kuongeza ile faini, ni kuitengenezea ile faini

iliyopo mazingira mazuri ili kila kinachopatikana kifike kunakotakiwa. Nitarudia na kwa msisitizo, naomba niweke mkazo kwa kunukuu kauli ya Mbunge... (*Makofi*)

(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante sana, muda umekwisha, msemaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Deo Sanga.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, niwashukuru wapigakura wangu wa Njombe Kaskazini, nimshukuru pia Mama Sanga kwa kuendelea kunilea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake, nimshukuru kwa bajeti nzuri. Nianze na ukurasa wa 74 wa Hotuba ya Waziri.

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa, nilisema msemaji wa mwisho ni Mheshimiwa Deo Sanga kumbe muda bado unaruhusu kwa hiyo Mheshimiwa Zainab Kawawa pia ajiandae, ahsante.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukurasa wa 74 unazungumzia juu ya usalama barabarani na kuongeza faini kutoka shilingi elfu hamsini hadi shilingi laki tatu. Nadhani kwanza tuangalie tulipokuwa na faini ya shilingi elfu moja, elfu mbili, elfu tano, elfu kumi, je, iliweza kupunguza kasi ya ajali na baadaye tukaiweka faini ya shilingi elfu ishirini ambayo watu hawa walikuwa wanashindwa kuilipa kama walivyosema wenzangu, leo mtu huyu tunampa faini ya shilingi elfu hamsini mpaka shilingi laki tatu, tutakuwa tumetatua tatizo la usalama barabarani au tutakuwa tumeongeza matatizo? Hebu tuiangalie, tujifunze na nchi zingine za jirani kwa mfano Zambia hapa, faini yao ni ndogo sana kwa hela ya Tanzania haizidi shilingi elfu mbili, hii faini ya shilingi elfu hamsini na laki tatu tunawapa watu wetu matatizo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la Viwanja vya Ndege, katika bajeti imeonesha viwanja vichache ambavyo vimepewa bajeti ya kutengenezwa au kuvikarabati. Ukiangalia viwanja kwa mfano pale Iringa, kuna kiwanja kizuri sana ambacho kingepewa bajeti na kikatengenezwa, kingeweza kuleta watalii wengi kwenda *National Park* ya Ruaha kule, lakini kwa sababu hatuna Kiwanja cha Ndege na wakati fulani wanashindwa kuja ni mbali, maana kuja Iringa inawezekana wanatua Dar es Salaam kuja kule watakujaje? Nilidhani ni vizuri mngeliwekea bajeti suala hilo. Sasa tuna Mkoa mpya wa Njombe, ni vizuri pia nao tungeuwekea bajeti ili watalii hawa wanapokuja kwenda Kitulo waweze kutua na ndege pale Njombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la kilimo, bajeti ya kilimo ya mwaka jana na mwaka huu, karibu zina uwiano. Naipongeza Serikali kwa kutizama vipaumbele ikiwemo kilimo lakini naomba sana Serikali itupie macho sana Mikoa

inayolima sana zao hili la chakula cha mahindi, ukiwemo Mkoa wa Iringa. Naomba sana Serikali kipaumbele hiki cha kilimo iongeze bajeti hususani ya mbolea katika Mikoa hii inayozalisha sana chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la madini au la umeme. Liko tatizo kubwa, juzi Waheshimiwa Wenzangu waliochangia wamezungumzia kwa mfano utakuta mwananchi anapotaka kuingiza umeme katika nyumba yake, upo umbali labda ambao unahitaji nguzo moja, mbili, tatu, mpaka nne. Kwa mfano, Mbunge mmoja alizungumzia nguzo tatu, mwananchi aliambiwa gharama yake karibu shilingi milioni moja na laki sita, ni bei kubwa sana. Sisi kule Iringa ndio tunaozalisha nguzo, nilidhani Wizara ingeweza kuwaruhusu watu, kama mtu anaweza kuipata nguzo mahali popote madam iwe na viwango aruhusiwe kuliko kufanya ni lazima anunue *TANESCO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Iringa wako watu wanaozalisha nguzo na kuiuzia *TANESCO*, ukitaka kwenda kununua wanauza bei ndogo sana, lakini ikifika *TANESCO* inakuwa bei kubwa. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara au *TANESCO* ingewaruhusu watu wanunue ili mradi zikiwa na viwango ambavyo vinaweza vikawekwa katika eneo linalohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleze na suala la umeme. Kule Njombe hususani kwenye Jimbo langu, yapo maporomoko makubwa kabisa katika Kata ya Ikondo katika Kijiji cha Ikondo ambayo yanaweza kuzalisha umeme *megawatt* 120, mpaka 100. Wako wenzetu wa *SEFA* wameweza kukipa kijiji kizima cha Ikondo umeme. Nadhani sasa ni muda muafaka, ni vizuri Wizara hii ya Madini itafute wataalam, tuongozane na mimi mwenyewe nikawaonyeshe ili waweze kuona, pale tunaweza kupata *megawatt* nyingi ambazo zinaweza kuingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *VETA* kwa vijana wetu. Hili lilizungumziwa kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ambapo tutahakikisha kutakuwa na *VETA* kila Wilaya. Mimi nadhani sasa ni muda muafaka Serikali kuweka msukumo ili kuhakikisha tunajenga *VETA* nyingi katika Wilaya zetu na hususani Wilaya ya Njombe iko *VETA* ndogo pale Mtwango kwa Mkoa wa Njombe tunganezia pale. Lingekuwa ni jambo jema sana ambalo lingewasaidia wananchi wetu katika vituo hivyo vya *VETA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Vituo vya Afya. Wizara ya Afya, utakuta kwa mfano mgawanyo wa dawa kwa Vituo vya Afya kwa nchi nzima karibu unalingana. Nadhani ni Sera ya Wizara ya Afya, lakini Kituo cha Afya cha Makambako ni kituo chenye watu wengi, wakati ule kinajengwa kilikuwa takribani na wakazi wasiozidi 15,000 leo wako watu 65,500, bado huduma ya mgao wa dawa ni uleule. Naiomba Wizara ipandishe hadhi ya kituo hiki na kuwa Hospitali Teule ya Mji wetu wa Makambako ili iweze kuhudumia vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko bado katika Jimbo langu la Njombe Kaskazini. Nashukuru Serikali katika Kijiji cha Nyombo, Kata ya Ikuna, walipeleka umeme pale katika Kijiji hiki cha Nyombo lakini umeme ule wananchi hawawezi kuweka mashine za

kusaga wala kuchomea kwa sababu *transformer* ni ndogo. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara iweze kupeleka *transformer* yenye nguvu ya kutosha ili wananchi hawa wasiende kusaga mbali wakati umeme wanao pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuondoa kodi ya mafuta. Kodi hii itaweza kupunguza bei ya bidhaa ambazo sasa hivi bei zimekuwa juu sana kwa mfano, sukari na vitu vingine, naipongeza sana. Niseme suala la sukari ipungue zaidi kuliko ambavyo imewekwa sasa ya shilingi 1,700/. Naiomba Serikali, muda unapofika wa kutoa vibali kwa watu ambao wanatakiwa kuingiza sukari ni vizuri ikaangalia Ukanda kwa mfano wa Kusini ukawapa vibali zaidi ya 10, watu watachukua Malawi, watachukua Zambia, bei itapungua tu, maana kutakuwa na ushindani kuliko kuwapa watu wachache na ndiyo inayoleta tabu ya bei hii. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, inapotoa vibali itoe kwa watu wengi ili watu waweze kushindana namna ya kuingiza sukari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe wenzangu na Watanzania kwa ujumla, watu ambao wanasema Serikali miaka 50 hakuna kitu kilichofanyika, niseme jambo moja tu kuwambusha wenzangu. Suala la elimu kwa mfano, Iringa historia inatuambia tulikuwa na Sekondari moja iliyohudumia Mikoa minne, Mbeya, Rukwa, Ruvuma na ilikuwa ni Malangali peke yake. Leo Iringa ina sekondari 235, utasemaje Serikali haijafanya kitu, tena kwa Mkoaa mmoja tu na ndiyo uwiano wa sekondari hizi ambazo zimezalishwa kwa wingi, umeipa sasa Serikali ya CCM ikiongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mriasho Kikwete kuweza kujenga *UDOM*, sasa utasema hakijafanya kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuangalie mahali ambapo tulipotoka. Barabara, mimi nilikwenda Songea mwaka 1976. Tulitembea kwa gari siku sita kufika Songea leo unakwenda na kurudi, utasema Serikali haijafanya kitu jamani. Lazima tuipongize Serikali kwa kazi nzuri ambazo imeendelea kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu lakini ni muhimu. Niombesana ndugu zangu, haya yote tutafanikiwa kama tutajenga umoja na upendo na mshikamano. Humu ndani wamo Wachungaji, nilisema hata wakati ule, Mashekhe wamo humu, mtuombee tupendane ili tuweze kutekeleza haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la chakula. Niombesana Serikali hususani Mkoaa wa Iringa na mahali pengine, tuongeze vituo vya kununulia mazao haya ya mahindi muda unapofika. Kwa mfano, niliandika barua kwa Waziri, Jimbo la Njombe Kaskazini, tuongeze kituo pale Tarafa ya Lupembe, Kata ya Matembwe, maghala yalishajengwa siku nyingi, yapo pale ya kutosha ili wananchi hawa wasipate usumbufu wa kupeleka mazao yao unapofika muda wa kununua mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la tumbaku linalolimwa na Mkoaa mbalimbali nchini Tanzania. Uko ujanja, tusipoangalia wako watu, Taasisi fulani ambazo zinanunua tumbaku hii kwa kuwakata wananchi shilingi 200, 200 kwa kilo. Niombesana Serikali isimamie, tusipoangalia ni mamilioni mengi sana wananchi hawa

watakuwa wananyonywa kupitia watu hawa wanataka kujinufaisha kwa maslahi yao binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la hoteli ya kitalii, iko hoteli ya Embassy pale. Hoteli ile imetelekezwa kwa muda mrefu. Hivi jengo lile kwa nini lisifanyiwe shughuli nyingine za Serikali badala ya kutelekezwa kwa muda mrefu sana lingeingizia Serikali mapato ya kutosha kwa kufanya shughuli zingine kuliko jengo lile kukaa kwa muda mrefu bila shughuli maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kule Njombe pale Ruhuji mpango huu wa mwaka 2011/2012 kwa kuweza kupata umeme kupitia gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100, nashukuru sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha Kikao hiki, napenda kutoa matangazo yafuatayo:-

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, ameomba niwatangazie wafuatao wafike Makao Makuu ya Chama saa saba mchana bila kukosa kuna jambo muhimu. Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Mtemvu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Daniel Mkapa, Mheshimiwa Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Hamisi Kagasheki, Mheshimiwa Profesa Anna Tibajuka, Mheshimiwa Magufuli, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Brigedia Generali Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Rostam Aziz, Mheshimiwa Samuel Sitta, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Jeremiah Sumari.

Pia naomba niwatangazie ambao watachangia tutakaporudi saa 11. Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Zainab Kawawa, Mheshimiwa Mohamed Chomboh, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga na wengine tutawatangazia kadri tutakavyokuwa tunaendelea.

Baada ya matangazo haya, naomba kusitisha kikao chetu mpaka saa 11.00 jioni. Ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu.

(*Saa 6.50 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni, Bunge lilirudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Tutaanza na Mheshimiwa Zaynab Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Chomboh, baadaye Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ajiandae. Mheshimiwa Zaynab Kawawa!

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali. Kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza katika historia ya maisha yangu, kuchangia hoja hii kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kuchukua nafasi hii kukishukuru sana Chama cha Mapinduzi, nachukua nafasi hii kuwashukuru wanawake wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi Taifa, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Sophia Simba. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wanawake wote wa Mkoa wa Lindi, kwa heshima kubwa walijonipa; naahidi nitawatumikia ipasavyo. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia wafanyakazi wenzangu wote wa nchi nzima nikiwa kama mwakilishi wao na naahidi nitaendelea kuwatumikia ipasavyo, naomba wanipe ushirikiano wa kutosha. Mwisho, naishukuru sana familia yangu kwa kuwa karibu na mimi, kwa kuendelea kunipa moyo na nawaomba waendelee kuwa wavumilivu na wastahimilivu, wanavyoniona ninavyopambana katika masuala mbalimbali ya kisiasa. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuweza kuandaajabeti hii. Kama ingekuwa kutoa Kauli Mbiu, basi mimi ningesema kwa kweli hii ni bajeti ya mnyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wenzangu wote kuunga mkono mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya mwaka 2011/2012, yaani Bajeti ya Serikali. Katika bajeti hii leo, nakusudia kuchangia eneo la ajira kwa vijana. Nitazungumza pia kwa uchache tu upande wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ndio kigezo kimojawapo cha kukuza uchumi wa Mtanzania mmoja mmoja. Ili tuweze kufanikisha utekelezaji wa bajeti hii, hatuna budi kuona kwamba matokeo yake yanakuza uchumi wa mtu mmoja mmoja ilhali ule uchumi mkubwa ukiendelea kukua vizuri. Naipongeza sana Wizara ya Fedha, kwa kuweza kuainisha kipaumbele kama kilivyojionesha katika Ukurasa wa tano, aya ya nane, kipaumbele cha kupanua ajira kwa sekta binafsi na sekta ya umma. Vile vile naipongeza Serikali kwa kuweza kuainisha mikakati mbalimbali ambayo itapelekeea kuchochaea ama kupanua ajira. Mikakati hii inagusia maeneo ya kukuza viwanda, maeneo ya mradi wa kilimo kwanza, lakini vile vile inagusia maeneo ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hali halisi tuliyonayo sasa hivi, takwimu zisizo rasmi zinaonesha kwamba vijana wanaomaliza katika shule za Sekondari kwa mwaka, wanafikia 1,600,000. Kati ya vijana hao, vijana 1,000,000 ndio wanaoweza kwenda kwenye *Higher Learnings*, kwa hiyo, tunayo *back log* ya vijana takriban 600,000 ambao wapo wamemaliza shule za Sekondari. Katika maisha yetu tuliyoyazoea mtoto anayemaliza shule ya Sekondari, huyu hana *skills*, bado hajaweza kujitegemea yeze mwenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Serikali, ione namna kama ilivyoahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tuendelee kuongeza Vyuo

Vya VETA katika ngazi ya Wilaya, ili tuweze kuwasaidia hawa vijana. Kwa sababu, ili vijana hawa waweze kuwa na sifa za kutumia nguvu kazi zao katika hii mikakati iliyoinishwa ya viwanda, kilimo, mikopo, na kadhalika, vijana hawa wanahitaji *skills* katika maeneo mbalimbali na wanahitaji kuhamasishwa hasa katika kazi za kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo chetu sasa kwa namna ilivyozooleka, japokuwa tunasema ni uti wa mgongo, lakini bado hakioneshi kuwa ni kazi ya kibiashara. Sasa kama tunataka kazi ya kilimo ifanywe na vijana, ni lazima vijana hawa wawe *sensitized* na waione kazi hii kama ni kazi ya kibiashara. Vile vile vijana hawa wanahitaji kuwezesha kiuchumi, wapewe miradi midogo midogo ili waweze kufanya shughuli mbalimbali za kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa ni lazima wawe na *knowledge* ya *investments*. Ni lazima Serikali yetu ione umuhimu wa kuwafundisha, wapate *knowledge* ya kuweza kujua namna ya kuwekeza. Lakini vile vile vijana hawa wanapaswa kufundishwa elimu ya kujitegemea, ili waweze kujua kujitegemea, wanapofanya shughuli hizi za kibiashara waweze kujua kufanya *savings*, lakini pia waweze kujua kufanya maendeleo mbalimbali na hapo ndipo uchumi wa mtu mmoja mmoja unaweza kukua na kuonekana. Hatuna budi kulizingatia hili kwa sababu hata nchi zilizoendelea, kwa mfano, Marekani, Viongozi waliopewa madaraka leo wanapimwa kwa namna gani wameweza kupunguza tatizo la umaskini kwa kupanua ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini sasa Wizara yetu inatakiwa ifanye? Nashauri, ni vizuri sasa tukawa na takwimu halisi ya vijana wangapi wanaomaliza katika shule za sekondari, vijana wangapi wanaomaliza katika Vyuo Vikuu na taaluma zao kwa takwimu na kufahamu maeneo yao, ili tuweze tunaposema tunaanzisha miradi ya namna hii, tuweze kujua tunawa-*intergrate* vipi ama tuweze kujua tunawashirikishaje kwenye miradi hii. Kwa hiyo, basi ni lazima tuwe na program kwa ajili ya kuwapa *knowledge*, kwa ajili ya kuwafundisha, kwa ajili ya kuwashamasisha na kadhalika. Najaribu kuangalia hapa wenzetu nchi ya Uganda na Kenya, wamefanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2011/2012, wenzetu wa Uganda wao wanakusudia kutenga shilingi bilioni 44.5 kwa mwaka kwa ajili ya kuzalisha ajira. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 25 za Uganda, zimetengwa kwa ajili ya Mfuko Maalum wa Ujasiriamali. Lakini vile vile shilingi bilioni 3.5 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo ya ujasiriamali, Shilingi bilioni 1.0 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo ya stadi kazi, Shilingi bilioni 16.5 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya vijana na wajasiriamali wengine kufanya biashara na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kuielezea mikakati ambayo wenzetu wa nchi ya Kenya, nao wamefanya. Katika nchi ya Kenya, wao wanaeleza kwamba shilingi za Kenya milioni 210, zitaongezwa mwaka huu katika mradi wa uwezeshaji vijana ili mfuko huo sasa uweze kuwa na jumla ya mtaji wa shilingi bilioni 1.8 na katika hizo Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali Vijana, utaongezewa shilingi milioni 385 za Kenya mwaka huu na ule wa Akinamama Wajasiriamali utaongezewa shilingi milioni 440. Kuna Mfuko wa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati

(*Small and Medium Enterprises*) wao watapewa shilingi bilioni 1.0. Lakini vilevile, kila Jimbo litapewa shilingi milioni 1.0, kwa hiyo itakuwa jumla ya shilingi milioni 210 kwa ajili ya kukuza michezo kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeamua kupitia hii kuona namna gani wenzetu wa Kenya na Uganda wamefanya katika bajeti zao, ukiangalia hapa katika ukurasa wa 49, Wizara ya Fedha, imetenga Bajeti katika vipaumbele vyote vilivyotajwa isipokuwa kipaumbele cha kukuza ajira kwa vijana. Lakini vile vile nilikuwa *keen* kujaribu kuangalia hata kwenye hiki kitabu cha miradi ya maendeleo, *Vote 65*, maana nilitafuta *element* ya *job creation*, *Vote 65*, haijatengewa Bajeti yoyote katika kukuza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yetu iliangular hili suala vizuri. Kama wenzetu wa nchi ya Kenya na Uganda, wameamua kutoa *specific programs* na *specific budget*, pamoja na kwamba na wao wana vipaumbele vingine vyta miundombinu na vyenyewe vimetengewa bajeti zao, vipaumbele vyta elimu kama ambavyo sisi tumevianisha kwenye bajeti yetu, ni vizuri sasa tutenge *programs* za kukuza ajira mahususi kabisa, lakini pia itengwe bajeti ya kukuza ajira. Hiki kipaumbele cha kupanua ajira kwa vijana kwa kweli kinatia moyo sana, vijana wengi wamehamasika lakini ili kitekelezwe, kwa kweli kinahitaji bajeti yake. Sijaona hapa, Serikali haijaonesha wazi ni kiasi gani cha fedha kitatumika, haijaonesha wazi ni program zipi ambazo zitafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala la wafanyakazi, hili liliikuwa ni ombi tu kwamba Serikali ilishakubali mikopo kwa wafanyakazi wa *rank* zote wa Serikalini na hili lilipitishwa kwenye Bunge lililopita. Naipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo kubwa, kwa vile inaonesha sasa inawajali wafanyakazi wetu. Lakini ningeomba sasa, hebu hii mikopo wapewe wafanyakazi, kwa sababu mpaka sasa hivi hawajapata hiyo mikopo! Ni vizuri sasa wapewe hiyo mikopo ili waweze kufanya mambo mengine ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumalizia kwamba, wakati watumishi wote wa umma wakiwa wanaadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma, nawaasa wawe waadilifu, wawe wachapa kazi na wawe waaminifu na wazingatie maadili katika kazi zao. Haya yote tunayoyajadili katika bajeti hii, hayawezu kutekelezeka kama wao hawatafanya kazi kwa bidii, kama wao watakuwa warasimu, kama wao hawatakuwa na nidhamu ya kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa Rehema kwa kunipa tena uwezo wa kusimama mbele ya Bunge hili, kutoa mchango wangu katika mada yetu iliyotukabili hapa ya Bajeti. Nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii, kwa maana ya kutoa mchango wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naanza kwa kuanzia pale alipoishia Kiongozi au Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Bajeti hii, kwa kukiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi wake kwamba Bajeti hii ni nzuri na inatekelezeka, ikiwa kila mmoja atatimiza wajibu wake pale alipo. Naungana naye moja kwa moja, nasisitiza hilo, kwa sababu michango yote iliyotolewa na Wabunge Wenzangu, bila ya kuwa na uwajibikaji na tukatekeleza majukumu yetu na dhamana ambazo tumepeewa, basi haitotekelzeza wala haitofanikiwa bajeti yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Serikali kuanzia Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote, kwa kila mmoja na sehemu yake aliyokabidhiwa wawajibike kutimiza malengo ya bajeti hii ili kusudi nia na madhumuni hasa yaliyokusudiwa yafikiwe, ili Mungu akijalia, *Inshallah*, mwakani hapa tukisimama siku kama hizi za kuchangia bajeti, kupitia Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi tuwe tunasimama kifua mbele, kutekeleza yale ambayo tuliyapitisha, *inshallah*, tutayapitisha kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaasa tena Watendaji. Mheshimiwa Rais, alishawapa majukumu ya kutekeleza na kila mmoja anajua hilo. Hivi karibuni tu, alitiisha semina elekezi hapa Dodoma na kwa jumla Watendaji wote wa ngazi za juu na hata Wakuu wa Vikosi vya Usalama na wengine mlhudhuria katika kuelekezana na kutekeleza majukumu yenu. Hii si mara ya kwanza, nakumbuka iliwahi kutokea kule Arusha, mwanzoni tu mwa Awamu ya Nne ambayo pia nia na madhumuni ni kila mmoja ajue wajibu wake. Mheshimiwa Rais, alishafanya pia ziara kwa Wizara zote, kutathmini utekelezaji au kazi ambazo kila mmoja alipangiwa nazo. Hii yote ni kuonesha ni kiasi gani ana nia halisi na ana imani na ninyi aliowachagua.

Basi nawasihi sana ndugu, msituangushe sisi Wabunge na wananchi tumewaamini tukawawekeni mlipo, mkae mkijua kwamba kuna mafisadi na mahasidi. Leo nataka niwafahamishe nani fisadi hasa kwa sababu hili neno fisadi watu wengi sana wanalitumia ndivyo sivyo. Lakini leo nataka kuwafahamisheni fisadi ni nani, na hasidi ni nani? Mtu hasidi na fisadi ni mtu mmoja na kwa kawaida mtu huyu huwa hataki sababu ni roho yake mbaya tu ya kutaka kufisidi kitu ambacho kinaonekana kinanawili vizuri au kinapendeza, sasa yeje kwa uhasidi wake ule anachukia. Ule uhasidi ni *primary stage* kwa anayechukia moyoni lakini akianza kufanya vitendo ule ndiyo ujisadi, anataka kukifisidi kile kisiwepo. Mtu huyu kwa kawaida au watu hawa wanakuwa ni waongo, wazushi, fitina na wala hawana haya wakati anapotetea ujisadi wao na ni mtu mbaya aliyejewa hana aibu. Anaweza kukaa akasimama mbele ya vyombo vya habari akazungumza mambo macho makavu kama mjiswi aliyejewa na mlango. Basi ndugu zangu ninyi nawaomba sana msitoe nafasi hii kwa mafisadi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu waliochukua hela zetu si mafisadi, wale ni wahujumu uchumi na Sheria ya Uhujumu Uchumi, imeshatungwa katika Bunge hili na ipo na inatekelezwa na wapo ambao washatekeleza na mnajua ninyi ni mashahidi. Lakini hawa mafisadi naona bado, maana yake wako watu wanataka kufisidi nchi yetu kwa kutugombanisha, kuondoa usalama wetu, upendo wetu, tugombane na wameanza, inafika hadi tunauana wenyewe, huo ndiyo ujisadi, ujisadi siyo kuchukua hela wale ni wahujumu uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnakumbuka kwenye miaka ya 80 hapa kulikuwa na *operation* ya kuwakamata wahujumu uchumi wale wenye umri kama mimi wanakumbuka sana, wale ndiyo wahujumu uchumi na wapo bado, wao wanachukua hela zetu lakini Sheria ipo ya Uhujumu Uchumi, ningeomba Serikali ilete pia Sheria ya Mafisadi hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo nilitaka kuwafahamisha katika Serikali yenu ya Awamu ya Nne, kuna jambo moja zuri sana limefanyika, Chuo chetu cha Dodoma (*UDOM*), hapo basi mafisadi walishakiona, wameanza kufisidi, sasa wanagombanisha wanafunzi na walimu wao wanagombana, nia ni kukifisidi kile chuo ili kisambaratike, wale ndiyo mafisadi. (*Makofi*)

Ndugu zangu msilitumie vibaya neno fisadi, fisadi ni mtu ambaye anafisidi kitu ambacho kinanawiri au kinapendeza, nia yake kife kabisa na wamejitokeza, basi muwe na tahadhari na sababu mojawapo wanayoitafuta hawana sababu wala hawataki hela, hawa wako radhi kutumia hela zao kufisidi kile kitu, waliochukua hela wale ni wahujumu uchumi. Ndugu zangu tuwajibike, kila mmoja na sehemu yake, nafikiri mmenielewa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja sasa *TRA*, nilikuwa nataka kuzungumza kuhusiana na *TRA*, Mheshimiwa Waziri wa Fedha utakapokuja kuhitimisha bajeti yetu kesho unipe ufanuzi hasa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chomboh ongea na kiti.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Fedha kesho atakapohitimisha bajeti yake atueleze ni namna gani wanakusanya kodi ya pesa ambazo Makampuni ya Simu wanatoa huduma ya M-Pesa, Z-Pesa, T-Pesa, kuna kodi zinapatikana pale ndani, ni namna gani wana *deduct* na wanapata kiasi gani katika kodi zile, kuna habari kwamba, kuna pesa chungu nzima kwa sababu hawa watu wa Makampuni ya Simu ni wajanja sana kukimbia kodi. (*Makofi*)

Kwa mfano wakati wa uuzwaji wa Kampuni ya *Zain* ikaingia kwenye *Airtel*, kuna pesa chungu nzima za kodi pale Serikali imekosa, kwa hiyo, lazima tuwe macho katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, *TRA*, hivi juzi wametoa waraka ambao kuna mtandao mpya wa kuweza kutathmini magari ambayo yametumika kutoka ng'ambo na kuingia nchini. Waraka huo umetoka siku ya tarehe 31 Mei, lakini ulianzia kazi tarehe 3 Juni, kuna watu wa Tanzania wameagiza magari yao ambayo yameshafika nchini kabla ya kipindi hicho na sasa hivi ninavyozungumza kuna magari ambayo yalilipiwa ushuru tofauti na mtandao huo lakini hayakupata *release* kutoka bandarini kwa sababu kwamba, yameshaingia katika mtiririko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri badala ya kuwafanya wafanyabiashara au waagizaji wa bidhaa kulipa kodi, badala kuwapiga adhabu ni kuwafanya wawe marafiki wa *TRA* na kulipa kodi hili limewafanya watu wachanganyikiwe basi kuna watu walikuwa wanajua kodi inakuwa namna gani lakini *all over the sudden* kwa ghafla imekuja mtandao huu umeshaingia wakajikuta wamekwama na kuna magari zaidi ya 400 pale kwanza ndiyo kutoka *transit* kule Zanzibar yamekwama pale hawajui wafanye nini na tayari walikuwa wameshalipa ushuru na wameshalipa tofauti ile ya ushuru uliotakiwa lakini magari yako pale hayakuwa *released*, naomba Mheshimiwa Waziri akija atueleze kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitambulisho vya uraia, naomba Serikali sasa hivi imeshaamua na ichukue juhudhi kile kitengo cha vitambulisho vya uraia kipewe pesa ambazo zitatengwa katika bajeti hii, kifanye kazi kwa sababu tutakapotoa vitambulisho vya uraia tutaweza kutathmini kodi, tutathmini watu wetu na ndiyo kichocheo cha maendeleo ya kila mahali. Hizi faini zinazotakiwa kutolewa shilingi 20 mpaka 50 ukitumia vitambulisho ya uraia ambavyo na teknolojia ya sasa hivi iliyokuwepo ni *smart card*, unaweza ukam-*direct* mtu kokote aliko na akalipa kwa wakati, hakuna sababu ya kuweza kulipishana kodi 20 mpaka 50 tunatengeneza nini si zaidi ya kuwatengenezea rushwa tu, nafikiri siyo jambo la busara kuweza kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TPDC*, ningeomba sana Serikali kwa makusudi kabisa iwape uwezo *TPDC* kuagiza mafuta kama ilivyokwishaamriwa ili kusudi kuweza kuonyesha angalau ule unafuu wa bei za mafuta ambao umetokeza huko ili kupunguza tozo tunayozungumza hazitoonyesha hasa ule upungufu wa bei ambao tunategemea zaidi kuwe na chombo ambacho kinaweza kuwa *kika-govern* ile petroli na yale mambo mengineyo. Lakini pia kuipa nguvu kuweza kuishughulikia gesi yetu ambayo iweze kutumika kwenye magari na pia iweze kutumika kwenye magari na pia iweze kutumika majumbani kwa maslahi ya wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla kengele ya mwisho haijapigwa, ningeomba tena kuwasisitiza ndugu zangu watendaji kila mmoja kwa sehemu aliyonayo, tujitahidi, hebu tufanye kweli ili tusiwape nafasi na Mwenyezi Mungu atawashinda wasitimizie hizo haja zao ya kuifisidi nchi yetu na hawatoweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa kuokoa muda wetu, wanaofuatia sasa hivi ni Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Kimwanga, Mheshimiwa Shekifu, pia Mheshimiwa Luhaga Mpina wote wajiandae. Mheshimiwa Sakaya!

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012. Nichukue nafasi hii kwa kutumia sekunde chache kwanza niwapongeze viongozi wangu wa Chama cha Wananchi (*CUF*) Taifa, Viongozi Wakuu wakiongozwa na Profesa Ibrahimu Lipumba, Mchumi wa Dunia na Manaiju wake wote na viongozi wengine wote. Pia niwashukuru sana wanachama wa *CUF* wote na wananchi wote

kuendelea kuniunga mkono katika utendaji wangu, nawaahidi nitakuwa mwaminifu, nitafanya kazi kwa bidii na sitachoka, nitaendelea kupigania haki zao mpaka siku ya mwisho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu ya mwaka huu 2011/2012 imeendelea kuwa ni bajeti tegemezi, mapato ya Serikali ni trilioni 7.13 wakati matumizi ni trilioni 8.6, matumizi ya kawaida yanazidi mapato ya Serikali kwa karibu trilioni 2.5, ni hatari sana kwa Taifa letu kuendelea kutegemea bajeti isiyokuwa endelevu kwa miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu inategemea sana wahisani, inategemea sana mikopo, wahisani wana haki ya kutoa pesa kwa muda wanaotaka, wana haki ya kutotoa au kwa kiasi chochote wanachokiweza. Pia tunajua mhisani ye yule wana *interest* zao kwenye hii nchi, huwezi kupata msaada bure lazima kuna *interest* zao. Saa nyingine Serikali inaingia kwenye mtafaruku na makampuni ambayo nchi zao zinatoa msaada, wanashindwa kutatua matatizo na makampuni hayo kwa sababu wanaogopa watanyimwa misaada na imewahi kutokea kwamba wakiingia kwenye mtafaruku tu msaada hautoki. Kwa hiyo, tumewekwa kwenye kilengeo kama tumetegeshewa kwamba hata kama kampuni imefanya kosa hamwezi kuishughulikia kwa sababu mnaogopa mtanyimwa msaada, tutaendelea kuwa na mfumo huu mpaka lini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea Serikali inakopa, Serikali inapokopa ndani kwanza inadhoofisha zile taasisi binafsi wanashindwa kupata fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, kwa ujumla wake hatuwezi kuwatoa Watanzania kwenye dimbwi la umaskini kama hatutaweza kuwa na bajeti inayojitegemea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje nchi ya Kenya, nchi isiyokuwa na rasilimali inaweza kuwa tegemezi kwa asilimia nne, nchi yetu inakuwa tegemezi kwa asilimia 29, nchi ya Kenya ina nini ambacho inatuzidi, sisi Tanzania tuna rasilimali za kila aina, tunashindwa nini kutumia rasilimali zetu kwa ajili ya kuwa na uchumi unaojitegemea, tungekuwa jangwa kama Namibia, tungekuwa hatuna rasilimali tusingekuwa tunashangaa kwa nini tunakuwa tegemezi, lakini sisi ni matajiri wa rasilimali, tumejaliwa kila kitu na neema ya Mungu hapa Tanzania, ni kwa nini tuendelee kuwatesa Watanzania kwa kushindwa kuwa na mapato mazuri yanayoweza kukidhi mahitaji yao? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mianya mingi sana ya mapato ya Taifa. Tumekuwa tunatoa hapa mapendekezo miaka nenda rudi. Tangu nimekuwa Bungeni, huu ni mwaka wa sita tumekuwa tunatoa vyanzo vya mapato, vyanzo vile Serikali haivitumii, samaki wanavuliwa bure, wanaondoka, ni shamba la bibi, madini yanaondoka, wanyamapori wanasafirishwa mpaka ndege zinakuja zinashuka, zinabeba, zinaondoka, misitu inateketea, tuna tatizo gani? Tunashindwa nini? Tuna watalam tumewasomesha na tuna watendaji ni kwa nini tunashindwa kuwa na bajeti ambayo inajitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inauza nje madini tena mengi sana, tunauza madini ya dhahabu nje yenye thamani ya karibu bilioni 1.5, tunaambulia mrahaba wa milioni 45 tu na bado makampuni hayo yanaidai Serikali kodi ya mafuta, kodi ya pesa ambazo wamelipia mafuta kwa ajili ya *ku-run* mitambo yao, bado hapo hapo

wanasafirisha mpaka udongo wa madini, hivi kweli unafikiri kwamba kweli mwekezaji ni mjinga, achukue mchanga, asafirishe, apeleke Denmark, Canada, kwamba hajui anachokipata. Kwa hiyo, sisi tumetulia kwa vile tumeridhika na tulichonacho, tuendelee kukopa tu, tuendelee kuwa na madeni, tuendelee kuomba misaada wakati rasilimali ya Tanzania inanufaisha watu wachache, ni lazima Serikali ijiangalie, lazima wakae chini wabuni vyanzo vya kuweza kupata mapato, tatizo ni kuvitumia. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Serikali kushindwa kusimamia utafutaji wa masoko kwa mazao ya biashara yanayozalishwa hapa nchini, nalo ni tatizo lingine ambalo linainyima Serikali mapato makubwa sana. Ukiangalia taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2010, utaona kwamba mazao ya biashara karibu yote ikiwepo pamba, korosho, chai, karafu, *cocoa* na mazao mengine yote thamani yake ilishuka na sababu ambazo zimetolewa na Serikali kwenye kitabu cha hali ya uchumi ni kwamba uzalishaji ulishuka, swalii la kujiuliza, ni kwa nini mazao karibu yote ya biashara uzalishaji ushuke? Kwa hiyo, ina maana kwenye mazao ya biashara haijawekeza vya kutosha. Tukiangalia kwa mfano, kahawa, mwaka 2009 ilikuwa tulipata USD 111.2 mwaka 2009, mwaka 2010 tumepata USD 101.7, kwa hiyo, pungufu ni asilimia 8.6, hiyo ni kahawa. Tukiangalia thamani ya pamba na yenye ilishuka, mwaka 2009 ilikuwa dola 111, mwaka 2010 dola 84.0, pungufu ni asilimia 24.3. Tukiangalia chai na yenye ilipungua karibu upungufu wa dola 22.4 na mazao mengine. Kwa hiyo, thamani ya mazao yetu inazidi kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma mazao haya ambayo ni ya biashara Serikali iliyapa uzito mkubwa sana na iliyapa uzito kuanzia kule kwa wananchi wale wanaolima kwa mfano, kahawa, wananchi wanaolima kahawa walipatiwa pembejeo, walipatiwa mbolea, walipatiwa madawa, walipatiwa na masoko ya kufaa, chai hivyo hivyo, *cocoa* hivyo hivyo, tumbaku hivyo hivyo. Leo wakulima wanaolima mashamba madogo madogo vijijini wamekata tamaa hawana uwezo wa kulima kwa sababu Serikali haiwaangalii kwa vyovyyote, hawapati ruzuku yoyote ya kuweza kuendeleza haya mashamba. Ukienda Bukoba na Kilimanjaro wameanza kung'oa kahawa wanapanda migomba sababu hawaoni faida ya ile kahawa. Mkulima ulime kwa shida uje uipate hata masoko pia ni shida, hili ni tatizo. Naiomba sana Serikali, ili tuweze kukuza uchumi wa ndani ni lazima tuhakikishe tunaangalia sana mazao ya biashara, lazima tuzalishe vya kutosha na *tu-export* pia, *tusipo-export* tutakuwa ni watu wa kuuza vya wenzetu, sisi tutakuwa bado hatuwezi kuinua uchumi wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye masuala ya mifugo, tuna mifugo mingi sana Tanzania, tena mingi kweli kweli, lakini bado ukiangalia hatujaweza kutumia rasilimali ya mifugo kwa ajili ya kipato na hii inadhihirika wazi kwamba, ngozi zetu zinaozea vijijini hazina thamani, tuna-*import* kila siku, tuna-*import* toka nje, kama vile Dubai na Uarabuni, viatu vya ngozi, mabegi ya kinamama, mikanda, tunaingiza vitu vingi lakini najaribu kufikiria viwanda vyetu vya ngozi Tanzania vingine viko *ICU*, vingine vimeshakufa kabisa kabisa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Serikali ikaamua tu kwamba viatu vya shule kwa watoto wa *primary* na watoto wa sekondari vitoke hapa nchini, viatu vya shule tu tusiende kwenye viatu vya akinamama, sijakwenda kwenye vitu vingine, ni pato gani

kwa mwezi ambalo lingeweza kuingia hapa, lakini kila siku tunaingiza makontena. Tunapoingiza vitu kutoka nje, tunawatengenezea wenzetu uchumi wao, hili Serikali inafahamu, kwanza tunaimarisha viwanda vyao, pili tunawatengenezea watoto wao ajira, tatu tunainua uchumi wao, lakini ni kwa nini tushindwe kwa vitu ambavyo viko ndani ya uwezo wetu, tuna tatizo gani? Tunao wasomi, tuna shida gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu ambacho kinanisikitisha kama nchi yetu kuingiza *tooth pick* ndani ya nchi hii, *tooth pick, cotton buds*. Tuna vijana wengi wamesambaa mitaani, wamezagaa hawana kazi, tunashindwa kuwapa ajira ya kutengeneza *tooth pick*? Tunaomba Serikali iangalie vitu ambavyo kweli tunaweza kuingiza kutoka nje, tuingize, vilivyo ndani ya uwezo wetu Waheshimiwa Mawaziri, tuvitengeneze, tuviuze ili kupatia vijana wetu ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mifugo. Inaonekana hata viongozi waliopewa *mandate*, waliopewa mamlaka makubwa hawajatambua thamani ya mifugo kwenye maeneo yao. Nitoe mfano mmoja tu kwa mamlaka au kwa maagizo ya Mkuu wa Wilaya, Wilaya yangu ninayotoka Wilaya ya Urambo, ameweza kukamata mifugo karibu 6,000 amewafungia *custody* amewaweka mahali, siku tano hawajala chochote wala kunywa chochote, siku tano mnyama hajanywa maji, hajala chakula na wakati Polisi na Mgambo wanawakamata na Maafisa Wanyamapori wanawaleta pale kwenye lile eneo wamepiga risasi ng'ombe saba wamekufa barabarani, ukijaribu kuangalia ng'ombe saba tayari kwenye uchumi ni kitu, ukiangalia wale wanyama wamedhoofika pale siku tano, tayari tumeharibu uchumi wa Taifa. Kwa hiyo, hata Mkuu huyu wa Wilaya hatambui thamani ya mifugo iliyoko kwenye Wilaya yake, kwamba ni *source* ya *income* kwenye Wilaya yake. Inaonyesha kwamba hata semina elekezi, baadhi ya watendaji wengine haziwasaidii, tunawaomba sana rasilimali zetu tuzitumie kwa ajili ya kusaidia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la tumbaku. Serikali imekazana sana, kila mwaka ukiingia Serikali inakazana kweli kweli kuongeza ushuru kwenye tumbaku, huu ni mwezi wa nne, wakulima wa Wilaya ya Urambo na Mkoa wa Tabora wamerundika tumbaku ndani haina mnunuzi. Wana hali mbaya kweli ya maisha, hata uwezekano wa kupata chakula sasa hivi haupo na ukizingatia kwamba wakulima wetu ni wakulima wa jembe la mikono mtaji wao ni kidogo, anategemea auze alicholima ili aweze kupata mahitaji mengine ya familia na pia ajiandae kwa kilimo kijacho. Kwa hiyo, kuendelea kukaa nayo pale ndani hajui hatima ataiuza lini, tunawakatisha tamaa, hivi sasa tunapoelekea hata tumbaku, wakulima wataacha kulima. Sasa sijui mtakuwa mnapandisha kodi wapi, sielewi! Maana kodi inapanda kwenye tumbaku, inapanda kwenye bia, inapanda kwenye soda, Watanzania wakiacha kunywa bia sijui itakuwaje, tukiacha kunywa soda wote sijui itakuwaje na tumbaku nayo tukiacha kulima nadhani tutapoteza mapato makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ihakikishe kwa uvumba na ubani na kwa namna yoyote ile wakulima wa Mkoa wa Tabora na Mikoa mingine ambayo Tumbaku haijauzwa wanapatiwa masoko, vinginevyo tunawakatisha tamaa na wana hali

ngumu sana ya maisha kwa kuwa hawana *means* nyingine zaidi ya kutegemea kilimo na mpaka sasa hivi hawajauza Tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni bajeti nzima ya Serikali. Sijaona sehemu ambayo imelinda mazingira kwa kusaidia kupunguza ushuru kwenye nishati ya kupikia, sijaona! Bajeti nzima ya Serikali haijangalia Gesi, Umeme, Mafuta ya Taa, Motopoa na kadhalika. Sasa tunaomba Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie kwamba bajeti hii inamsaidiaje mwanamke wa Tanzania kupata nishati ya kupikia? Mazingira yetu yanateketea, kitendo cha Serikali kutopunguza ushuru, kwenye nishati umeme na gesi havishikiki, Mafuta ya Taa lita moja shilingi 1,700/= au 1,800/=, Motopoa ndiyo usiseme. Ni kwamba Serikali imebariki mazingira yaendelee kuharibika kwa sababu nishati pekee ambayo Mtanzania anaweza kumudu ni nishati ya Mkaa na Mkaa sasa hivi unaendelea kumaliza misitu yetu na nchi yetu itageuka kuwa jangwa. Naomba sana tuambiwe ni kwa vipi nishati itapatikana na suala la kuuliza haya makaa ya mawe, nilitegemea bajeti hii ingetwambia makaa ya mawe yanaanza kutumika lini? Kwa nini hatutumii nishati ya makaa ya mawe kwa ajili ya kupikia chakula majumbani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tunaendelea kukalia rasilimali ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu huku tunashuhudia misitu yetu ikiteketea? Huu ni udhaifu mkubwa kwa Serikali. Kwa hiyo, naomba sana suala hili liangaliwe kwa sababu ni lazima tule vyakula vilivyopikwa, ni lazima wananchi wapike, hawana jinsi, lakini kwa kuendelea kuachia bila kuwa na nishati mbadala kwa kweli ni matatizo na tutakaribisha jangwa tupende tusipende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ...

(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Anayefuatia ni Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, hayupo! Mheshimiwa Henry Shekifu.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru wewe na niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Lushoto kwa kuendelea kuwa na imani na mimi. Lakini pia nianze kumshukuru sana Waziri wa Fedha, Ndugu yangu Mheshimiwa Mkulo kwa kazi nzuri ya uandaaji wa bajeti ambayo kwa kweli ni nzuri. Naelewa wazi kwamba kitu kilichopo katika sahani ni kidogo na ni lazima kwa kweli kila mtu apate, ni rahisi kusema lakini siyo rahisi kutenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mbunge mmoja aliyetoea tafsiri ya ujisadi, Mheshimiwa Chomboh alieleza vizuri kwamba wale ambao wanaharibu hali ya hewa kwa madhumuni yao, hawa ndiyo wanaopaswa kuitwa mafisadi. Kama leo huwezi

kuona ukweli posho umeipokea kuanzia mwaka 2005, leo ni mwaka 2011 unakwenda kuchafua hewa, hizo za nyuma utazirejesha? Sitaki kuingia huko lakini niende katika mjadala na kuwahakikishia wenzangu waliopo upande wa pili, nitajielekeza zaidi katika fikra nzuri ambazo zinajielekeza katika Jimbo langu. Naamini kabisa bajeti haitoshi lakini kushauri ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza na upande wa barabara. Nachukua nafasi hii kuishukuru sana Wizara ya Ujenzi kwa kutenga fedha kidogo kwa ajili ya barabara ya kuunganisha Jimbo langu la Lushoto na Makao Makuu ya Wilaya ya Lushoto. Barabara ya kutoka Mombo kupitia kijiji cha Ngulwi ambako ndiko nilikozaliwa kufika Lushoto ambako kwa kweli ni kilomita chache na ni barabara ambayo kukiwa na dharura inaweza ikatumika. Nawashukuru sana lakini niendelee kuomba barabara ya kutoka Mlalo, Ngwelo, Mlela, Makanya hadi Mashewa ambayo inahudumia Majimbo manne katika Mkoa wa Tanga, basi iangaliwe katika kupandishwa daraja ili iwe barabara ya Mkoa kwa sababu ni barabara muhimu sana. Niishukuru pia Serikali kwa ujenzi wa barabara ya kutoka Lushoto kwenda Magamba kwa kiwango cha lami, naomba iendelee hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua yapo mahitaji mengi ya barabara lakini niseme tu kwamba barabara ya kutoka Magamba kwenda Mlola ndiyo barabara kuu katika Jimbo langu, isimamiwe vizuri, naona juhudzi za Serikali zipo, kwa hiyo, ni kuendelea kusisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji, ni kweli kwamba tunahitaji maji. Katika bajeti hii tumezungumzia upelekaji wa maji na Wabunge wengi wamelalamika sana kuhusu miradi ya *World Bank*. Kwa kweli miradi hii imechelewa sana, wananchi wameanza kupoteza tumaini. Lakini nisisitize kwamba mipango hii ikamilike ili maji yapatikane. Ni kweli kwamba hata bajeti ambazo zimebekwa katika miradi hii ambayo inahudumiwa na fedha za *World Bank* vile visima 10 au vijiji 10 kila Wilaya, ukweli ni kwamba hazitoshi kwa sababu muda umepita sana. Visima hivi vilianza kuzungumziwa kuanzia mwaka 2004 mpaka leo bado. Kwa hiyo, hata utekelezaji wake utakuwa ni mgumu sana, mafanikio yake pia yatakuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ushauri kuhusu uvunaji wa maji, haukusitisizwa sana katika bajeti. Yapo maeneo kame ambayo kwa kweli bila kuweka mpango wa kuvuna maji bado tutaendelea kuwa na matatizo, maeneo mengine hayapatikani maji ya kuchimba chini lakini kwa kujenga mabwawa nina uhakika tunaweza kuiondoa nchi yetu katika tatizo hili kubwa la ukosefu wa maji na kuiweka katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi ya Kenya ni jirani tu, wenzetu wana Chako *Dams*, kwa maeneo ya wafugaji, hizi zimesaidia sana na Serikali imeweza kuongeza fedha kidogo, wananchi wenye kwa juhudzi zao wakajipanga *Chako Dams* zitajengwa. Ni mabwawa madogo madogo ambayo kwa muda fulani yanaweza kusaidia. Sisi watu wa milimani, kwa mfano China katika Jimbo la Hainan au Guangzhou wenzetu wanavuna maji yanayoweza kutumika na kaya hata 2000 kwa sababu wanaanza

kuyavuna kuanzia katika vyanzo vya msingi yanashuka na yanaendelea kutumika, kila mahali yanapofika yanajengewa kizua, yanasaidia kwa ajili ya umwagiliaji.

Kwa hiyo, naamini Serikali ikitenga fedha za kutosha kwa mfano, Mkoa wa Manyara kule Mbulu kuna bwawa la Mangisa, wananchi wamejengewa bwawa lile, sasa hivi wameweza kuongeza uwezo wa uchumi wao kwa kulima vitunguu swaumu ambavyo vinauzwa nchi za nje mpaka Uarabuni. Wamejengewa na ghala ambalo linasaidia kuweka vitunguu mpaka wakati wa msimu ambapo bei zitakuwa zimepanda. Naamini kwa kutumia mfano ule tunaweza kuleta mapinduzi ya maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu ni ardhi. Ni kweli kuwa kila Mbunge amelalamika sana kuhusu hatimiliki za kimila. Hatuwezi kuendelea na hatuwezi kupambana na umaskini bila kuitumia rasilimali ardhi vizuri. Naamini Serikali kwa dhati ikikubali na kulisimamia jambo hili, inawezekana. Kulikuwepo na mpango wa tathmini katika Wilaya mbili yaani Babati na Bariadi Mkoa wa Shinyanga. Serikali iliweka mpango ili kujaribu kutathmini kama kuna uwezekano kupitia fedha za *World Bank* ili kuweza kufanya mradi huu wa upimaji ardhi uwe ni kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri Serikali ikatoa kauli wakati wa hotuba ya Waziri wa Ardhi, ule mpango uliishia wapi? Kwa sababu kama tungefanikiwa katika hili tukaweza kutoa hatimiliki za asili wananchi wataweza kukopa. Maeneo kama Lushoto ambapo tuna uhaba wa ardhi, tuna uhakika wananchi watakuwa na uwezo wa kupata dhamana na waweze kukopesheka ili wajilettee maendeleo yao. Wanachokihitaji wananchi wa Lushoto ni kupata pembejeo ambazo kwa sasa ni ghali sana, lakini kama wataaminika kukopeshwa wataweza kulima mbogamboga na matunda na Serikali ikachukua jukumu la kuyasindika (*value added*) yaani kuyatengeneza katika hatua za mwisho. Nina uhakika wananchi wa Lushoto wataondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni usimamizi wa fedha, wenzangu wengi wamezungumzia. Bajeti hii imezingatia sana suala la usimamizi wa fedha, lakini kwa kweli naona kuna upungufu fulani. Katika upande wa fedha za kigeni tuna udhaifu mkubwa, usimamizi wa fedha za kigeni ni dhaifu, uzalishaji wa fedha za kigeni ni duni. Nchi yoyote isiyo na uwezo wa fedha za kigeni ni sawa na mcheza zumari anakwenda kwenye ulingo hana vifaa vya kuchezza. Hatuwezi leo kushindana katika dunia hii bila kuwa na fedha za kigeni ambazo zitatwezesha kununua vifaa vinavyohitajika katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli tumezungumzia katika *speech* ya Waziri, *Export Processing Zones*, lakini nazo hazijapewa msimamo na msingi wa kutosha maana hizi *Export Processing Zones* zinahitaji miundombinu, bila miundombinu kama umeme, barabara na maji hakuna mwekezaji atakayekwenda kuwekeza na hili ni kazi ya Serikali. Basi kama tutashindwa kuwekeza kwa nchi nzima ni vizuri basi tukachagua maeneo machache ambayo yameiva. Maeneo yale ambayo tuna uhakika miundombinu ya msingi kama barabara, umeme uko jirani, maji yapo na sisi ni kupeleka miundombinu hiyo ili uzalishaji uanze, itatusaidia sana katika suala la *export processing zones*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye umeme. Ni ukweli kwamba umeme mijini umetengewa karibu 70% na vijijini bado ni 30%, ni kidogo sana. Naomba na ninasisitiza kwamba hakuna asijejua juhudzi zinazofanyika kupata umeme wa kutosha. Lakini niseme kwamba *REA* imeundwa kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini tuone kazi za *REA* yaani Mamlaka ya Usambazaji wa Umeme Vijijini. Mashirika mengine kwa mfano kule nyuma tulikotoka kama *TANESCO* au *TTCL* walikuwa na utaratibu wa kutoa vijitabu vidogo vidogo vya kueleza mipango yao ya miaka mitatu, minne au mitano kwa kuelezea umeme au simu au mambo yanayohusu mashirika yao, kama ni umeme utapelekwa wapi. Ni vizuri kwa leo kwa mfano, nikiweka katika mpango vijiji vya Tarafa ya Mlola vitapata umeme mwaka 2014, najua na nitawaambia wananchi wangu na tukienda kwa ratiba hizo tutakuwa na uhakika. Lakini kila siku maswali ni yale yale lini nitaletewa, Waziri akiamka anaahidi, tuna fedha chache na kadhalika. Sasa ni lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukaenda kwa ratiba na tukawa na programu. Tukiwa na programu nina uhakika hatutakuwa na malalamiko maana hakuna siku tutasema hela zinatosha lakini tukipanga vizuri hela zitatosha, pato letu ni dogo kutegemea vipaumbele vyetu, tukapanga vizuri, tukasimamia vizuri nina uhakika fedha hizi kila mmoja atapata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala la ardhi lakini sitzungumzia Benki ya Ardhi. Tunalo tatizo la kuwa na ardhi na sheria zinazoeleza vizuri. Nafikiri sheria namba 4 na 5 zinahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa ili nchi ijue wawekezaji wakija wapelekwe wapi, bila kunyanyaswa na engo ni ku waheshimu wananchi wetu katika ardhi wanazozitumia. Sasa ni vizuri tukajua maana hakuna nchi inayoendelea bila kujua uwekezaji na kitakachoombwa kwanza ni ardhi si vinginevyo, mwekezaji ye yote akija kulima kama tunataka wawekezaji wakubwa watakwambia nipe ardhi, sasa hatujui ardhi iko wapi kwa sababu hakuna *land bank* yaani Benki ya Ardhi. Ni vizuri Serikali sasa ikawa na utaratibu huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila Mkoa maeneo ambayo kwa kweli yatatumika kwa ajili ya uwekezaji, kwa ajili ya wananchi wetu na kwa ajili ya malisho na kilimo yajulikane na Serikali itenye fedha za kutosha. Kupanga ni kuchagua hatuwezi kufanya kila kitu lakini nafikiri kuna maeneo ambayo ni muhimu sana katika kuinua uchumi, kama hujyawakea msingi utalalamika kila siku. Nchi zote zilizoendelea zimechagua maeneo machache, kuna visiwa vidogo sana lakini wamechagua mambo muhimu machache yanawavusha kwenda mahali fulani, wakifika wanaongezea, kila mwaka wanaongezea jambo lingine. Kuwa na mambo mengi na kugawa kakuku kadogo tulikonako si jibu katika kupanga, ni vizuri tukapanga mambo machache tukayatekeleza kwa ukamilifu na tukaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika suala la mwisho ambalo nalo linahusu Jimbo langu ambalo ni usindikaji wa mazao. Bila usindikaji hatuwezi tukapiga hatua, lazima tukubali usindikaji ni kitu muhimu sana. Naomba Serikali katika suala la usindikaji kwa kweli kupanga pia ni kuchagua. Kuna Mikoa na maeneo ambayo yanalima mbogamboga...

(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, tunakushukuru sana naona muda umekwisha.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Anayefuata ni Mheshimiwa Luhaga J. Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani na Mheshimiwa Selemani Said Jafu ajiandae.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na bila kuchelewa niseme rasmi nalishukuru sana Bunge lako, katika Bunge la mwezi wa Nne niliomba ridhaa linitume kuwakilisha katika Bunge la Afrika nikisisitiza kuniwekea shwaaaaa mbele ya Mpina na Bunge lako lilifanya hivyo. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa heshima hiyo na niendelee kuahidi kwamba sitawaangusha katika uwakilishi wangu huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache sasa na kwa sababu hoja nyingi Waheshimiwa Wabunge wameongea basi, nitajaribu kujikita katika hizi chache zilizobaki au zile za kusitisiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyowasilisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha akisisitiza vipaumbele vitano ambapo katika hivyo vitano kuna Kilimo na Umwagiliaji pamoja na kukuza ajira za vijana. Wenzangu wote wameongelea vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusitisiza ni kwamba katika Sera ya Elimu ambayo inatayarishwa hivi sasa na inatarajiwu kuwasilishwa katika Bunge au katika Kamati nasisitiza suala hili la somo la ujasiriamali lifundishwe katika shule za msingi mpaka sekondari, wanafunzi wafundishwe elimu ya ujasiriamali na tuweke kwenye sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kilimo. Tunazungumzia kilimo wakati masomo ya kilimo tumeshayafuta katika shule. Unawezaje kukiendeleza kilimo wakati vijana ambao sasa wanaandaliwa ili baadaye wakasimamie kilimo hawafundishwi maarifa yoyote yale kuhusu kilimo? Nashauri katika Sera ya Elimu inayoandaliwa na ambayo itawasilishwa baadaye tuijadili. Suala la somo la kilimo lifundishwe kuanzia shule za msingi na sekondari ili vijana wajiandae vizuri zaidi kufanya kazi ya kilimo na hapo ndipo tunaweza tukafikia yale mapinduzi ya kijani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana, wakati nachangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, tulikuwa tunazungumza kwamba, sekta binafsi ili iweze kukua ni lazima uihakikishie kwanza upatikanaji wa mikopo *access to finance*, kwamba ni suala la msingi sana katika ukuaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali katika mpango wake wa kuipelekea Benki ya *TIB* shilingi milioni 100, sasa badala ya kuipelekea shilingi bilioni 100 kwa

muda wa miaka mitano, iipelekee shilingi bilioni 500. Serikali imekubali nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine lilikuwa ni kilimo, kwamba Benki ya Kilimo ipelekewe shilingi bilioni 100 kwa muda wa miaka mitano, nikaiomba Serikali ipeleke shilingi bilioni 500 kwa kipindi cha miaka mitano, Serikali ikakubali na nashukuru sana na huko ndiyo kuwa Serikali ambayo ni sikivu, Serikali ambayo inawasikiliza wawakilishi wake na kwa kufanya hivyo baada ya miaka mitano tutakuwa na uhakika kwamba wawekezaji wetu wakubwa, wadogo na wa kati wanapata mikopo wanayohitaji kwa muda wanaoutaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kulisisitiza hapa ni kwamba, kuna suala la kufikisha mikopo hii vijijini, tuna *VICOBA* vijijini, tuna *SACCOS*, hizi *SACCOS* na *VICOBA* basi viimarishwe ili viandaliwe vyema kupokea fedha kutoka kwenye hizi taasisi za fedha na zenyewe ziweze kutoa mikopo kwa wananchi wa kawaida kwa sababu mwananchi wa kawaida toka Meatu, kumwambia kwamba aje kuomba mkopo *Tanzania Investment Bank*, Dar es Salaam ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki nyingine ambayo naiomba Serikali iiangalie ni *Tanzania Postal Bank (TPB)*. Kwa muda mrefu benki hii na yenye we inafanya kazi kubwa, inakopesha *VICOBA*, inakopesha *SACCOS*, sasa hivi inakwenda mpaka inakopesha na Halmashauri kutekeleza miradi ya maendeleo, lakini mtaji wao ni mdogo mno na hii ni benki yetu ambayo tunamiliki asilimia mia moja (100%), hisa zote ni za Serikali. Zipelekwe fedha za kutosheleza mtaji wao ili waweze kuhudumia vizuri jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulisema hapa, ni posho na mishahara ya Waheshimiwa Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani. Maswali mengi yameulizwa hapa Bungeni lakini majibu ya kweli hatuyapati. Viongozi hawa tumewapa jukumu kubwa sana *D by D*, madaraka yote ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo tumeyapeleka kule vijijini, lakini Wenyeviti wetu wa Vijiji wanafanya kazi usiku na mchana, wanahudhuria vikao, wanasmamia miradi ya maendeleo, wanakusanya michango, wanasmamia suala la ulinzi na usalama usiku na mchana, Wenyeviti hawa wameendelea kujitolea kwa muda wa miaka mingi sana, lakini katika bajeti hii nimefungua vitabu vyote vya bajeti hakuna mahali ambapo naona sasa Serikali imewaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti huyu wa Kijiji ni tofauti na Mwenyekiti yule wa zamani ambaye alikuwa kazi yake ni kufungua kikao na kufunga kikao, anasubiri kikao kingine. Wenyeviti wa Vijiji wa sasa hivi ni wafanyakazi kabisa ambao wameacha shughuli zao zote za msingi kwa ajili ya kuhudumia umma, kwa nini waendelee kujitolea kwa kipindi chote hicho? Waheshimiwa Madiwani ambao kwa kweli ndio wanaotuwakilisha na ndiyo wanaosimamia fedha nyingi sana zinazopelekwa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumezindua mpango mkubwa wa miradi ya maendeleo wa miaka mitano ambao unakwenda kutekelezwa kule, Waheshimiwa Madiwani ndiyo wanaosimamia shughuli hizo kila siku, ndiyo wanaokwenda kusimamia fedha zetu hizo kwa kipindi chote, lakini Waheshimiwa Madiwani hawa tunawalipa sh. 120,000/= na nimeangalia hakuna mabadiliko katika bajeti hii, wanaendelea kulipwa posho hiyo hiyo ya 120,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba hii haiwezekani. Waheshimiwa wetu Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani, wanastahili kulipwa kama watumishi wengine. Sasa hivi tunasema kwamba wao wanajitolea na tunalalamika kwamba idadi yao ni kubwa, lakini kwa nini Mtendaji wa Kijiji analipwa? Kwa nini Mtendaji wa Kata analipwa? Leo hii tunaendelea kuanzisha mashirika ya umma kila kukicha na tukianzisha mashirika ya umma tunalipa mishahara minono, hakuna mtu anayejitolea, kwa nini hawa viongozi wao waendelee kujitolea kila siku? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kulalamika kwamba fedha watakazolipa kwa Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji ni kubwa, nikaangalia takwimu. Takwimu zinasema tunao Waheshimiwa Madiwani 4,451 nchi nzima, ukiwalipa shilingi 500,000/= kwa mwezi kila Diwani maana yake ni shilingi bilioni 2.2 kwa mwezi. Wenyeviti wa Vijiji wako 11,812 ukiwalipa shilingi 120,000/= kwa mwezi, utakuwa umelipa shilingi bilioni 1.4 kwa mwezi, jumla ni shilingi bilioni 3.6 kwa muda wa mwaka mmoja ni shilingi bilioni 43.2 tu (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma ile Volume II ‘*Public Expenditure*’ nimeisoma vizuri, nimeyaona majedwali na mapendekezo ya gharama zilizopendekezwa. Inawezekana hizi shilingi bilioni 43 tunaweza kabisa kuzitafuta kwenye kitabu hicho tukapunguza matumizi mengine. Watu wengine wanakwenda mafunzo kila siku, watu wengine wanakwenda safari kila siku, sasa tunaweza tukapunguza kabisa kutoka kwenye matumizi haya tukapatu mshahara wa shilingi bilioni 43.2, tukawalipa hawa viongozi, wakaendelea kusimamia shughuli zetu za maendeleo vizuri sana. Waheshimiwa Wabunge niwaombe, tunayo bajeti ya Waziri Mkuu hasa TAMISEMI, kama mishahara ya Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji haikuwekwa basi tusiipitishe kabisa bajeti hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu matumizi ya Serikali. Wakati nachangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, nilipongeza sana suala la Serikali la kupunguza matumizi yake ya kawaida kutoka mwaka 2009/2010 kwa kutoka asilimia sabini (70%) mpaka asilimia 63%) maana yake kwa asilimia saba (7%), lakini ikaongeza matumizi yake ya maendeleo kwa asilimia saba (7%) mwaka 2011/2012. Nilisema hizo kwa kweli ni jitihada nzuri za Serikali, Serikali imefanya kitu kizuri lakini bado tunaiomba Serikali iendelee kupunguza matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, alipokuwa anazungumzia suala la kupunguza matumizi, nikaangalia kipengele kilichozungumzwa kipengele cha *sitting allowance* na cha *per diem*, lakini bahati nzuri hotuba yake ni nzuri kwa sababu amesema yawezekana kipengele hiki cha *per diem*

kimepitwa na wakati kiboreshwe. Sasa ukiangalia kama kipengele cha *per diem* kinaboreshwu kwa maana ya kufuta *sitting* maana yake ni kipengele hicho tena hakitusaidii kupunguza matumizi ya Serikali kama tunavyoyazungumza sasa hivi. Naomba sasa nipayendekeze njia ambazo zinaweza zikaisaidia Serikali kupunguza matumizi yake. Njia ambazo zinaweza zikaisaidia Serikali kupunguza matumizi yake niliwahi kuchangia pia siku za nyuma kwamba, tatizo kubwa la matumizi ya Serikali yetu liko kwenye bajeti, huwezi kudhibiti matumizi ya Serikali kama hujadhibiti bajeti, ukiishakosea kupanga utakosea matumizi *obvious*.

Waheshimiwa Wabunge tumekuwa kwenye Kamati zetu, lakini bajeti tunazoletewa watu wanasema tu posho ya kujikimu milioni 200 hakuna *details* zinazoonesa kwamba milioni 200 hizo anajikimu akiwa anakwenda wapi ili *a-justify* matumizi hayo. Posho ya mafunzo hakuna *details* wanakwenda watumishi wangapi, kwenda kujifunza nini na kwa kipindi gani? Wabunge wangkuwa wanapata hiyo nafasi wangeweza kuyapunguza haya matumizi na kuzichukua fedha hizo na kuzipeleka kwenye miradi mingine. Kwa hiyo, kwenye Kamati Waheshimiwa Wabunge hebu tuangalieni kipengele kile cha kupunguza matumizi ya Serikali, posho za kujikimu, safari, mafunzo zipo Halmashauri zilizofanya hivyo na zikapunguza vizuri sana matumizi yao ya Serikali. Halmashauri ya Meatu, sisi tumefanya hivyo, tumpunguza matumizi shilingi milioni 120 tukazipata kutokana na kudhibiti haya matumizi ambayo hayana tija na zimekwenda kwenye shughuli ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo Wilaya nyingine kama Moshi, wao wamepata shilingi milioni 300. Kwa hiyo, wote tukifanya hivi tunaweza kuokoa fedha nyingi sana kutoka kwenye matumizi yasiyo na tija na tukapata fedha tukazirudisha kwenye fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, Serikali inatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kulipia pango la ofisi pamoja na kumbi. Pitia kitabu kile Volume II utaona *millions of money* zimeelekezwa katika matumizi hayo. Kwa mfano, hata Mashirika ya Umma, mengi yanapanga na wanalipa fedha nyingi sana. Sisi *TCU* pale pango tunalipa shilingi milioni 231 kwa mwaka, sasa shilingi milioni 231 ukiweka miaka 10 tu unawenza kujenga ofisi kubwa na sehemu nyingine ukapangisha ukapata fedha. Lakini tujiulize hivi ni lazima mpaka leo hii, kwa mfano, tunapozungumza *D by D*, leo Wizara ya Elimu yenye watumishi wengi wa shule za Sekondari pamoja na shule za misingi zimehamia TAMISEMI, watumishi hao walioko kwenye Wizara ile bado wanahitajika? Ukipitia *the whole Government structure* utagundua kwamba kuna matumizi mengi sana ambayo tukiipitia *Government structure* pamoja na mfumo mzima wa matumizi tukaupitia vizuri, tukaufanya marekebisho, tutakomboa matumizi mengi sana ya umma na kuyaleta kwenye shughuli za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu umekwisha lakini kuna mambo ya msingi kwa mfano, fedha zinacheleweshwa sana kupelekwa katika miradi ya maendeleo na katika matumizi ya kawaida, sijajua sababu ni nini. Mapato yetu ya ndani kuishia Machi yalikuwa ni asilimia sitini na tisa (69%) lakini mikopo ya nje ilikuwa ni asilimia mia moja na tatu (103%), miradi ya maendeleo ufadhili tulikuwa na asilimia hamsini na

nane (58%) lakini ukienda sasa kwenye utekelezaji, fidia ya vyanzo vya mapato vya Halmashauri ni asilimia thelathini (30%), Miradi ya maendeleo iko 0-20% basi, Serikali itwambie kwamba ucheleweshaji wa fedha au kwenye utekelezaji tatizo ni nini wakati fedha tunapata kwa wakati? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba tuna taarifa ya *financial*...

(*Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante muda wako umekwisha.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Anayefuatia ni Mheshimiwa Selemani Jafo, pia Mheshimiwa Assumper Mshama na Mheshimiwa Joseph Selasini ajiandae.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu jioni ya leo kwa kupata fursa hii kuongea na Watanzania katika suala zima la bajeti kwa mwaka huu fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe kwa kuniwezesha kijana wao na kijana mwenzao kufika katika Bunge hili na hasa siku ya leo nikijadili bajeti ya maendeleo, bajeti ya Taifa letu hili kwa muda wa mwaka fedha 2011/2012. Itakuwa si vyema kama sikuwashukuru wazazi wangu hasa mama yangu mzazi, namwomba Mwenyezi Mungu ampe kila la kheri pale alipo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujikita moja kwa moja katika bajeti hii, lakini naomba kujielekeza katika sehemu ambayo watu wengi naona hawajapenda kuigusa, suala la 1.9 trilioni, pesa za Kitanzania. Karibuni kila mtu anajiuliza kwa nini bajeti hii itenye fedha hizi nyingi sana kwa ajili ya madeni? Ndugu zangu, naomba kutofautiana na wenzangu, Tanzania yetu hii ndiyo tunaolalamika kwamba kuna Walimu wengi wanadai mishahara yao haijalipwa, Tanzania hii ndiyo tunaosema kuna Polisi wengi wanafanyakazi lakini bado wanaidai Serikali, Tanzania hii ndiyo tunasema kuna Manesi wanafanya kazi katika wakati mgumu, kuna malimbikizo yao bado hayajalipwa. Ndugu zangu Serikali isipotenga fedha hawa watu watalipwa vipi? Kama sisi Waheshimiwa Wabunge hatulioni hili ina maana kwamba kweli hatuguswi na wananchi wetu na wafanyakazi wetu katika sekta hii ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kkwa hilo lakini naomba kuzungumza lifuatalo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kipaumbele cha kwanza ihakikishe watumishi hawa wanalipwa madeni yao na malimbikizo yao yote. Hii ndugu zangu ndiyo itakuwa kumtendea haki Mtanzania anayefanya kazi katika mazingira magumu, ukienda hospitalini watu wanafanya kazi usiku kucha na wengine wanadai. Walimu wetu tunaona

mpaka wengine wanashindwa morali ya kazi kwa sababu wana madeni yao wanadai. Ndugu zangu naipongeza sana Serikali kwa kuweka fedha hizi, lakini naomba kipaumbele cha kwanza tuhakikishe kwamba Walimu wote, Polisi wote, wafanyakazi wote wa hospitali, Mabwana Shamba na wengineo walipwe madeni yao yote ikiwezekana haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kujielekeza katika ukurasa wa 57 ambapo inaongelea suala zima la kuwezesha marupurupu na mishahara ya wafanyakazi. Napenda kuishukuru sana Serikali kwa kuliona hili. Ndugu zangu *purchasing power* ya mfanyakazi wetu sasa hivi Tanzania imeshuka, gharama za maisha ziko juu sana kuliko kiwango anachokipata Mtanzania anayefanya kazi. Kwa hiyo, katika hili naipongeza sana Serikali, mtu anayesema bajeti hii haifai maana yake hamtakii mema mfanyakazi wa Tanzania anayefanya kazi katika mazingira magumu. Ndugu zangu hili ni jambo jema, wafanyakazi wetu wakipata hii mishahara ndiyo inawapa morali ya kuweza kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani asiyetaka mfanyakazi aongezewe mshahara? Naona ajabu kweli kweli mtu anamlilia mfanyakazi wa Tanzania, eti anasema nakuthamini sana halafu hapa anasema bajeti hii siiungi mkono, huyo anaonekana ana matatizo binafsi, ndugu zangu lazima tulione hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali hasa ijielekeze vizuri katika suala hili. Kuongeza mishahara ni jambo moja lakini kuna suala lingine, suala zima ni Maafisa Utumishi pamoja na Wakuu wa Idara. Tuna matatizo ya Maafisa Utumishi wengine, wana upendeleo, kuna wafanyakazi wengine wanafanya kazi za utumishi katika mazingira magumu lakini hawapandishwi vyeo hata siku moja, tatizo ni Maafisa Utumishi hawa tuliokuwa nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi kuna wengine ambaao ni Wakuu wa Idara, hawatoi mapendeleko kwa wafanyakazi wanaofanya vizuri isipokuwa kwa mtu wake *either* wa dini moja, khabila moja au upande mmoja. Hii ni hatari kwa mustakabali wa Taifa letu. Ndugu zangu japokuwa tunaongeza mishahara, lakini tuangalie maslahi ni kwa nani zaidi, lazima Idara ya Utumishi na TAMISEMI wahakikishe kwamba wanaweka watu ambaao wataangalia maslahi ya wafanyakazi wa hali ya chini, la sivyo ndugu zangu hatuwezi kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujielekeza katika suala zima la ardhi. Kila mtu anaposimama hapa anazungumzia tatizo kubwa la ardhi katika nchi yetu, lakini kuna watu wanaitwa Makamishna wa Ardhi, hawa wamekuwa kama Miungu watu, wanagawa ardhi ya watu kama karanga, hii ni hatari sana kwa mustakabali wa nchi yetu na ukiangalia migogoro mikubwa katika nchi yetu hii inasababishwa na hawa. Bahati mbaya sana watu hawa hata anapovuruga anahamishwa baada ya kuachishwa kazi, hii ni dhuluma kwa wananchi. Mtu akiharibu muondoe kazini, kuna vijana wengi wako mtaani wanasaaga soli kwa kutafuta hizi kazi. Kwa nini hawa Maafisa Ardhi wanafanya uharibifu na tunapata taarifa zao lakini hawajibishwi? Kuna nini hapa au tunapeana kazi kwa kujuana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatari na napenda kuwaambia kwa mfano, Jimbo langu la Kisarawe lina matatizo sana ya ardhi, matatizo makubwa na nina imani hata wengine Waheshimiwa Wabunge mna ardhi zenu kule na wengine wanapata hati miliki. Kwa mujibu wa sheria ni kwamba, huwezi ukamiliki ekari 300 bila Halmashauri ya Wilaya kuitisha hiyo *document*, wao wamepata hati miliki kutoka wapi? Maana yake hapa ni kwamba, ndani yake kuna ujisadi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili lazima tujipange, watu wote hata ambao wana hati miliki lakini ikiwezekana kama wamekuwa sheria tutawang'oa na tutawapeleka Mahakamani kwa sababu wamefanya ujisadi mkubwa katika nchi hii. (*Makofit*)

MBUNGE FULANI: Uhujumu uchumi.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Huo ni uhujumu uchumi na hili halivumiliki katika ulimwengu wa sasa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujielekeza katika suala zima la maji. Maji ni tatizo na janga kubwa katika nchi yetu hii. Kule vijijini watu wanaoga tunaita *passport size*, yaani mtu anaoga kuanzia kiunoni mpaka kichwani, anavua shati anaima anapigwa kopo moja tu la maji, ameoga kwa ajili ya shida ya maji. Sisi kwetu kule Uzaramoni tunaita mtu huyu ameoga kwa sababu kule maji ni tatizo. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Kisarawe watu wanakaa siku tatu wanatafuta maji, jamani ndoa mpaka zinaharibika, ndio maana mtu anayesema kwamba bajeti hii haikulenga nanihi, kipaumbele chetu cha bajeti hii ni suala zima la maji, wewe Mtanzania gani unasema bajeti hii haifai? Ndugu zangu naomba tujikite katika hili kuhakikisha kwamba tunapigana ili wananchi wetu waweze kupata fursa ya maji. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu Kisarawe kuna shida ya maji sana, wananchi wangu wa kule Chole, Mzenga hivi sasa wanalala visimani, shida kubwa kweli kweli, hata suala zima la kukuza uchumi linashindikana. Mtu anaamka saa kumi usiku mpaka saa saba mchana bado anatafuta maji, atalima saa ngapi? Naomba hili tuliwekee mkazo, kwa vile tumeweka kipaumbele cha maji, basi tuangalie jinsi gani wananchi wetu tutaweza kuwapa fursa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujielekeza katika suala zima la miundombinu ya barabara. Napenda kuishukuru Serikali kwa kuweka hiki kuwa ni kipaumbele, bila ya barabara bidhaa hazisafiri, uchumi haukui. Naiomba Wizara ya Miundombinu Jimbo langu la Kisarawe hivi sasa, ni mionganoni mwa miji mitatu iliyoanzishwa kwa wakati mmoja mwaka 1907, miji mingine ni Nairobi na Mji wa Goma. Kwa sasa Kisarawe ina miaka takriban 104, lakini leo hii Kisarawe ina tabaka la lami la kilomita 12.5 tu. Naiomba Serikali, Kisarawe ni *strategic area* ya uchumi, karibu na Jiji la Dar es Salaam, viwanda vinaweza vikajengwa kule, naomba ile ilani yetu ambayo nashukuru pia Serikali imeona kwamba tutajenga barabara ya lami kilomita 54 na ile kilomita 148 kutoka Makofia kuja Mlandizi, Mzenga mpaka Vikumburu naomba Serikali iweze kutoa nguvu

na watu wa Kisarawe nao wajione wako peponi sasa hivi kama wananchi wengine wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala zima la umeme. Wilaya yangu ya Kisarawe japokuwa iko karibu na mkoa wa Dar es Salaam ni vijiji vinne tu vyenye nishati ya umeme ni sawa sawa na asilimia 5.19, ina maana hata *average* ya Kitaifa hatupo. Lakini kwa kweli kwa dhati nipende kuishukuru Serikali yetu, nipende kumshukuru Waziri mwenye dhamana ndugu yangu Mheshimiwa William Mganga Ngeleja kwa kufanya changamoto kubwa, hivi sasa Mungu akijali huenda miaka 50 tukiitimiza basi umeme utakuwa umeshawafikia vijijini. Katika hili sasa naiomba Serikali kwamba nishati hii ya umeme tuweze kuweka nguvu kwa sababu tumeweka kipaumbele chetu kwa Taifa. Naomba tuikumbuke na Kisarawe basi tunavyosherehekea Uhuru, umeme utakuwa umewaka Msanga mpaka kule sehemu ya Mzenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala zima la makazi kwa askari polisi. Hivi sasa wengine ndugu zangu tunafanya uwekezaji wa majengo katika miji peke yake, vijijini askari polisi wapo katika mazingira magumu sana. Naomba tuweze kulirekebisha ili tuhakikishe jinsi gani kama vyombo vyala ulinzi na usalama vinapatiwa maeneo mazuri ya kuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujielekeza katika suala zima la viwanda. Bahati nzuri Bajeti hii imetuelekeza jinsi gani Serikali yetu inadhamiria kwa ajili ya kuboresha viwanda na ufufuaji wa viwanda maana yake utawawezesha vijana wengi kupata ajira, hili halina shaka. Lakini naiomba sana Serikali pale Kisarawe tuna kiwanda cha *KIBPRICO* na *STAMICO*, viwanda hivi vimukufa. Viwanda vile vingechukua vijana wengi sana katika suala zima la ajira. Kisarawe ipo karibu sana na Dar es Salaam. Naiomba Wizara yenye dhamana ya viwanda ije kutembelea kule Kisarawe na kuonekana kwamba ni jinsi gani vijana wa Gongo la Mboto na Kisarawe wenyewe wakawenza kupata fursa kubwa ambazo tutaongeza suala zima la uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kujielekeza katika suala zima la *Regional Development Budget*. Ndugu zangu naomba tutendewe usawa. Ukiangalia mikoa ambayo ipo nyuma tunazungumza Mikoa ya Pwani, Lindi na Singida. Lakini ukiangalia Bajeti Mkoa wa Lindi ndio imepewa Bajeti ya shilingi bilioni karibuni 20 inafuatwa na Mkoa wa Pwani kwa Bajeti ndogo ya shilingi bilioni 22 ya maendeleo kimkoa, baadaye Mkoa wa Singida. Jamani tusipojitalahidi kuhakikisha kwamba mikoa hii ambayo ipo nyuma tuweze kuiongezea juhudhi tutazidi kuiacha nyuma zaidi. Lazima tulielewe hili kwa dhati kabisa. Ndugu yangu Mheshimiwa Salum Barwany juzi alizungumza sana kwa uchungu Pwani, Lindi, Singida zote ziko nyuma. Tuwekewe Bajeti zake za mikoa angalau Bajeti yenye kuridhisha vile vile ili tuweze kuzisukuma mikoa hii iweze kupata changamoto kubwa sana ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza mengi lakini nitakuwa sijatenda mema kama sijazungumzia suala zima la kilimo. Napenda kuishukuru sana Serikali kwa kuwekeza kwenye suala zima la kilimo, kilimo maana yake kinaajiri kwa upana mkubwa zaidi. Akinamama na vijana watazidi kuimarika kwenye suala zima la kilimo. Kwa kweli

ningependa kuipongeza sana Serikali kwa kuona hili, lakini ili tuweze kuibua zaidi kuna mambo mengi sana ambayo kwa kweli hayajaweza kutumika.

Nimeshagongewa kengele ya kwanza, lakini sasa naomba kuzungumzia shukrani zangu kwa wale watu ambao wanaleta miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali hapa Tanzania. Nitakuwa sijatenda mema kama watu wanafanya shughuli nzito sana halafu unakosa kuuthamini mchango wao. Kwanza napenda kuwashukuru watu wa *ICAP* wameweza kutusaidia pale Kisarawe katika suala zima la hospitali yetu ya Wilaya na kituo cha afya cha Maneromango, naomba salamu hizi ziwafikie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kuapongeza ndugu zangu wa *Plan International*, wanatupelekea mradi wa shilingi milioni 250 kule kijiji Gwata kwa ajili ya mfumo wa maji. Hivi sasa wanasantaza maji katika Kijiji cha Kikwete na wanaeleke na harakati mbalimbali za ujenzi wa maji katika Wilaya yetu ya Kisarawe nauthamini sana mchango wao. *Ahead International* tunawashukuru sana kwa mchango wao, watu wa *IDB* na Mashirika ya Walemaru wote ambao wanafanya kazi Wilaya ya Kisarawe kwa kweli tunawathamini sana. (*Makofi*)

Mwisho ndugu zangu naomba tusisitize kwamba viongozi sisi tumebeba dhamana na kila kiongozi ataulizwa kwa haya madaraka tuliyokuwa nayo. Naomba tutende wema kwa raia zetu. Hapa usipoulizwa leo, utaulizwa kesho ambayo itakuwa ni siku nzito sana. Naomba tuwe na huruma, tusitumie madaraka yetu na midomo yetu vibaya kwa ajili ya kuiharibu nchi hii tutakuwa tumefanya kosa. Ndugu zangu tutakuwa tumefanya kosa na makosa haya tutakuja kuujutia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana sitaki nigongewe kengele kwa sababu ni busara ukipewa muda huo, tumia muda huo huo, ahsante kwa nafasi hii naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi jioni ya leo. Kwanza nianze tu kuapongeza wana Nkenge kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ajili ya kuleta maendeleo. Napenda pia nitoe salamu zao walizonitura kwamba tunapongeza Waziri Mkuu alipokuja kule kwetu wananchi walibarikiwa sana na ukizingatia alianzia Mkoa wa Kagera na hasa katika Jimbo la Nkenge. Sisi kumpokea kwetu tulikuwa na zaidi ya magari 60, ukizingatia kwamba yule ndiye mfalme wetu, ndie kiongozi wetu ninachotaka kusema kama hata angepokelewa na magari mawili, magazeti yote yangetangaza kwamba Waziri Mkuu ameenda Kagera amepokelewa na watu watatu. Kwa hiyo, nampongeza na naomba wananchi tulipo mikoani, viongozi wetu wakubwa wanapokuja tuinuke, tuwaonyeshe kwamba tunawapenda na tuwapokee na tuwe nao kwa wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikitembelea tu kata napokelewa na pikipiki 50, baiskeli 80, kwa hiyo, kuna ajabu gani Waziri Mkuu kupokelewa na magari hayo 50 kama sio *STK* ni kuonyesha kwamba tunampenda na tutaendelea kumpenda kwa sababu na ye ye analipenda Taifa letu. Nipende tu kuchangia sasa katika suala la kilimo. Katika Bajeti hii ukiangalia ongezeko la Bajeti katika kilimo limeongeza shilingi bilioni 2.5 tu

Lakini ukiangalia katika ongezeko la nishati utakuta ni asilimia 65 utakuta maji asilimia 56, ukienda elimu asilimia 12, afya asilimia 0.3 ukienda katika miundombinu asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niongee kidogo na nitakuwa tofauti labda na wachangiaji wengine kwa sababu watu wengi wameongelea sana habari za umeme. Wameongelea sana habari za miundombinu, lakini mimi naomba tu niongelee kilimo. Tanzania tumesema kabisa kwamba tunakwenda kwenye Kilimo Kwanza, lakini Bajeti yetu inaonyesha kilimo mwisho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize na sisemi wana Nkenge mbaki kwenye giza, lakini tangu nimekuja Bungeni simu za njaa zinazidi simu za kuniambia nihimiza umeme. Ningemba Serikali iangalie vizuri kwa mfano tunakubali umeme ni muhimu lakini kwa upande upi katika vijiji au mijini na viwandani? Kwa mfano, mtu anapokuwa kijijini tingesema watu wa vijijini tuongeze matrekta, watu wa vijijini tuongeze fedha kwa ajili ya umwagiliaji, hawa watu wakishiba wataweza kuweka nyaya za umeme na wataweza kulipia bili za umeme.

Mimi najiuliza hivi sasa nilikuwa napiga hesabu sikatai na watu wanapenda umeme, lakini wananchi katika kijiji changu wenye uwezo wa kulipia umeme si zaidi ya kaya tano au kumi. Lakini ukiangalia kilimo kama tungewawezesha wananchi hawa wakapata nyenzo za kilimo wakashiba, wakauza mazao yao na wao wanaweza kuja *stage* ya pili, wakaweza kulipia umeme ambao tunaulilia kuweka mpaka vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya kulipia umeme wanayo? Utaweka *transformer* lakini hawa wananchi waliopo huko vijijini wanaweza kununua umeme huo? Tunaomba tutofautishe maeneo ya viwanda na maeneo ya vijiji, *priorities* zinatofautiana. Mkulima wa kule Nkenge kijijini kwetu kule Kitobo hata kama hakuna umeme akawa ameshiba hawezi kukumbuka kwamba yuko katika matatizo ya umeme. *Primary* ni kilimo, ni chakula *second* ndio umwekee umeme *ata-switch on* umeme lakini jioni chakula hakuna? Mimi nilikuwa nashauri katika suala la kilimo kama kweli tumekusudia *priorities* zitofautiane mijini na vijijini. Kama wameshiba tukiwapa umeme kutakuwa hakuna tatizo wataweza kulipia hata huo umeme tunaopenda kuupeleka kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Napenda tu niipongeze Serikali imeweza kukusanya mpaka asilimia 93. Ukiangalia ninaona kwanza kuna bado upungufu tumepoteza katika malengo yao kukusanya shilingi bilioni 381. Nilikuwa napenda kushauri tu makusanyo mengi yanapatikana katika *TRA*, lakini *TRA* yetu ya sasa hivi ukiwa kweli ni mfanyakishara huwezi kuitisha mizigo yako katika bandari ya Dar es Salaam, utakuta mtu kama ameleta kontena, kontena kuja kulitoa linachukua wiki sita, miezi miwili huo mzigo hata *uli-estimate* kupata mapato yako yamepotea na matokeo yake kwamba kule kuzungushwa tu kunavunja watu moyo wa kuja kuwekeza katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofî*)

Mimi nilikuwa nashauri ni vyema tuweke *system* nzuri katika watu wa *TRA* namna gani tunaweza kukusanya ushuru kwa mfano, tungeweza kupunguza zile siku ungeshangaa kuona uchumi wetu unavyopanda katika nchi hii. Tungeweza kupunguza pesa kuwa nydingi tukaweka kodi kidogo ina maana tungekusanya nydingi na watu badala ya kupita Mombasa wangepita Dar es Salaam. Tungeongeza kipato hata shilingi bilioni 381 zisingepotea. Suala la gari nashangaa mtu mmoja anaagiza gari sawa sawa na mwingine lakini tukifuatilia utakuta malipo ni tofauti kwa kila mmoja ana ushuru wake ana *storage* yake kitu ambacho hakitoi *uniform*. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri watu wa *TRA* waangalie uwezekano wa kutoza *uniform* ili kusudi watu wote watendewe sawa kwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda kushauri kwa Serikali hii kodi ya kutoza vijiji shilingi 10,000/=. Sina uhakika vizuri kama litakwenda kufanyika kama lilivyokusudiwa. Ningependa itoe uoanisho kwamba ni nani wanastahili kulipa shilingi 10,000/=. ni nani wanastahili kutolipa ili kusudi mwisho wa siku sio mgambo ukakuta wamejiongezea kipato kuliko kusudio ambalo nchi imekusudia. Tumekusudia nini kusema shilingi 10,000/=. mwenye kioski au mbangaizaji au muangaikaji au wale wa mikononi. Kwa hiyo, ikleleweshwa vizuri hii tozo ya kodi ya shilingi 10,000/= inaweza ikaleta tija. Lakini bila hivyo unaweza ukashangaa kukuta kwamba hii shilingi 10,000/= inaleta mgongano na zaidi ya yote hatupati kile tulichokikusudia. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ongezeko ya tozo ya faini ya barabarani. Sina uhakika aliywaza kutoa hii shilingi 20,000/= kwenda shilingi 50,000/= alikuwa ana malengo gani. Kwanza hiyo, shilingi 20,000/= sina uhakika kama yote ilikuwa inakwenda kwa Serikali. Nina uhakika hiki kitendo cha kuongeza shilingi 20,000/= tumeongeza ulaji kwa askari. Mtu kuona aende kulipa shilingi 20,000/= bora akamlipe askari shilingi 10,000/= aende zake nyumbani na halafu askari aweke mfukoni biashara imeishia pale. Kama tungetaka watu wote walipe mimi nashauri ingepungua ungeona kila mtu anakimbilia kulipa ili kusudi aweze kuongezea kipato kuliko shilingi 50,000/= iliyowekwa. Uaminifu huo askari wameutoa wapi wa kupeleka shilingi 50,000/= katika Serikali, sina uhakika huo hata kidogo na kweli tendo la kuweka shilingi 50,000/= ni kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye jambo lingine la Benki ya Wanawake kuhusu mikopo. Hapa tulipokuwa na sera ya kuweka Benki ya Wanawake nia ya Serikali ilikuwa inataka wanawake wakombolewe wale wa chini. Lakini nataka niseme hii Benki imekuwa sawasawa na Benki zingine haina tofauti na Benki nydingine, kwa nini nasema hivyo. Nimejaribu kwenda pale kuomba mkopo kwa ajili ya wanawake wa Misenyi matokeo yake niliyoambiwa ni kwamba tulete hati, kitu ambacho hata *CRDB* inakifanya. Kwa hiyo, nimetafuta tofauti ya Benki ya Wanawake na Benki ya *CRDB* nimeikosa.

Naishauri Serikali itusaidie kuweka mazingira ya tofauti ili kusudi wanawake wengi wapate mikopo kutoka katika Benki hii. Tafadhalii, tafadhalii wanawake wengi tunawatangazia tunapokwenda huko kwenye kampeni, kwenye kuwakusanya wanawake kuna Benki yetu ya Wanawake, lakini mwisho habari yote imeishia Dar es Salaam wala

haijaenda katika hatua zingine. Nashauri Serikali itusaidie ili wanawake waweze kujikwamua kutoka umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuishauri Serikali ni kuhusiana na vijana na nitaendelea kusema kuwa vijana wanaweza kusaidiwa kama kweli, narudia tena kama kweli tutaweka mazingira mazuri ya kuwatia moyo ili waweze kuipenda nchi yao na kujitolea kwao. Hivyo ninachoomba kama tunaweza hata kwenye Halmashauri. Mimi siku moja nilikwenda kutembelea vijana, nilipowaita nilikwenda na Afisa Utamaduni tunafika pale wanasema kwamba vijana hamuombi hela na hela tumerudisha. Kijana hajui kama kuna hela yoyote inayomhusu kijana matokeo yake hela ilirudishwa na vijana hawajakopeshwa. Hivyo naomba Afisa Utamaduni basi wapewe mikakati ni nini cha kufanya ili kusudi vijana wapate kujua kwamba kuna fedha zao pale kwa ajili ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa naomba kusisitiza katika suala la elimu tunachukua pesa hizi tunawakopesha vijana wa Chuo Kikuu. Lakini ni namna gani tunaweza kurudisha zile pesa na ni namna gani tunawa-*committ* mfano kwetu tuliletewa walimu watano, wengine wameripoti wakamaliza kuripoti wakachukua pesa zao wakarudi Dar es Salaam. Lakini je, wakati ule wanachukua fomu hatuwezi kuweka kipengele cha kum-*commit* mwanafunzi kwamba utakapokuwa umeingia Chuo Kikuu na tumekukopeshwa angalau miaka mitano tukikupeleka Singida uende kwa ajili ya kuanza *at least* tuone namna gani wanaweza kutumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ametangaza wakati wa Kampeni kwamba kuna walimu wengi watamaliza na atawagawa katika kila jimbo alipopita, lakini hawa walimu hawajaonekana, wamefika wamerudi matokeo yake Serikali inaonekana hajili na haileti walimu. Mimi nashauri *commitment* kwa mwanafunzi kabla hajachukua mkopo ajisajili pale kwamba mimi nitakubali kwenda popote ambapo Serikali itanipeleka angalau kwa miaka mitano tuweze kuona kwamba yale tunayoyasema tunayafanya yaweze kuonekana yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kugongewa kengele, nabaki nikisema kwamba vijana wakijidanganya, nakumbuka Mheshimiwa Mwakyembe siku moja alisema enzi zile za Mwalimu kuna watu walifutwa kabisa Chuo Kikuu. Hivi kila siku wanafunzi wanagoma na kuna mtu anatetea tu, lakini unatetea nini mtu amevunja sheria, anagoma na eti tuwaache, hata nyumbani mtoto akikosa anapata kiboko na hao watoto wakumbuke kwamba wao hawako juu ya sheria. Kama wakicheza tunaweza wakafutwa wakapelekwa watu wengine. Wale walioko vijijini wamekosa nini kutokuwepo *UDOM* hawajakosa chochote yamkini wengine walikuwa na uwezo wa akili kuliko waliopo pale, lakini wao wamefika pale wanachezea nafasi ile.

Mimi nashauri wajue kwamba kuna siku wanaweza kufutwa na mtetezi aliowatetea asionekane na aliowachochea asionekane kuwasaidia. Bora wao waelewe ni kitu gani cha kufanya na kwa nini wapo vyuoni na wengine wako nyumbani na hawajapata nafasi ya kwenda vyuo hivyo. Ni hayo tu nachangia Mungu awabariki sana naunga hoja mkono nikizingatia kwamba kilimo kitapewa nafasi ya kwanza. (*Makofi*)

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nataka nikupongeze wewe na Wenyeviti wenzio kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Pili, nataka nimpongeze sana kaka yangu Waziri wa Fedha kwa Bajeti nzuri aliooleta safari hii kwani inatia hamasa kiasi ambacho hata nikifika kule kijijini wananchi wanajua tutafanya nini. (*Makofi*)

Vilevile nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wamechangia kwa hali na mali wameonyesha ukakamavu mkubwa sana kwenye Bajeti hii ya Fedha na mimi nasema kama Mwenyekiti wa timu ya Wabunge nakuhakikishia ndugu yangu Mheshimiwa Mkulo Bajeti hii itapita bila ya matatizo aina yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka niwashukuru timu ya Bunge kwa kazi nzuri waliyoifanya juzi. Ndugu yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia, ahsante sana tuendeleze hivyo hivyo ili timu ya Bunge iwe inaheshimika. (*Makofi*)

Mimi sitakuwa nje sana na wenzangu, wenzangu wamechangia vizuri sana na bahati nzuri Bajeti hii imeleta msimamo na msisimko kwa wanaviji. Ninachoomba tu kuwaeleza Bajeti hii iende kwa walengwa. Nimesema hivyo kwa sababu kuna Mheshimiwa amechangia hapa akitaja kwamba kuna sehemu mikoa maskini sana. Lakini nataka niseme kwamba kuna sehemu Wilaya ni maskini sana pamoja na kwamba wana haki na wana mali, lakini mali zile hawawezi kuzipeleka sehemu yoyote kwa sababu kwanza miundombinu ya kusafirisha mazao imekuwa ni migumu, kwa mfano kwenye jimbo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona kwamba Bajeti tunazipitisha tena kwa vishindo, lakini tunashindwa kutengeneza barabara ya kutoka Gombero kuja Makorola, mtu anatengeneza barabara ya kwenda kwa Babu Loliondo, inasikitisha sana! Ningombwa sasa hivi Serikali iangalie sana yale mambo ya kwenda tu, kama watu wa kutengenezewa barabara basi mngenitengenezea mimi Maji Marefu kwa sababu muda mwingi sana nimeifanya mazuri na nina jina kubwa Tanzania na nje ya nchi, lakini mtu anatokea leo Serikali inakwenda inampeleke mabilioni ya pesa wakati wananchi wa Tanzania tunakwama, hivi vitu naomba iwe mwisho sasa. Muangalie zile sehemu zenye kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu kuna matatizo makubwa sana, wananchi wangu wanalima sana, lakini ni mahali gani pa kupeleka mazao yao. Barabara hakuna, maji hakuna, kitu kibaya zaidi ni kwamba kwenye Jimbo langu mimi ndiyo kunakotoka umeme mkubwa sana, lakini utashangaa umeme huo kwangu hauna kazi, unafanya kazi kwenye mikoa mingine. (*Makofi*)

Naiomba Serikali iangalie, kwa mfano kwangu umeme mkubwa unatoka Hale, lakini Shamba Kaporu hakuna umeme, Kwa Mziwanda hakuna umeme, Mkwakwani hakuna umeme na ni karibu, lakini umeme huo utashangaa upo Morogoro, utashangaa uko Mikoa ya jirani, lakini Dindila hakuna umeme, Vugiri hakuna umeme, Makumba hakuna umeme, lakini hapa tunakuja tuna-support sana vitu, cha kushangaza pesa

zinatolewa nyingi na pesa hizi zinakwenda kwa walengwa, lakini pesa hizi zinaletwa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inafika kwangu tumetengewa pesa zinaletwa mwezi wa tano, mwezi wa sita unaambiwa zinatakiwa zirudi Hazina. Lakini ukiangalia Hazina zinachokuja kufanya ni siku tumepitisha Bajeti unakuta Wizara zinafanya sherehe. Hii inakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizo si afadhali kama Serikali ingepanga mpango mzuri kwamba zile pesa zinazoletwa siku za mwisho mwisho kwenye Wilaya ambazo zina matatizo zifanye kazi, wapelekewe vielelezo kwamba wamefanya hivi, lakini unaletewa pesa mwezi wa tano kwenye Wilaya yako kwamba ipelekwe ikajenge shule au ipelekwe kwenye hospitali, leo hii unaambiwa irudi tena Hazina, ukija huku inapangiwa sherehe, mikutano ya hadhara, semina inahusiana na nini, wakati Magunga kwenye hospitali ambayo inahudumia Mikoa mitatu ya Tanzania sasa hivi watu wanalala chini, hakuna hata wodi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi imeniumiza kidogo, lakini ninafurahishwa na hii Bajeti ya safari hii, lakini isije kuwa Bajeti ya kuonesha tu kwa vidole kwamba tumeipitisha, tunaipitisha na ninaiunga mkono mia kwa mia, lakini muangalie Jimbo langu.

Jimbo langu mimi halina maji, halina mawasiliano, sasa hizi Bajeti tunazopitisha zinaenda mikoa gani au kuna Wilaya na Mikoa ambayo inaonekana ni mizuri zaidi na kuna zingine zinaonekana siyo nzuri zaidi? Naomba Serikali ituangalie na sisi watu wa Korogwe Vijijini kwa sababu inanisikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kwangu ya kutoka Mgombezi kwenda Mswaha imeshindikana, lakini Samunge imetengenezwa tena kwa muda mfupi! Nimekwenda Muhimbili wagonjwa wamerundikana waliojifungua lakini watu wamekwenda kufanya utafiti wa shilingi milioni 34 kwa ajili ya dawa ya Babu? Kwa nini msifanye utafiti wa dawa ya Maji Marefu kama kweli ninyi mnataka kuwasaidia watu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu amekuja juzi amejitangaza tu, kwa sababu ni imani basi watu wanaiona imani hiyo, wakati Hospitali ya Mombo hata jenereta ilikuwa inawashinda watu, kwa nini hizo shilingi milioni 34 msizipeleke jenereta katika Hospitali ambazo zina shida? Kwa nini hizo shilingi milioni 34 zisiende kufanya kazi ambazo zinahusiana na wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwenye Jimbo langu kuna njaa, watu watakula nini? Naomba Serikali ijue hivyo kwamba kwenye Jimbo langu nimeingiliwa na njaa ambayo haina kifani. Wale wanaokula mazao wamekula, Kata ya Kerenge, Magoma, Makuyuni, Mkomazi, Mazinde mpaka Kizala wananchi wangu wapo nje, njaa imeingia kule. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie hili ikiwezekana hata kesho mnisaidie. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuige nchi za wenzetu, Serikali ya Kenya Bajeti ya wanafunzi wale wanaosoma wanapelekewa mwezi wa kwanza, ukiingia tu unapewa cha kwako kabisa, lakini cha kushangaza Tanzania leo wamepelekewa shilingi bilioni mbili, kesho shilingi bilioni tatu matokeo yake wanafunzi wanaandamana, tena tukija hapa tunaanza kushikana mashati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu Wapinzani, leo hakuna kibaya ambacho ninyi hamjaacha kukisema, lakini Rais Kikwete amefanya mazuri sana. Utashangaa kwenye Majimbo ya CCM Rais Kikwete hajafanya chochote, lakini kwenye Majimbo mengine amefanya mazuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mtu anakuja anadiriki kusema kwamba posho isitolewe, lakini kwenye Mashirika ya Umma kule tayari ameshajijengea, ukinikatalia mimi ninakufanya hiki, anapelekewa kisiri siri kule akija huku anasema Wabunge wasipewe posho, sasa hii tuangalie mimi nina majina hapa kabisa watu wanaosaini na kuchukua pesa na wakija huku kwetu wanajifanya wao waonekane wazuri sana kwa mazingira ya kujitengenezea umaarufu. Kama ni umaarufu hapa hakuna mtu maarufu kuliko Maji Marefu, maana nimetembea nchi zote za dunia sasa ndiyo umaarufu? Na mwenzangu Nkamia hapa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa mtu unakuja kujipa umaarufu hapa wakati wapiga kura wako wanakosa mahali pa kutembelea, wakati kule Jimbo lako watu wanalala chini, leo hii hapa nijipe umaarufu wakati soko ambalo linalisha Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Kilimanjaro halina hata choo! Soko la kwa Shemshi na Magoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali hapa inatutengea pesa, hata kujenga choo ambacho mazao yanapatikana kwa wingi watu wameshindwa. Sasa naomba Mheshimiwa Mkulo safari hii Serikali iangalie kule, maana umetoa Bajeti ambayo mimi nimefurahishwa sana, kiasi ambacho nimeiona kwamba Bajeti hii ni nzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kitengo cha maji, maji ni kero kubwa sana, wananchi wetu wa Korogwe wanapata shida sana ya maji. Maji yanayonyewa pale Korogwe ndiyo haya kama tunayotumia hapa yalishanawiwa hapa wakati tukitaka kula chakula hapa kantini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niwahakikishie wananchi na ninawahakikishia Wabunge wenzangu kwamba tuiunge mkono Bajeti hii, lakini na wenzetu Mawaziri ni wachache sana ambao wanapokea simu wakati kukiwa na kero, tusipendezane wakati huu wa Bajeti, tupendezane hata tukiwa huko mitaani wakati inatokea kero kwa Mbunge wa Jimbo lolote Tanzania, tukiwapigia simu mpokee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo moja kubwa sana, kuna baadhi ya wenzetu mkishapitishiwa Bajeti simu zote mnaziweka *off*, sasa tunaona namba kwenye vitabu, kunakuwa kuna kero kubwa ambayo unaweza si kunisaidia kwa pesa, unaweza kunisaidia kwa mawazo tunafanya nini, mnakuwa hampatikani, sasa mnataka nikalie kwa nani? Kila kitu tuende kwa Waziri Mkuu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vya namna hii ni lazima tuviangalie kwa sababu hili mimi hapa nimelileta lakini nimetumwa na wananchi, ninapotumwa na wananchi natakiwa niwasaide kero zao. Wale wanaokataa posho naomba wazipeleke kwenye hospitali yangu ya pale Magunga nitawashukuru sana kwa sababu nina shida sana pale hospitalini, nataka njengewe ofisi ambayo itaweza kunisaidia Wagonjwa wanaotoka kule kwa ndugu yangu Rombo na wanaotoka Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Tanga wale wanaopata ajali pawepo na kitengo maalum pale kwa ajili ya kuwasaidia. Ni hospitali kubwa lakini haina vifaa na haina mahali pa kusaidiwa, kwa hiyo wale wanaokataa posho wote naomba basi wazipeleke kwenye Jimbo langu, nina hospitali pale ambayo inahudumia, ingepata hadhi ile ingesaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache naendelea kuunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha, ahsante sana. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mzungumzaji aliyekaa anazungumza, ametamka kwamba Wajumbe wanaotoka kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma wakirudi hapa wanasema hatutaki posho na majina anayo, je, anaweza akalithibitishia Bunge hili kwamba usemi anaoutamka ni wa kweli au anataka kuwapaka Wajumbe hao wa Kamati mambo ambayo siyo ya kweli? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo nitautolea taarifa baadaye, naomba tuendelee. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae na Mheshimiwa David Kafulila atafuatia.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ambayo nilikuwa naisubiri kwa hamu kubwa sana. Kabla sijatoa mchango wangu niseme tu kwamba naunga mkono pongezi zote ambazo zimekwishatolewa humu ndani kwa viongozi, Wabunge na wote ambaao wamepewa nyadhifa mbalimbali katika Bunge letu na katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naunga mkono hotuba iliyosomwa hapa na Msemaji wetu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara yetu ya Fedha na kwa sababu hiyo naomba ninukuu sehemu ya hiyo hotuba ambayo pia itaniongoza katika mchango wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Msemaji Rasmi wa Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Fedha ukurasa wa tatu, alimnukuu mwanasiasa maarufu Marehemu Mahatma Ghandi aliyesema kwamba mabadiliko ya kidemokrasia hayawezekani iwapo hatupo tayari kusikiliza upande mwingine, tunafunga milango ya kufikiri wakati tunapokataa kusikiliza wapinzani wetu au baada ya kuwasikiliza tunawafanya mzaha. Kutovumiliana kunapokuwa ndiyo mazoea, tunajiweka katika hatari ya kutojua ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nikumbushe tu kwamba tarehe 11 Juni, 1991 tulipoanzisha Mageuzi pale *Diamond Jubilee*, tulitengeneza kitabu kwa wale wanaokumbuka kinachosema Upinzani siyo uadui na kwamba tutapingana bila kupigana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba yapo mawazo mazuri ambayo tumeyasikia katika hotuba ya Kambi ya Upinzani na mambo haya ni kwa mfano, wazo la kuongeza mapato ya Serikali. Kwa sababu kimsingi ni kwamba yote tunayotamani kuyafanya katika nchi yetu yanategemea fedha na yale ambayo tunashindwa kuyafanya hatuyafanyi kutokana na umaskini wetu. Kwa hiyo, wazo la kuongeza mapato ya Serikali ni wazo zuri nadhani Serikali inao wajibu wa kusikiliza mawazo ambayo yanatolewa, kuyafanya uchambuzi na kuangalia yale yanayoteklezeka kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo mojawapo ambalo limetolewa na Kambi ya Upinzani ni kuhusu kuongeza mapato kwa kuimrisha utalii wetu wa ndani na nje, hili ni wazo zuri, kwa sababu viro vivutio vingi sana vya utalii vya hapa ndani, sisi Watanzania hatuvijui na hamasa kwa Watanzania ili wavijue na viwe chanzo cha mapato kwani nchi yetu imekuwa ndogo sana. Hali kadhalika vyanzo hivyo vinaweza vikatumika kwa ajili ya uhamasishaji na vikawa vivutio vipyta kwa ajili ya wenzetu wanaotoka nje na tukapata mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna wazo ambalo limekuwa likizungumzwa hapa Bungeni kuhusu kutumia fursa ya kijiografia ya nchi yetu, ili tuweze kukuza uchumi wetu. Hili ni wazo zuri sana lakini sasa utekelezaji wake unasuasua mno. Nasema hili nikiunganisha na hilo nililosema awali la utalii, nikitoa mfano kwamba hivi sasa wenzetu wa Kenya wana mpango wa kutengeneza uwanja mkubwa sana wa ndege pale Holili jirani na Jimbo la Rombo na kama uwanja huo utatengenezwa utaua kwa vyovyote vile uwanja wetu wa ndege wa Kilimanjaro, na matokeo yake watalii na faida ya utalii kwa wale ambao tunajua ni kwamba unatokana zaidi na zile *ticket* ambazo watalii wanakuwa wameshalipia kutoka kwao huko wakija huku, ni kitu kidogo sana wanatuachia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali twende mbio zaidi kwa sababu kama hatutawezza kuutumia vizuri ule uwanja wetu wa ndege, ukavuta wasafirishaji na wasafiri wakauamini, matokeo yake ni kwamba huu utakapojengwa na watu wa Kenya wana haraka sana katika kutekeleza mambo yao. Kwa mfano sasa hivi tupo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukienda pale Holili na nimekwenda safari hii wakati tulipotoka hapa

Bungeni, upande wa Tanzania ukiangalia Ofisi zetu za *TRA*, ofisi za *Immigration* ni aibu, lakini ukiangalia kwa wenzetu wa Kenya wana majengo mazuri, yana kamera nzuri zinazoangalia wanaoingia na wanaotoka na kwa sababu hiyo sisi kila mara tunakuwa na mawazo mazuri lakini utekelezaji unakuwa ni wa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri hili ni wazo zuri lakini sambamba na haya, kwa upande wetu Serikali imekuja na wazo la kuongeza nguvu katika uzalishaji wa umeme, nasema ni wazo zuri kwa sababu katika kipindi chote ambacho nimekaa katika siasa za mageuzi tumekuwa tukizungumza hayo, tumekuwa tukihimiza umeme wa kutosha, tukihimiza maji, tukihimiza kilimo bora, tukihimiza elimu bora, tukihimiza utawala bora na sasa Serikali imekuja na hayo. Sasa sioni sababu yoyote ya kutoona kwamba haya ni mawazo mazuri kama yatatekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hoja ya umeme; sisi watu wa Rombo tunashida sana ya umeme kuliko watu wengine wanavyofikiria. Umeme wa Rombo unatoka *TPC Kiyungi* unakwenda Bomang'ombe unakuja Moshi ndiyo unakuja kwetu Rombo, kwa hiyo, hitilafu yoyote Moshi, hitilafu yoyote Himo, Marangu inasababisha sisi Rombo iwe ni giza. Tunaweza tukakaa hata wiki nzima bila kupata umeme, kwa hiyo, mimi wakati nikishukuru wazo hili naomba sana rafiki yangu Waziri Mheshimiwa William Ngeleja aangalie sana kilio cha watu wa Rombo kuhusu umeme. Nadhani ni jambo linalowezekana kwa sababu nilishasikia kwamba kuna tetesi za kazi fulani ambayo itafanyika pale, mimi naomba ifanyike ili watu wa Rombo na wenyewe waweze kujisikia kwamba Serikali imewaangalia na kuweza kusaidia wale wafanyabiashara ndogo ndogo na wale wazalishaji wadogo wadogo amba wanategemea umeme katika shughuli zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala limezungumzwa hapa la maji, naomba nilunganishe na suala la kilimo, watu wa Rombo siyo wavivu, wanateseka sana katika kilimo, lakini kwa heshima tu nikuambie Rombo huu ni mwaka wa tano tunapewa chakula cha msaada. Hata leo ninavyozungumza watu huko wanagawana mahindi ya msaada yaliyopelekwa na Serikali tani 500, si kwa sababu sisi tu wavivu, ni kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi. Wanalima wakishalima ukame unakuja, chakula kinaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Halmashauri ilishaleta Serikalini mpango wa kujenga malambo katika mito ya Msimu Saba, nadhani Serikali ilishapokea huo mpango. Katika Bajeti iliyotolewa ya umwagiliaji, Serikali ione uwezekano wa kusaidia watu wa Rombo fedha walizoomba ili kujenga malambo hayo ambayo yatawasaidia katika kilimo cha umwagiliaji lakini hali kadhalika yatawasaidia katika maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani suala la elimu lilijadiliwa na mawazo ni kwamba ikiwezekana Serikali ifikirie kuondoa ada katika shule za sekondari za Kata au ikishindikana walau izipunguze nusu kwa watoto wa kike. Naomba niongezee kwamba kama ikishindikana mawazo yote mawili basi Serikali ione uwezekano wa kufuta ada kwa watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto yatima wanaongezeka katika nchi yetu kila mahali. Katika jimbo langu ni wengi sana. Sasa ningeiomba Serikali iangalie uwezekano au kuwafutia hawa watoto ada moja kwa moja au kuzihamasisha Halmashauri au kuzihimiza Halmashauri ziweze kuweka mpango wa kusomesha watoto yatima katika Bajeti zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nilitaka kuongea kuhusu utawala bora. Sasa hivi kukiwa na shida ya njaa katika Jimbo la Rombo, malori yanapita yakisafirisha mahindi kupeleka Kenya kwa siku zaidi ya malori 70. Haya malori sasa imekuwa ni mtaji kati ya *TRA* na polisi. Wanawazuia katika Mji Mdogo wa Himo. Kila lori ili lipite ni shilingi 50,000. Hiki kilio nimeshakipeleka kwenye Serikali ya Wilaya hata kwenye Serikali ya Mkoa wanajua. Sasa wafanyabiashara hawapeleki mahindi katika masoko ya Rombo kwa sababu wanazuiwa Himo matokeo yake mahindi yote yanasantikizwa, yanavuka mpaka yanakwenda Kenya. Sasa ni rushwa inayotolewa wazi wazi kila mtu anaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na kwamba kuna biashara huria lakini basi Serikali ione kwamba hili ni jambo ambalo huko tunakokwenda litaongeza tatizo la njaa katika nchi na hususan katika eneo ambalo nimelitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kulizungumza ni hizi kodi ambazo zimerejeshwa, leseni za biashara katika vijiji shilingi 10,000/=. Nasema hilo kwa sababu sasa hivi kuna hizi pikipiki zinaitwa bodaboda karibu katika kila sehemu. Sasa sijui maeneo mengine lakini kule Rombo ni mapambano kati ya bodaboda pamoja na *TRA* na polisi, maana pikipiki inatozwa kodi mpaka shilingi 90,000/= sasa matokeo yake ni kwamba hao vijana wanawakimbia polisi ajali zinakuwa nyingi na kadhalika. Mimi ningeiomba sana Wizara iangalie hizi kodi za pikipiki kama zinaweza zikapunguzwa kwa sababu ni njia pia ya kuwasaidia hawa vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningefikiria kwamba ikiwezekana hata Wizara ya Mambo ya Ndani itoe tamko fulani maana ikijulikana tu una pikipiki hata kama ni pikipiki kwa ajili ya kutafutia maji maana yake kule Rombo mtu anachukua pikipiki anakwenda Kenya kufuata maji basi lazima polisi watakukamata au wataifuata ile polisi imepaki nyumbani usiku wataifuata ile pikipiki, watakutoza faini, wataipeleka kituo cha polisi na kadhalika. Sasa huku ni kuleta chuki kati ya wananchi na Serikali. Mambo kama haya ni mambo tusipoyaangalia yanaweza yakatuletea matatizo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme tu kwamba ipo haja ya kuvumiliana kwa sababu kama tulivyosema mwanzo tunajenga nchi na tuko hapa wote, hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siyo Bunge la Chama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kabla sijamaliza hotuba yangu niwapongeza Wabunge leo, walau Taarifa na Miongozo imekuwa michache sana. Tujisikie kwamba kutotumia huu muda vizuri maana yake huu muda ni muda wa wananchi, ni aina fulani pia ya ufisadi kwa sababu tuko hapa kwa ajili ya kufanya kazi za

wananchi. Sasa pande zote mbili tunapotoa Mwongozo, Taarifa matokeo yake hatufanyi kazi tulizokusudia inakuwa ni matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ahsante. (*Makofi*)

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia jioni hii ya leo. Kwanza kabisa niungane na wenzangu vile vile kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anatuwezesha kuwa wazima na kulitumikia Taifa letu kupitia Bunge letu tukufu. Lakini vile vile kwa sababu nasimama kwa mara ya kwanza nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Manyara na wananchi wote kwa ujumla kwa imani yao kubwa kwangu na mimi ninawaahidi nitaendelea kuwatumikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa Bajeti nzuri, imesemewa vizuri sana na mimi nikiwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ninaelewa kabisa jinsi ambavyo hii Bajeti yetu ni ya kihistoria. Ni Bajeti ambayo ni *realistic* na hivyo nawaomba Watanzania wote tutimize wajibu wetu kuitekeleza kwa ajili ya maendeleo yetu wenyewe kwa kukuza uchumi na ajira ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na sekta ya kilimo. Mengi yamezungumzwa kwa ubora wa kulenga kilimo na mimi naunga mkono kabisa kuweka kipaumbele katika sekta ya kilimo. Lakini naomba kutoa masikitiko yangu katika eneo dogo sana katika kitabu hiki cha Bajeti kuanzia ukurasa wa 11 kwa upande wa mazao. Tanzania ina mabonde mazuri yenye rutuba, kwenye kilimo cha mpunga katika Mikoa ya Tabora, Mwanza, Shinyanga, Kigoma, Pwani, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga na Morogoro chini ya utaratibu huu wakulima wadogo wadogo watawezesha kupata huduma za mikopo, ugani, mbegu bora na mbolea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyejua umuhimu na ubora wa mchele wa Magugu. Ninasikitika kuona kwamba bonde la Magugu ambalo linatoa mchele mzuri sana ambao unapendwa na Watanzania wengi na hata nje ya nchi hawakuweza kufikiria katika utaratibu huu. Naomba kama hii ni *error* au ni *deliberate* naomba irekebishwe ili na wakulima wetu wadogo wa Magugu Mkoani Manyara huko Babati waweze kunufaika na utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika pia kuona kwamba uchumi wetu unaelekea kwenye viwanda kwa maana tunapozalisha zaidi tutakuwa na malighafi na tunaweza kuanzisha viwanda vyta kusindika mazao na kwa hiyo, naipongeza Serikali katika hatua hiyo. Tunajua kwamba nchi yoyote yenye uchumi unaotegemea kilimo ndio kigezo kabisa cha kuona kwamba nchi hiyo ni maskini na kwa hiyo, nadhani Bajeti hii na mipango yetu tuliyoweka imeonyesha dira na mikakati mizuri ya kuweza sasa kuijandaa kutoka kwenye uchumi unaotegemea kilimo kuelekea kwenye viwanda. Kwa hiyo, naipongeza Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu *Southern Agricultural Corridor*, mimi pia napongeza mpango huo, lakini nina wasiwasi kidogo unatokana

kwamba mpango huo wa *Southern Agricultural Corridor* umekuwa *heavily supported* na *external support*. Sasa nina wasiwasi kwamba ule usaidizi kutoka nje utakapopungua *sustainability* au uendelevu wa mpango huu unaweza ukaathirika. Kwa hiyo, naishauri Serikali wahimize zaidi wawekezaji wa ndani ili waweze ku-*support* mpango huu ili uweze kuwa endelevu. (*Makofi*)

Vile vile nilikuwa naiomba Serikali kwamba sambamba na kuboresha uzalishaji au kuhimiza uzalishaji wa mazao kule Kusini naomba sasa umaana huo huo uweze kuanzisha viwanda kule Kaskazini kuwe na *Northern Industrial Corridor* ili kuweza kuchukua mazao yale na kuweza kuanzisha viwanda vyta kusindika huko Kaskazini ili kwa pamoja nchi yetu iweze kukuza uchumi kwa pamoja na tuweze kuendelea pia kukuza ajira. Naambiwa na *Central* vile vile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwamba Watanzania tunaanza kusonga mbele na tujizatiti kabisa kama kila mtu atatimiza wajibu wake, nadhani tutapiga hatua kubwa sana katika kuendeleza nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kidogo kuhusu migogoro ya mashamba ya wawekezaji. Naiomba Serikali ione hili na iipe kipaumbele. Natoa mifano migogoro ilianza kule *NAFCO* Wilaya ya Hanang kwa maana ya kwamba wafugaji walianza kuwafukuza wawekezaji kutokana na kuhitaji ardhi yao ya asili. Kule Vilima Vitatu wafugaji walitaka ku-*claim* ardhi yao kwa kuona sasa wanahitaji lile eneo. Bonde la Kiru kule Babati hali kadhalika kuna mauaji kwa wananchi kuona kwamba wanahitaji lile eneo na maeneo mengi ya migodi. Hili linatufundisha mambo makubwa mawili, la kwanza inadhihirisha wazi kabisa kwamba *population* yetu inaongezeka lakini ardhi inabaki pale pale. La pili uelewa wa wananchi unaongezeka kwa mahitaji ya kujiendeleza na kwa hiyo, ku-*reclaim* lile eneo lao lililopewa mwekezaji. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali kwamba inapowaruhusu wawekezaji hapa nchini iweze kuweka vigezo kwamba wawekezaji wakae kwa muda fulani ili kuruhusu *population* inayoongezeka ya nchi yetu waweze na wenyewe kunufaika na ardhi ile na hata niktoa mfano kule Kiteto ardhi bado ipo kubwa, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri anaelewa hilo na wengi wanakimbilia eneo lile kutafuta mashamba. Nina hakika baada ya miaka kama mitano inaweza ikazuka vita sasa kwani wananchi wale uelewa utaongezeka, *population* imeongezeka wataanza ku-*reclaim* ardhi yao. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali inapowekeza pia iweze kuwafikiria wananchi na wenyewe waweze kunufaika baada ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kidogo uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Naunga mkono utaratibu wa *SACCOS* na *VICOBA* vile vile naunga mkono taasisi na mifuko mbalimbali ambayo inatoa mikopo kwa wananchi wetu ili kuondoa umaskini. Lakini mikopo maana yake ni fedha unazompa mtu ukitarajia atarejesha. Sasa kuna maeneo ya nchi yetu na jamii mbalimbali ambayo kusema kweli hawakopesheki. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikafanya utafiti pengine hata utakuta mikopo ama kuanzishiwa *SACCOS* siyo *priority*. Kwa sababu kama mtu ana njaa kwa mfano ama hana afya njema, ama kuna tatizo kubwa la maji, hawezi akachukua ule mkopo akafanya biashara kwa ufanisi kwanza hana elimu ya biashara. Kama alivyosema Mbunge mmoja

hana, hawana hata elimu ya ujasiriamali na hivyo biashara kwao ni kama historia. Kwa hiyo, nashauri Serikali kwamba popote pale inapoanzisha utaratibu fulani wa kuondoa umaskini uweze kufanya utafiti kuona ni nini (*immediately needs*) za jamii ile mahitaji ya dharura ili iweze kuwasaidia na wenyewe wakaondokana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu suala zima la migomo na maandamano. Mimi nawakilisha Bunge kwenye Baraza la Chuo Kikuu cha Mzumbe, na kwa hiyo, naomba kuchukua nafasi hii kuupongeza uongozi wa Chuo Kikuu Mzumbe nadhani wote hamjawahi kusikia Chuo Kikuu cha Mzumbe kimegoma ama kuandamana. Mara nyingi ni rahisi sana kuona mabaya yale yanayoonekana na kuyasemea. Lakini yale mazuri tunayasahau.

Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikatambua hilo si kwamba wale hawana matatizo, wana matatizo makubwa pengine kuliko hata *UDOM*. Lakini uongozi bora uliopo pale chini ya Mkuu wa Chuo Jaji Mstaafu Barnabas Samatta pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo wenyewe wanatumia *dialogue* na Baraza la Wanafunzi. Kwa hiyo, nadhani suluhisho siyo migomo na migogoro na maandamano. Chuo hicho kimeweza kuonyesha mfano na ni dhahiri kwamba ni vizuri hata Serikali ikakipongeza chuo hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu masuala ya riba ya benki. Tunapoweka fedha zetu benki na ni hamasa kwa wananchi wote kuanza kuweka *focus* yao kuweka fedha benki kwa sababu tunahimiza mikopo, tunahimiza *SACCOS*, tunahimiza *VICOBA* vyote hivi vinahitaji kuweka fedha benki. Lakini tunapoweka fedha benki asilimia inayowekwa kwenye riba ya *savings* ni kidogo sana. Hili limezungumziwa sana kwenye taarifa yetu ya kamati lakini naomba kuweka msisitizo kwamba ukichukua mkopo benki wewe unawekewa asilimia 16 hadi 20 ya riba. Lakini wewe unaweka milioni zako nyingi tu benki *savings* unawekewa *interest* ya asilimia 0.5 kitu kama hicho. Sasa naiomba Serikali na taasisi za fedha ziweze kufikiria sasa ili hata iwe hamasa ya kuwafanya wananchi waweke fedha benki iweze kuongeza riba ya kwenye amana ya *savings* za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeandaa haya machache na nimechangia kwa ufupi. Naendelea kuipongeza Serikali kwa Bajeti nzuri. Ahsante sana na naiunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi niseme kwamba nawashukuru Wananchi wa Kigoma Kusini kwa uamuzi ambao waliufanya na leo hii nimesimama mbele yako kwa ajili ya kujadili hotuba ya kwanza ya Bajeti tangu nikiwa Mbunge. Ni heshima kubwa ambayo mmenipa ambayo itanifanya niendelee kuwashukuru kila ninapojadili hotuba ya Bajeti. (*Makofi*)

Baada ya kupitia hotuba hii ya Bajeti na pengine kabla sijaanza kuzungumzia kipengele hadi kipengele napenda kusema kwamba nashukuru walau katika Bajeti hii Jimbo la Kigoma Kusini limekumbukwa kwa kiasi kwamba kuna barabara ya lami ambayo haikuwepo tangu historia, kuna Daraja la Maragalasi ambalo halikuwepo tangu historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine hii ni changamoto kwao kwamba hatu mkichagua Upinzani mnayo nafasi ya kupata maendeleo. Nalizungumza hili kwa sababu kuna watu wanahisi maendeleo ni itikadi. Lakini maendeleo ni ya wananchi wote kwa sababu wote ni walipa kodi wa Taifa hili na wana haki ya kupata maendeleo ndio sababu daraja linajengwa, barabara inajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani zangu hizo naomba nianze kwa kusema kwamba tunapojadili kupunguza umaskini wa Taifa hili ambalo kwa takribani miaka 50 tumeshindwa.

Ushauri wangu naomba tukubaliane kwamba sekta mama za kuzipa kipaumbele kubwa kabisa ni mbili, umeme na miundombinu. Leo tunazungumza hapa wataalam wa uchumi wametuambia asilimia 40 ya uchumi wa dunia unategemea nishati. Kwa hiyo, hauwezi ukaendeleza Taifa lolote lile kama hauna nishati ya uhakika. Hauwezi ukaendeleza Taifa lolote lile kama umeshindwa kuunganisha Taifa lako kwa maana ya miundombinu. Kwa hiyo, miundombinu na umeme ndio nguzo kubwa za kujenga uchumi mkubwa na baadaye ule uchumi uweze kutafsiri. Ule uchumi mkubwa (*macro economy*) iweze kusambaa kwa mtu mmoja au kwenye (*micro level*) kwenye uchumi mdogo mdogo. (*Makofi*)

Nakubaliana na sekta ya miundombinu kupewa kipaumbele na naona kwamba Bajeti yake pamoja na mapungufu yote lakini ni Bajeti ambayo kimsingi inatosha kama itasimamiwa vilivyo kuonyesha tofauti. Hoja yangu katika miundombinu ningeomba msukumo wa kwanza upelekwe kwenye reli kwamba tuanze na reli, kwamba ni aibu kwamba reli yao ni mbovu kuliko reli ya Uhuru, ni aibu miaka 50.

Kwa hiyo, yapo mambo mengi kwenye sekta ya miundombinu. Lakini nashauri tuanze na eneo la reli. Reli ya Kati Bajeti ya ni shilingi bilioni 240 sidhani kama itachukua muda mrefu kupatikana hiyo fedha. Ningeshauri kwamba tuanze na reli. Tukamilishe reli lakini pia tukamilishe Bandari ya Kigoma na Bandari ya Dar es Salaam. Unapozungumza Taifa hili kufaidika na jiografia yake unazungumza kwanza uwezekano wa kuifanya iwe na bandari yenye *capacity* ya kutosha. Lakini pia iwe na usafiri wa reli ya kati wa uhakika. Kwa sababu ni hii reli ya kati ambayo inakwenda kusaidia usafiri wa Watanzania na nchi jirani ambazo ni *land locked countries*, inatuunganisha na nchi ya Zambia, inatuunganisha na nchi ya Burundi, Rwanda na Congo. Ukiwa kule Kigoma Zambia unakwenda kwa meli, kwa hiyo, mizigo yote ya hizi nchi za Zambia, Burundi, Rwanda, Congo kutoka nchi zingine za Asia, Ulaya na Amerika zinaweza zikashuka Bandari ya Dar es Salaam zikasafirishwa kwa reli ya Kati, zikifika Kigoma zisambazwe kwa njia ya meli ambaa ni usafiri nafuu kuliko wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mizigo yote ya hizi nchi kwa maana ya Burundi, Rwanda na Congo ambayo inatakiwa isafirishwe kwenda Asia, Amerika na Ulaya itasafirishwa kwa meli Mkoa wa Kigoma kama bandari ya pale Kigoma tayari imeboreshwa vya kutosha na kwa hiyo, ikitokea Kigoma itasafirishwa mpaka Dar es Salaam na Dar es Salaam isafirishwe kwenda Ulaya, Asia na Amerika. Hivyo ndivyo

ambavyo tunaweza tukafaidi na kupakana na nchi ambazo hazina bandari na kama ajenda hii ikitekelezwa, mfaidikaji wa kwanza au mtu wa kwanza kufaidika itakuwa ni sisi watu wa Kigoma; kwa sababu Kigoma ndicho kitovu cha kupokea mizigo ya nchi nne kati ya tano ambazo ni *land locked countries* ambayo itapaswa kusafirishwa mpaka Dar es Salaam halafu iende Asia, Ulaya na Amerika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kigoma hiyo hiyo ndiyo kama reli ya kati imeboreshwa tutapata mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam kufika Kigoma, isafirishwe kwenda hizo nchi nne ambazo ni jirani na hazina bandari. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba ajenda hiyo ianze na reli, tufuate na bandari ya Kigoma na Dar es Salaam ili kusudi tuibadilishe Kigoma. Kigoma ina nafasi ya kuwa Dubai ndugu zangu, tuna ardhi ya kutosha tena yenyre rutuba. Tukiboresha reli ya kati na bandari hizi mbili tunao uwezo wa kuibadilisha na ikatoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa hili, sio kwa faida ya Kigoma tu, kwa faida ya Taifa hili, leo Kigoma inawalipa kodi elfu tano, Kigoma nzima, Mkoa mzima unawalipa kodi elfu tano tu ni aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kuonesha msisitizo na nasikitika sana kwamba pamoja na Waziri kuzungumzia uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya umeme, lakini Bajeti ya takribani shilingi bilioni 500, tusidanganyane haitoshi kufanya mapinduzi ya umeme, haitoshi kabisa na bado ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati nilikuwa nashauri kwamba sekta hii ya umeme kama tuliweza kutenga shilingi trilioni 1.7 kama *stimulus package* mwaka 2008, tungetazama madhara au athari za kukosa umeme, tungefika mahali tukakubaliana kabisa kwamba jamani hii sekta ya umeme hebu tuitengetee mfuko maalum kama *stimulus package* kwa ajili ya kufua umeme nchi hii. *Megawatt* mia nane miaka 50 ya Uhuru hatuwezi kusonga mbele, Bajeti ya shilingi bilioni 500 safari hii haiwezi kuonesha tofauti yoyote, haiwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashauri Mheshimiwa Waziri, lazima tuongeze Bajeti kwenye sekta ya umeme na tunavyozungumza kwenye Bajeti kuhusu sekta ya umeme, sio tu kuzalisha umeme, leo ni aibu Kigoma tunaambiwa kwamba tuna ziada ya umeme ni mambo ya aibu, Mkoa ambao tuna shida kubwa ya umeme eti tuna ziada ya umeme, ni kwa sababu watu wengi hawajawa *connected*, hamjaunganisha watu na umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuja Wamerekani Jimboni kwangu pale Uvinza, wanafanya utafiti, wakagundua kwamba wanaweza wakatengeneza kiwanda cha kuzalisha zaidi ya tani milioni moja ya simenti, lakini wanahitaji *megawatt* 24 za umeme. Mkoa mzima wa Kigoma unazalisha *megawatt* 11 tu za umeme. Kwa hiyo, kuna hasara ambazo zinatokea hatuzioni kwa sababu hatujafanya ule umeme uweze kufika maeneo ya uzalishaji.

Pale nyumbani Uvinza au Mkoa wa Kigoma tulikuwa na kiwanda ambacho kinazalisha chumvi bora Afrika Mashariki na ya Kati. Leo kimefungwa kwa sababu hakuna umeme na bahati mbaya labda niunganishe na hili sana baada ya mgodi ule

kufungwa *PVD plant* ambayo ilikuwa inazalisha chumvi kwa kutumia umeme, wale wawekezaji wa kihindi wameng'oa mitambo ya ile *plant* wanaiza nje, kwa kweli jambo hili ni kitu ambacho hatuwezi kukubaliana nacho. Lazima ifike mahala mtueleze kwenye ubinafsishaji mlikubaliana nini, mliuza kila kitu au mlikodisha tu kwa maana kwamba wazalishe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu amebinafsishiwa mgodi una *plant* tatu, moja ya kuzalisha chumvi kwa *solar* wanaanika kama bustani, nyingine kwa kuni ambapo wanatumia kuni kukausha maji ya chumvi na nyingine kwa umeme, *PVD*, ambayo ilijengwa kwa msaada wa pesa nyingi sana. Leo kabinafsishiwa mwekezaji tukitegemea kwamba ataongeza uzajalishaji na teknolojia, tuongeze ajira na biashara, tuongeze mapato ndani ya Taifa; anang'oa mgodi anauza mitambo yote nje, haiwezekani na Serikali inatazama tu, haiwezekani. Hatuwezi kukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi mgodi ule baada ya kuuzwa kuna wafanyakazi wamedai mafao yao, tangu mwaka 1998 mpaka leo hawajapata mafao yao, nasoma *documents* za Wizara ya Fedha wananiambia kwamba makampuni yale ambayo yalikuwa hayapeleki michango kwenye Mifuko ya Hifadhi, Wizara imepeleka pesa kule kwa ajili ya ku-compensate ili kusudi waweze kupata mafao yao mazuri wale ambao walikuwa watumishi kwenye migodi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Chumvi Uvinza tangu mwaka 1998 bado wameshindwa kupata mafao yao, wakati *PSRC* kabla ya *CHC* wakitangaza kubinafsisha mgodi ule walisema watatoa mkono wa kwaheri kwa wafanyakazi wa mgodi ule, toka mwaka 1998 mpaka leo watu wanakufa; yaani zaidi ya nusu hawapo tena, kweli?

Sasa haya ndiyo mambo ambayo wananchi wanalamika kwamba haiwezekani, ni lazima tuangalie upya eneo zima la ubinafsishaji, kuna mambo mengi ya hovyo katika eneo la ubinafsishaji. Tuangalie hii migodi ni ya kwetu, haiwezekani mbinafsisha na muuze kila kitu kwamba mtoe haki ya kuza kila kitu, tunabinafsisha kwa bei nafuu ili kusudi anayepewa mgodi ule auendeleze, aongeze ajira, aongeze *export* tuweze kukuza uchumi, hatubinafsishi mtu awe na uamuzi wa kwenda kufanya chochote kuhusu ambacho amepewa, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza kwamba Bajeti ya Tanzania kwa muda mrefu imebaki kuendelea kuwa tegemezi.

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, muda umekwisha. Msemaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza nikiwa kama mzungumzaji wa mwisho kwa jioni hii ya leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuiunga hoja mkono kwa sababu nimesoma vizuri mpango wetu uliopo mbele yetu, lakini nimeisoma vizuri Bajeti yetu ya mwaka 2011/2012, ni Bajeti ambayo nimehisi kabisa kama kutakuwa na utekelezaji mzuri wananchi wetu wanaweza wakapata unafuu wa maisha. Nazungumza hivyo juu ya kipengele cha kupunguza bei ya mafuta; tumekuwa tukishuhudia wananchi wetu wakilalamika juu ya upandaji wa gharama ya bidhaa mbalimbali, lakini ukiangalia msingi wake mkubwa ni juu ya kupanda gharama za mafuta. Sasa kama kweli tutapitisha Bajeti hii na gharama za mafuta zikapungua, nina amini kabisa wananchi wetu watanufaika kabisa katika kuondokana na kupanda kwa maisha ambako kuko hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoiomba Serikali katika suala hili la kupanda kwa gharama za mafuta, tukipunguza wananchi wale ambao walikuwa wamepandisha bidhaa mbalimbali na zenyewe zishuke kwa sababu Watanzania tumekuwa na utaratibu gharama zikipanda kwa ajili ya sababu fulani kama hii ya kupanda gharama za mafuta, hata ikishuka bado bei ya bidhaa zinabakia pale pale. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali isimamie kabisa kwamba gharama za mafuta zitakaposhuka na bidhaa zetu kwa mfano bidhaa za vifaa vya ujenzi, bidhaa mbalimbali kama bei ya sukari, tuangalie na tuhakikishe kwamba zinashuka.

Vilevile hata gharama za usafiri, sasa hivi wananchi wetu wanapata gharama kubwa sana wanapotaka kusafiri na hata wananchi wetu wengine wamekuwa wakipoteza maisha kwa kushindwa gharama za usafiri kwa kuwasafirisha wagonjwa kwenda kwenye mahospitali. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kama kweli tuna lengo ya kuwasaidia wananchi tusimamie vilevile katika kuhakikisha kwamba bidhaa zinapungua bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulichangia ni suala la miundombinu. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo inafanya kuhakikisha kwamba miundombinu hasa ya barabara zinaunganika Mkoa hadi Mkoa, tofauti na miaka mitano au kumi iliyopita, lakini katika hili, mimi nilikuwa naiomba Serikali, sisi watu wa Mikoa ya Kusini tumepeata shida miaka mingi sana kwa ajili ya kutokuwa na barabara ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya jitihada za kuhakikisha kwamba tunapata barabara ya uhakika kutoka Dar es Salaam hadi kufika Mtwara, lakini ni masikitiko yangu makubwa ni kwamba, kazi ilianza vizuri sana, lakini huku mwishoni inakotaka kumaliza kufanya kazi hiyo, kilomita 60 zimekuwa zikisumbua, hazina hata uhakika zitaisha lini. Naomba Serikali ihakikishe kwamba kilomita 60 zilizobakia zinaisha mwaka huu ili na sisi watu wa Mikoa ya Kusini tuweze kunufaika na barabara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisisitiza hilo kwa sababu kama kuna maeneo ambayo bidhaa zinauzwa bei mbaya ni Mikoa ya Kusini na wafanyabiashara

ukiongea nao wanakuambia tunashida sana kwa ajili ya matatizo ya barabara. Kwa hiyo, naomba sana Serikali isimamie na ihakikishe kwamba kilomita hizi 60 mwaka huu zinaisha, tuache zile hadithi za kwamba tutamaliza barabara hii baada ya miezi fulani. (*Makofi*)

Vilevile katika miundombinu, naomba nitoe masikitiko yangu makubwa. Serikali iliamua kufanya ukarabati wa jengo la abiria kwenye uwanja wa ndege wa Mkoa wa Mtwara, lakini kwa masikitiko makubwa nashangaa kila Bajeti ikifika fedha zinatengwa kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo, lakini sasa hivi ni takribani karibu miaka minne na zaidi, jengo hili halikamiliki, je, fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukarabati wa jengo hili zinaenda wapi? Naomba Serikali tunapopanga mipango yetu kwa ajili ya kumaliza tatizo fulani basi tuwe na usimamizi mzuri ili tuweze kumaliza tatizo moja na baadaye tuweze kwenda katika tatizo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopanga mipango kila mwaka unatenga fedha kwa ajili ya mpango fulani na mpango huo haukamiliki, tunachelewa kupanga miradi ya maendeleo mingine. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ituambie kwa nini jengo hili linachukua miaka mungi bila kukamilika na wakati Serikali kila mwaka inatenga fedha. (*Makofi*)

Vilevile, nataka kujua katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 fedha zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama katika maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye Wilaya ya Masasi Kata ya Lukuledi ilitengewa fedha za kujenga Mahakama pamoja na nyumba ya hakimu na kwa kumbukumbu zangu zinanionesha kwamba si Lukuledi peke yake ambayo ilikuwa imetengewa fedha hizo, kulikuwa na Wilaya zingine vilevile walitengewa fedha, lakini hadi leo ujenzi huu haujakamilika. Maagizo waliyopewa wananchi kwa nafasi zao wameshatekeleza, Serikali inasubiri nini kupeleka fedha hizi na ujenzi wa Mahakama ukaanza kujengwa? Naomba nipate jibu wakati Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unatoa majumuisho, Mahakama hizi zitajengwa lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niende kwenye suala la Serikali za Mitaa. Kwenye Serikali za Mitaa ndiyo kitovu cha maendeleo ya wananchi wetu vijijini, lakini tumekuwa tukishuhudia hivi karibuni karibu kila Mbunge anayesimama hapa amekuwa akilalamika sana juu ya utendaji mbovu uliopo kwenye Halmashauri nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningiomba Serikali ingefanya utafiti wa kuangalia Halmashauri zetu, wale watendaji wabovu ambao wanashindwa kusimamia shughuli za maendeleo ya wananchi, hawana sababu ya kuendelea kuwepo, wanachelewesa shughuli za maendeleo ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia sasa hivi hawa vijana wetu wanaopata ajira, anakuja kuanza lakini baada miezi sita ana nyumba sita, ana magari kumi, fedha hizi wanazitoa wapi? Mimi ningiomba Serikali iangalie upya juu ya wale watendaji wabovu, tuwe na watendaji ambao kwa kweli watakuwa tayari kuisimamia na kuitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nazungumzia suala la Serikali za Mitaa, naomba nizungumzie vilevile juu ya maslahi ya Madiwani. Mimi binafsi nimekuwa Mbunge toka kipindi kilichopita, nimekuwa nikisikia michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ndani ya Bunge wakilia na kuwatetea Waheshimiwa Madiwani waweze kufikiriwa kupatiwa mishahara. Sasa naomba niiambie Serikali, ukiona Wabunge wengi wanasimama humu ndani, wanaishauri Serikali kwa jambo fulani, mjue kwamba hapo pana jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Waheshimiwa Madiwani, wao ndiyo wasaidizi wetu katika kutekeleza shughuli zetu, Serikali ni kwa nini inashindwa kusikiliza kilio cha Waheshimiwa Wabunge ikafikiria kuwalipa mishahara hao Waheshimiwa Madiwani. Lakini vilevile tuna mpango mzuri sana wa kupeleka ruzuku vijijini, naomba kujua kwa nini sasa kwa kipindi kirefu Serikali imeacha kupeleka fedha za ruzuku kwenye vijiji vyetu kwa sababu ruzuku vijijini ndizo zilizokuwa zinasaidia na kuleta changamoto katika miradi yetu ya maendeleo, lakini hivi sasa ruzuku haziendi, wananchi wamekuwa tu wakichangia wao wenyewe, naomba kujua kwa nini ruzuku za vijiji zimesimama na haziendi vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie vilevile suala la elimu. Tumeona katika mpango wetu huu au katika Bajeti yetu imeazimia kwamba Serikali itaongeza kujenga Vyuo kwenye Wilaya zetu hasa Vyuo vya VETA, lakini vilevile tumekuwa tukishuhudia jinsi Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilivyoona umuhimu wa kuongeza vyuo katika nchi yetu, ni masikitiko makubwa sana na mimi naomba niungane mkono na wezangu ambao walitangulia kuchangia kwa kuizungumzia migomo inayoendelea.

Waheshimiwa Wabunge, mimi ninachotaka kuzungumzia hapa juu ya migomo ni kwamba tumepata bahati kuwa na Chuo chetu Kikuu cha Dodoma na tumekuwa tukipata bahati mara nyingi sisi Wabunge tumekuwa tukiwa hapa Dodoma, nilichokuwa ninakitarajia mimi, sisi hapa ni mkusanyiko wa Wabunge kutoka maeneo mbalimbali, tungekuwa tunautumia muda wetu mwangi kuhakikisha kwamba vijana wetu waliotoka katika maeneo yetu tunawapa ushauri mzuri, tunawaelekeza, tunawasaidia, ili waweze kusoma vizuri na hatimaye waweze kupata *degree* zao waende wakatutumikie huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe Wabunge tumekuwa tukilalamika kwamba tunakosa wataalamu mbalimbali katika Wilaya zetu, sasa nashangaa tunapokuja hapa, sisi wenyewe ndiyo tukawe washawishi wakubwa kuwashawishi watoto wetu wawe wanaingia katika migomo kila siku, hawasomi, hawa wataalamu tunaosimama humu tukililia, tutawapata kutoka wapi? Kwa sababu siku ya siku itakapofika, hawa watoto kila siku wanafanya maandamano, migomo, hawasomi, siku ya siku ikifika matokeo yake hawatafanya vizuri katika mitihani, watarudi vijijini. Lakini vilevile niwaombe wazazi wenzangu, naamini kabisa sasa hivi tumeshuhudia watoto wetu wamerudishwa majumbani. Hebu tukae na watoto wetu tuwaelimishe, watoto wetu tuwashauri kwamba walicho jia Dodoma ni kuja kusoma kwa ajili ya maendeleo yao ya kesho na kesho kutwa na wala si kuja kufanya migomo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina amini kabisa wazazi walio wengi hawajabahatika kuja Dodoma, ninachotaka kuwaambia ni kwamba hawa watoto wetu kama tutakaa, tukawashauri, wakatusikia kwa sababu sisi ndiyo wazazi, waachane na ushawishi wanaopewa, kwa sababu wanaowashawishi wenzao wana maisha yao, wanajitegemea, hawana wasiwasi wa aina yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao sasa hivi wapo katika safari ya kutafuta maisha, waje Chuoni kwa ajili ya jambo la kutafuta elimu yao kwa manufaa ya kesho na kesho kutwa na kwa vizazi vijavyo, kwa sababu sisi tunawategemea wao watakapomaliza chuo, ndiyo watakuwa madaktari wetu, ndiyo watakuwa watendaji wetu katika Halmashauri zetu mbalimbali kwa ajili ya kusimamia shughuli za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme, naomba nirejee tena kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa jinsi ambavyo walisimamia kuhakikisha kwamba sisi watu wa Mikoa ya Kusini tunatafutiwa na kuchimbiwa ule umeme wa gesi na hivi karibuni nimekuwa nikisikia kwamba umeme ule utakuwa na utaratibu wa kuletw Dar es Salaam, mimi napongeza utaratibu huo, lakini ninachoomba Serikali katika hili na sisi watu wa Mikoa ya Mtwara na Lindi...

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante sana.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za leo nina matangazo yafuatayo.

Kwanza wachangiaji wa kesho asubuhi wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Jitu Soni, wa pili atakuwa Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Christina Mughwai na wengine watatangazwa kesho. Lakini la pili ni kuhusu Muongozo niliotakiwa kuutoa na Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Miongozo, Taarifa au Taratibu ina *base* kwenye Kanuni yetu ya 68 na vifungu vyake vinavyofuatia. Mheshimiwa Mbunge alipotaka Mwongozo, hakujiweka katika Kanuni yoyote ile kwa vile mimi kama Mwenyekiti nashindwa kutoa msimamo kuhusu ombi lake kwa vile yejote yule atakaetaka kuuliza a-*base* katika Kanuni kutohana na Kanuni zetu hizi. (*Makofi*)

Baada ya hapo naomba kusitisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi, ahsanteni sana. (*Makofi*)

(*Saa 1.42 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*

Tarehe 21 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)